

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 26 Mei, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Kamili Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa mwisho, Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha leo ni cha Thelathini na Sita.

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 336

**Kudhibiti Ufanyaji Biashara Holela Nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Zoezi la kuwapatia vitambulisho wajasiriamali wamachinga limefanyika vizuri na kuendelea kufanya biashara zao mahali popote.

Je, Serikali imejipanga vipi ili kuhakikisha kuwa na usimamizi na udhibiti katika ufanyaji wa biashara holela?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imetunga Kanuni za Usimamizi wa Kodi (Usajili wa Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma) za mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Kanuni hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeelekezwa kusimamia na kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara na watoa huduma Wadogo ili kuhakikisha biashara holela zinadhibitiwa. Udhubiti na usimamizi utafanyika wakati wa kusajili na kuwapatia vitambulisho wajasiriamali wadogo kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi na kuhakikisha wanaendesha shughuli zao pasipo kubugudhiwa. Sambamba na Kanuni hizo, Serikali imeandaa mwongozo wa usimamizi wa Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo ambao umeainisha majukumu ya kila mdau katika usimamizi wa Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo.

Na. 337

**Uhaba wa Maji – Kata za Mtimbira na Usangule**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Wakazi wa Kata za Mtimbira na Usangule zenye vijiji saba na idadi ya watu 70,000 wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa utekelezaji katika kutatua changamoto hiyo ya uhaba wa maji kwa wakazi wa vijiji hivyo saba katika muda mfupi na muda mrefu?

**WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Jimbo la Malinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Mtimbira na Usangule zinapata huduma ya maji kupitia mradi wa maji kutoka Mto Munga. Hata hivyo, mto huo umekubwa na changamoto za kupungua kwa wingi wa maji kipindi cha kiangazi hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma ya maji.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imechukua hatua za dharura kwa kuchimba visima virefu nane na kufunga pampu za mkono. Visima vitatu (3) kati ya visima hivyo vimeonekana kuwa na maji mengi na hivyo vitaendelezwa kwa kujenga miundombinu ya kusambaza maji ya bomba katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuhakikisha huduma ya maji inaimarika Serikali inaendelea na usanifu kwa ajili ya kufanya ukarabati na kuongeza upatikanaji wa maji kwa kutumia visima na kujenga miundombinu ya maji katika Kata ya Mtimbira na Usangule. Utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa kutumia wataalam wa ndani (*Force Account*). Aidha, shirika lisilo la kiserikali la *Help for Underserved Communities (H.U.C)* limesaini makubaliano na Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi kusaidia uchimbaji wa visima virefu 50 ambapo kati ya hivyo vinne vitachimbwa katika vitongoji vilivyo pembezoni mwa kata ya Mtimbira vya (Nganawa) na Usangule (Mipululu).

Na. 338

**Hitaji la Pampu ya Maji-Kijiji cha Kasanda-Kakonko**

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA** aliuliza:-

Shirika linaloshughulikia wakimbizi lilichimba kisima cha maji katika Kijiji cha Kasanda kwa ajili ya kuwahudumia

wakimbizi wanaoishi Kambi ya Mtendeli. Maji yanayopatikana yanatosha kuhudumia sehemu ya kijiji cha kasanda ambacho tayari kina baadhi ya miundombinu ya kuhifadhia maji kama tanki.

Je, kwa nini Serikali isifanye mazungumzo na wakuu wa makazi ya wakimbizi ili wagharamiwa kufunga pampu na kusambaza maji katika Kijiji cha Kasanda kwa gharama nafuu?

**WAZIRI WA MAJI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Injinia Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanya jitihada kubwa katika kuhakikisha kuwa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi katika kijiji cha kasanda inatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *Water Mission* imetekeleza mradi wa maji safi na salama ulioanza kutekelezwa mwezi Desemba, 2017 na kukamilika mwezi Aprili, 2018 kwa gharama ya shilingi milioni 227. Mradi huu unazalisha lita 96,000 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji halisi ya lita 296,827 kwa Kijiji cha Kasanda. Mradi huu unahudumia sehemu ya Kijiji cha Kasanda na maeneo machache ya Vijiji vya Kewe na Nkuba.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uhitaji mkubwa wa maji uliopo katika Kijiji cha Kasanda, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wakuu wa makazi ya wakimbizi ili kujiridhisha na wingi wa maji katika kisima hicho kilichochimbwa ili kuona kama kinaweza kuhudumia wananchi wa Kijiji cha Kasanda ndipo utaratibu wa kuweka miundombinu ya kusambaza maji ufanyike.

Na. 339

**Kuhamasisha Zao la Kahawa Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Uzalishaji wa kahawa umeshuka sana katika maeneo mengi nchini hasa Kilimanjaro na Arusha hali iliyopelekea umasikini kuongezeka katika maeneo hayo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha wakulima wa kahawa katika mikoa hiyo kufufua mashamba hayo?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti maaalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa kahawa kanda ya kaskazini umeshuka kutoka tani za kahawa safi 6,706 mwaka 2014/2015 hadi tani 5,882 mwaka 2018/2019. Kushuka huko kumetokana na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na kupungua kwa maeneo ya uzalishaji uliosababishwa na ongezeko la watu, kubadilishwa matumizi ya maeneo ya kilimo cha kahawa kwa ajili ya makazi, utalii na uzalishaji wa mazao mengine kama mboga mboga na matunda. Sababu nyingine ni kubadilika kwa vipindi vya mvua na kusababisha ukame ambao umechangia kukwama kwa shughuli za umwagiliaji pamoja na kuzorota kwa ushirika wa *KNCU* ambao ndio ulikuwa muhimili wa uzalishaji wa kahawa katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo kuhamasisha kilimo cha kahawa Arusha na Kilimanjaro ikiwa ni pamoja na kufufua na kujenga upya ushirika wa *KNCU* ili uweze kutoa huduma kwa wakulima kama ilivyokuwa hapo awali. Katika kutekeleza hili Serikali imeongeza usimamizi

katika shughuli za Vyama vya Ushirika na kuwachukulia hatua za kisheria viongozi wote waliofanya ubadhilifu na kusababisha hasara kwa vyama vya ushirika, uhamasisha upandaji wa miche bora ya kahawa ambayo inazaa mapema na ina ukinzani wa magonjwa ya kahawa. Matumizi ya miche hii yanapunguza gharama za uzalishaji kwa karibu asilimia 50 hivyo kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na kuongeza faida ya kilimo cha kahawa.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kuendelea kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (*TaCRI*) ili kuendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani walioko kwenye kata na vijiji vinavyozalisha kahawa kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa kutoa huduma bora kwa wakulima wanaozalisha kahawa na kuimarisha sekta binafsi katika kuhamasisha uendelezaji wa ubora na masoko ya kahawa kama vile kuwezesha wakulima kufikia viwango vya kusajiliwa katika taasisi za ubora wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, ni matumani ya Serikali kuwa hatua hizi zinazochukuliwa zitachochea ufufuaji wa zao la kahawa katika mikoa hiyo na katika maeneo mengine yanayolima kahawa nchini kwa kuwa zao la kahawa ni moja ya mazao ya kimkakati yaliyoainishwa na Serikali.

Na. 340

### **Sekta ya Kilimo Kuajiri Vijana**

**MHE.VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu na ni sekta ambayo inaajiri watu wengi zaidi:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba vijana wengi wanaweza kujajiri katika sekta hii ya kilimo?

(b) Je, ni kwanini vijana wanaoijiunga na JKT wasitumie muda mwingi kuzalisha mazao ya kilimo ili wapate mitaji ya kuendesha maisha yao?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza sera, programu na mikakati mbalimbali inayohusu ushirikishwaji wa vijana katika kilimo. Katika jitihada hizo, Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Kitalu Nyumba unaolenga kutoa mafunzo yatakayoweza vijana kupata ujuzi wa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba ili kuongeza tija na kuvutia vijana wengi kujijiri. Kupitia Mradi huo, imejenga vitalu nyumba 84 katika Halmashauri 81 za mikoa 12 ambapo vijana 8,700 wamepewa mafunzo. Ujenzi wa vitalu nyumba na mafunzo katika mikoa 14 iliyosalia ipo katika hatua za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 4 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo inahamasisha vijana kujiunga katika vikundi ili kupata mikopo hiyo. Pia, kuhusu upatikanaji wa ardhi, Serikali imezielekeza Serikali za Mitaa na Vijiji kutenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya vijana. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la *SUGECO* chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (*SUA*) Serikali imefundisha vijana 1,000 katika vituo atamizi vya Mikoa ya Morogoro na Pwani kuhusu kilimo biashara, uzalishaji na ujasiriamali. Kati ya vijana hao, vijana 225 wamekwenda Israel na 105 wamekwenda Marekani kwa ajili ya kuongeza ujuzi zaidi kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliitisha makongamano ya vijana katika Kanda sita nchini yaliyofanyika tarehe tofauti baada ya Kongamano moja la kilele kuahirishwa kutokana na tatizo la ugonjwa wa Corona. Makongamano hayo yalihudhuriwa na vijana takribani 2,100 ambao wamejadili namna bora ya kutumia fursa zilizopo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo na kubadilishana uzoefu wa shughuli za kilimo. Wizara imeandaa taarifa yenye maazimio yote yaliyojitokeza katika makongamano hayo pamoja na

Mpango Kazi wa utekelezaji wa maazimio hayo kwa ajili ya kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, lengo la mpango wa kuwapeleka vijana makambini JKT si kuwapa mitaji, bali ni kuwapatia maarifa mbalimbali ya stadi za kazi na maisha kama kilimo, ufugaji, uvuvi na ufundi wa aina mbalimbali hivyo muda mwingi hutumika kuwafundisha masomo hayo kwa nadharia na vitendo. Maarifa wanayopata huwasaidia kuendesha maisha yao baada ya kumaliza mkataba.

Aidha, hupewa mafunzo ya uzalendo ili wawe raia wema na walenzi wa taifa lao. Nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine kupitia halmashauri zetu tunapoteua vijana kwenda JKT tuwaandalie mipango madhubuti ya kuwapokea vijana wanapomaliza mikataba yao ili waweze kuendeleza ujuzi walioupata.

Na. 341

### **Kudhibiti Vitendo Viovu Magerezani**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia vitendo viovu na vibaya Magerezani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza ni chombo pekee cha Serikali chenye dhamana Kisheria kuwapokea na kuwahifadhi wahalifu wa aiana zote wanaoletwa Magerezani kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Pamoja na ukweli kwamba nyakati kadhaa kumekuwepo na vitendo viovu magerezani mathalani askari kuwa na



mahusiano mabaya na mfungwa (*Trafficking*) uingizaji wa vitu visivyoruhusiwa magerezani, matumizi mabaya ya nguvu dhidi ya wafungwa, wafungwa kujaribu kutoroka, kupigana, kutoeleana lugha za matusi, kuharibu mali ya gereza na kadhalika. Vitendo hivyo vimekuwa vikidhibitiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo za magereza nazo ni:-

(i) Sheria ya Magereza ya Mwaka 1967 (*The Prison Act of 1967*);

(ii) Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Magereza za Mwaka 1997 (*The Prisons Service Regulations of 1997*);

(iii) Kanuni za makosa Magerezani (*The Prison (Prison Offences Regulations)*);

(iv) Kanuni za kudumu za Jeshi la Magereza, Toleo la 4 la Mwaka 2003 (*Prisons Standing Order*).

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria na kanuni tajwa zimeainisha aina ya makosa, hatua na adhabu zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya afisa/askari wa magereza na mfungwa/ mahabusu pale inapothibitika amefanya vitendo hivyo gerezani.

Mheshimiwa Spika, hivyo, mpango ambao Serikali kupitia Jeshi la Magereza imekuwa nao ni kuongeza vifaa vya upekuzi magerezani (*ditectors*) na kufunga CCTV – Kamera Magerezani ili kubaini matendo maovu pia kuendelea kufuata sheria na kanuni tajwa ambazo zilipitishwa na Bunge lako tukufu na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaohusika na kufanya vitendo viovu magerezani.

Na. 343

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Wilaya ya Karatu**

**MHE. QAMBALO W. QULWI** aliuliza:-

Vijiji vya Chemchem, Kinihe, Makhromba, Endamaghang, Mikocheni, Gidbaso, Sumbechand, Matala na Endesh vyenye jumla ya vitongoji 46 Wilayani Karatu havijafikiwa kabisa na umeme.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji hivyo?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya vijiji 16 vya Wilaya ya Karatu vinatarajia kupatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza unaoendelea. Kazi za mradi zinajumuisha ujenzi wa kilomita 58.94 za njia za umeme msongo wa kilovoti 33; kilomita 74 za njia za umeme za msongo wa kilovoti 0.4; ufungaji wa transfoma 37; pamoja na kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja wa awali 1,096. Gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 5.016.

Mheshimiwa Spika, vijiji 14 vilivyobaki vikiwemo Vijiji vya Chemchem, Makhromba, Endamaghang, Mikocheni, Gidbaso, Sumbechand, Matala na Endesh vitapelekewa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili unaotarajia kuanza kutekelezwa mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Na. 344

### **Kupanga Bei Elekezi kwa Mazao na Mifugo**

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Bei ya mifugo inayumba kila wakati kwa sababu ya viangazi virefu vinavyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kupanga bei elekezi kwa kilo za mifugo akiwa hai au nyama kama ilivyo kwa mazao ya kilimo mfano Pamba, Kahawa na Korosho?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bei za mifugo zimekuwa zikiyumba sana kutokana na kudhoofu kwa mifugo wakati wa kipindi cha kiangazi kirefu kinachojitokeza sehemu nyingi hapa nchini, kwa kuwa kiangazi hicho kinaambatana na uhaba mkubwa wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo. Kukosekana kwa malisho na maji kunadhoofisha afya za mifugo na kupunguza ubora wake hivyo kushusha thamani ya mifugo hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa biashara ya mifugo unaotumika hapa nchini ni mfumo wa soko huria, ambapo bei ya mifugo hupangwa kutokana na nguvu ya soko inayotokana na kiasi cha bidhaa au ubora wa bidhaa zilizopo sokoni na mahitaji ya walaji. Katika biashara ya mfumo huo, kuingiliwa kwa namna yoyote ya uendeshaji wa biashara hiyo kwa kuweka bei elekezi kunapingana na dhana ya soko huria na kunavuruga utaratibu na kusababisha mtikisiko na hivyo kupoteza mwelekeo wa hali ya biashara. Kufanya hivyo, kunaweza kuchochea kuwepo kwa biashara zilizo kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za masoko jambo ambalo sio rafiki kwa uchumi wa nchi na afya za walaji. Kwa mazao ya mashambani tofauti na mifugo, kiangazi huathiri zaidi kiwango (wingi) wa mazao hayo na kwa kiasi kidogo ubora wake. Aidha, mazao yaliyotolewa mfano na mheshimiwa Mbunge (Pamba, Kahawa na Korosho) ni mazao ya biashara ambayo hali ya soko lake ni rahisi kukisia kwani inaamuliwa na bei ya soko la kimataifa tofauti ya mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na athari za ukame kwa mifugo, Wizara ikishirikiana na wadau mbalimbali

inaendelea kutekeleza Mkakati wa Upatikanaji wa Malisho na Maji pamoja na kukamilisha maandalizi ya Miongozo ya usimamizi wa rasilimali hizo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imewezesha elimu ya uzalishaji wa malisho kwa vitendo katika Halmashauri 11 ambapo, jumla ya mashamba darasa 25 ya malisho yameanzishwa na wafugaji 685 wamepata elimu ya kilimo cha malisho kwa vitendo.

Aidha, Wizara inatekeleza hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa malambo matatu (3) katika vijiji vya Chamakweza (Chalinze), Kimokoa (Longido) na Narakauo (Simanjiro) na ukarabati wa malambo matatu (3) katika vijiji vya Kimana (Kiteto), Narakauo (Simanjiro) na Kimokoa (Longido). Pia, Wizara imechimba visima virefu viwili (2) katika Vijiji vya Mpapa (Manyoni) na Nsolanga-Ismani (Iringa).

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuweka mkazo wa kuuza na kununua mifugo minadani kwa kutumia mizani ili kumwezesha mfugaji kupata bei nzuri yenye tija, uwazi na ushindani sokoni. Wizara imesimika mizani katika minada kumi na moja (11) ya upili na mipakani na kuagiza Halmashauri kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kuhakikisha minada yote ya awali inasimikwa mizani ili kuwezesha wafugaji na wafanyabiashara kupanga bei kulingana na uzito wa mnyama.

Na. 345

### **Matumizi Mabaya ya Mitandao ya Kijamii**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya mitandao ya kijamii kama vile uchochezi, upotoshaji, udhalilishaji na kadhalika.

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imechukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuweka mazingira salama kwa wananchi hususan kwenye mitandao. Mwaka 2015 Serikali ilitunga Sheria ya Miamala ya Kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimtandao; na Sheria ya Makosa ya Mitandao kwa lengo la kutambua kisheria makosa yanayofanyika kwenye mitandao ili kuweza kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo. Pia katika kujenga mazingira salama ya kisheria, Serikali iko kwenye mchakato wa kutunga Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi ambayo lengo kuu ni kuweka utaratibu wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi ili kupunguza matumizi mabaya ya taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Kitengo cha Uhalifu wa Mitandao (*Cybercrime Unit*) chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya mitandao ikiwemo uchochezi, upotoshaji, udhallishaji na kadhalika mtandaoni na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Kurugenzi ya Mwendesha Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ilianzisha Kitengo cha uratibu, ufuatiliaji na usimamizi wa matukio yanayotokea kwenye anga ya mtandao (*TzCERT*) ambayo iko chini ya Mamlaka ya Mawasiliano. Kitengo cha *TzCERT* kinashirikiana kwa ukaribu na Taasisi nyingine za hapa nchini, Taasisi za Kikanda na Kimataifa kupeana taarifa za kiintelijensia kuhakikisha anga ya mtandao inakuwa salama. Aidha, Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Mitandao wa mwaka 2018 ambao unaweka bayana mikakati ya kukabiliana na uhalifu wa mitandao. Serikali itaendelea kujengea uwezo watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama wa kukabiliana na matukio ya kimtandao, kuweka mifumo thabiti ya kukabiliana na matukio ya kimtandao, kuboresha mazingira ya kiudhibiti ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa matumizi mabaya ya mitandao

hususan mitandao ya kijamii na kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mitandao.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Kama mtakumbuka mara ya mwisho tulipokutana hapa tulikubaliana kwamba leo ndiyo tutahitimisha mjadala wetu kuhusiana na hoja iliyowekwa mezani na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Kwa hiyo mjadala unaendelea na tunaanza na Mheshimiwa Balozzi Adadi Rajab na watakaofuata nitawataja.

**MHE. BALOZI A. MOHAMED RAJAB:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza leo baada ya kutoka kwenye sherehe za sikukuu za *Eid al-Fitr*. Ningependa kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na mapendekezo mbalimbali ambayo wameyatoa. Kabla ya hapo ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa busara zake nzuri ambazo amezitoa kuhusiana na masuala mbalimbali ya ugonjwa huu wa (*Covid 19*), lakini hususani kwa maelekezo sahihi ya aliyoyatoa hivi karibuni kuhusu mipaka yetu. Ni uamuzi wa busara ambao kwa kweli ungeweza kuleta matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Ma-RC hususani RC wangu Mheshimiwa Shigela ambaye pia alifanya maamuzi ambayo ni sahihi kabisa, wanadiplomasia

kufuatana na *Vienna Convention ya diplomatic immunities* na *International relations*, wanasema NI for NNI, sasa tumechokozwa tumefunga mipaka na tumekuja kwenye *negotiations*. Kwa hiyo maamuzi ya Mheshimiwa Rais ni ya kupongezwa sana kwa sababu nchi jirani zote sisi tunategemeana kwa mambo mbalimbali hasa ukiangalia kwa mfano wananchi wangu wa Muheza walipata matatizo makubwa sana baada ya machungwa yao kuoza na kuharibika kwa sababu Kenya, Mombasa ni wateja wetu wakubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana CAG Mheshimiwa Kichele kwa kazi nzuri ambayo ameanza kuifanya, ukaguzi wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na anafanya ukaguzi mzuri sana na taarifa ambayo anaitoa kwa Mheshimiwa Rais kila mwaka ni taarifa ambayo inaibua mambo mengi ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Taarifa hii ukiangalia kwa ujumla wake utaona imegawanyika kwenye mambo mawili makubwa, kwanza taarifa za kiutawala; na pili taarifa ambazo zinamwelekeo wa makosa ya kijinai. Sasa Mheshimiwa Rais anapokabidhiwa taarifa hii ya CAG mara nyingi zile zinazohusu mambo ya utawala anayatolea maamuzi palepale na amekuwa akifanya hivo kuonyesha namna gani ambapo anachukia masuala ya ufisadi, uzembe na utumiaji wa fedha za Serikali kwa manufaa ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo ambalo naliona ni kwenye hii *part* ya pili ya tuhuma ambazo zimeibuliwa na CAG ambazo zina mwelekeo wa kijinai. Hapa naweza kuona kwamba kuna matatizo kwa sababu kuna makosa mengine ambayo ni ya kijinai ambayo kwenye taarifa yanaokana kwamba ni *straight forward* ni makosa labda ya wizi, ya *conspiracy*, au labda ya uzembe ambayo ukiangalia ni makosa ambayo yanakwenda moja kwa moja ambayo yanatakiwa yashughulikiwe na Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi imekuwa kwamba taarifa yote hii pamoja na matatizo yote haya ambayo yanaibuliwa yote yanakabidhiwa TAKUKURU. Kwa hiyo

yanapofika TAKUKURU wanakuwa na mzigo mkubwa na mambo mengi ya kuweza kushughulikia tuhuma hizi, wakati tuhuma hizi zingeweza kugawanywa zile ambazo zinaonekana kwamba zinahusika na Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, ziende kule na zile ambazo zinahusiana na mambo ya rushwa ziweze kushughulikiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa.

Mheshimiwa Spika, huu mkanganyiko unafanya tuhuma ambazo zimebuliwa zisiweze kushughulikiwa kwa haraka kwa sababu unapopeleka taarifa yote kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU inamaana makosa mengi ambayo yako kwenye Sheria ya TAKUKURU yanakwenda yanaambatana na uhujumu uchumi. Yanapoingia kwenye uhujumu uchumi usikilizaji wake unakuwa ni mrefu, kwa sababu kwenye taarifa hii utaona kwamba kuna malipo, kwa mfano malipo ya ziada ambayo yamefanyika kwenye baadhi ya mashirika; kuna *misappropriations* ambazo zimefanyika ambazo unaziona; kuna uzembe ambao umefanyika ambao unauona; ambayo haya yote ni makosa ambayo ni *direct* yanaweza kushughulikiwa na *Penal Code*.

Mheshimiwa Spika, yapo makosa mengine kama usipofuata taratibu sahihi za manunuzi ambazo zina harufu ya rushwa, mikataba mibovu ambayo ina harufu ya rushwa, ambayo ni mambo ambayo ni moja kwa moja yanakwenda kwenye Taasisi yetu ya Kuzuia Rushwa. Kwa hiyo nashauri kwamba siku zijazo mambo kama haya, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, ripoti zile zinapokabidhiwa wakae pamoja waweze kuchambua ni kitu gani hii iende huku na hii iende huku, basi ufanisi unaweza kuwa wa haraka zaidi. Pia ni vizuri tukaweka utaribu kwamba wakati anapoiwasilisha taarifa hii kwa Mheshimiwa Rais, basi pawepo na taarifa (*metrics*) inayoonyesha tuhuma ambazo zimebuliwa mwaka huu zimeshughulikiwa namna gani na vyombo vyetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye taarifa hii utaona kwamba kampuni ya *TTCL*, inadaiwa karibu bilioni 11, mtu unajiliza kampuni kubwa kama hii ambayo inafanya



biashara mbalimbali itadaiwaje fedha zote hizo. Sasa hapa kuna kitu ambacho kinatakiwa kifanyike kwa uangalifu zaidi ili kuweza kujua kwamba mashirika yetu haya tunayalea namna gani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano *NIDA*, hivi unafanya kazi na Taasisi nyingine lakini huna mikataba, kuna kazi nyingi ambazo utaona kwamba wameikosha mapato Serikali kwa sababu ya kuingia kufanya kazi bila kufuata taratibu. Sasa vitu kama hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa vichukuliwe kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *TPA* inafanya kazi nzuri sana, shehena za mizigo zimeongezeka, zimepamba moto kule, lakini sasa mfumo ambao wameuweka wanaouita *TPA billing system* imeleta dosari nyingi sana, pale kuna dosari karibu bilioni mbili. Sasa ni vitu ambavyo vinatakiwa viangaliwe na viweze kushughulikiwa kwa upana zaidi. Naamini kabisa hiyo tume ambayo Kamati ambayo imetengenezwa na *CAG* kwa ajili ya kushughulikia hii mikataba mibovu ambayo mikataba saba imeingia ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, hata *REA*, kwa mfano hiyo kampuni ya *SMEC International* ambayo imelipwa fedha za ushauri, lakini *REA* yenyewe hawakufanya kazi kufuatana na ushauri huo ambao umetolewa na ikaleta hasara karibu ya bilioni moja na ushee. Sasa nasema kwamba, Taasisi kama hizi zikae zikubaliane na Kurugenzi ya Upelelezi na Kurugenzi ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili itumie vizuri *forensic lab* ambayo iko pale, maabara ya uchunguzi ambayo yupo kwenye Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ambayo inachunguza vizuri sana kisayansi. Sasa wakitumia *lab* ile inaweza ikaleta matokeo chanya na mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala ya *TANESCO*, nashauri kama Kamati ilivyoshauri kwamba, mapambano ya kudai madeni kutoka kwa Taasisi za Serikali pamoja na wateja ni deni kubwa sana karibu bilioni 454, sasa *TANESCO* lazima iongeze juhudi za kudai haya madeni. Nakumbuka Mheshimiwa Rais aliwahi

kusema kwamba kama usipolipa madeni kata na amri imeshatolewa, sasa kwa nini madeni haya yanapatikana. Kwa hiyo ni vizuri wakiongeza juhudi katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni Baraza letu la Rufaa la Kodi ambapo utaona kwamba kuna nafasi karibu 10 hazijajazwa pale. Sasa hapa baraza linashindwa kufanya kazi na kuna kesi nyingi ambazo zipo kwa ajili ya rufaa naamni rufaa hizo zitakapoamuliwa basi hawa wataweza kulipa mafao yao kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono mapendekezo yote ambayo Kamati wameyatao na haya ambayo nimeyaongelea. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. Naomba leo wachangiaji muwe tayari tayari, nikikuita tu basi uweze kunyanyuka hapo hapo na kuanza kuchangia. Mheshimiwa Anatropia Theonest

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niseme nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, nimeshiriki katika Kamati pamoja na Wajumbe wenzangu, tumeweza kutoa ushauri tulioutoa, tumetoa maazimio kadhaa ambayo tunaliomba Bunge liliridhie na Serikali iyafanyie utekelezaji. Tumekutana na changamoto kwa maana ya mabadiliko ni madogo, mwaka hadi mwaka tunashauri, lakini mabadiliko yanakuwa ni madogo. Leo itakuwa ni sehemu ya ushauri uleule, zipo hoja nyingi sana ambazo tumepitia, lakini mapendekezo au zipo chache ambazo tumeweza kuwasilisha kwa *interest* ya muda.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea suala mojawapo au masuala mawili, matatu kutegemea na muda wangu. Kuna suala la *Pride*; Wabunge wenzangu waliotangulia wameongelea ufisadi uliojitokeza katika hiyo Taasisi ya *Pride*, lakini kilichosikitisha ni kuona *Pride* kwa maana ya viongozi waliokuwepo wakijua kwamba *Pride* ni Taasisi ya Umma kwa maana ya kumilikiwa na Serikali *hundred per cent*, lakini tangu

ilivyoanzishwa mwaka 1993, lakini *all of the sudden Pride* inakuja kubadilika kuwa kampuni ya mtu binafsi. Sasa nashindwa kuelewa viongozi waliokuwepo waliona nini kilibadilika, kuna Muswada ulikuja, kuna *tender* ilitangazwa, iliuzwa au nini kilitokea hapa katikati mpaka *Pride* kumilikiwa na mtu binafsi. Hiyo tu haitoshi, lakini kuna fedha nyingi za walipakodi wa Norway ambao walikuwa wanawaletea maskini au wananchi maskini wa Tanzania waweze kukopeshwa, waweze kujinua katika maisha yao kwa nia njema kabisa, lakini fedha ikawa *diverted* kama tulivyoona, mtu akajimilikisha *Pride*.

Mheshimiwa Spika, ni mambo ya kusikitisha sana kwa sababu ufidadi ambao unaonekana ulifanyika, hizi nyingine ni *transactions* za *bank to bank* ambao unataraji kwamba kama tuna taasisi ambazo ziko *sensitive* zilipasa kujjuliza ni kwa nini aina za *transactions* kama hivi zinafanyika. Kwenye tarifa yetu imeonekana kwamba *Pride* walikuwa na hisa Benki ya Mkombozi zaidi ya bilioni moja na baadaye bilioni mbili. *Ernest and Young* walifanya ukaguzi mwaka 2016 wakaonyesha hiyo fedha ipo, lakini CAG alivyoenda kufanya ukaguzi kwa mwaka huu tunaomaliza akakuta hakuna tena kitu chochote kwa maana ya bilioni *two point something* imeyeyuka.

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, lakini pia walikuwa na fedha kwenye *account* zaidi ya milioni 400, *Ernest and Young* 2016 walionyesha, lakini CAG alivyokwenda kukagua katika mwaka huu hapa unaoisha akakuta hakuna kitu. Pia kulikuwa na fedha ambayo walikopa kwa maana ya *Pride* kukopa katika benki za biashara; *CRDB*, *NMB* na benki nyingine ambao ni zaidi ya bilioni 48 wakashindwa kulipa mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zile *collateral* zaidi ya bilioni 48 zikawa zimechukuliwa, ni fedha nyingi sana hizi; CAG ameeleza kwamba siyo hela zote, siyo vitu vyote ameweza kuainisha na akaitaka Wizara ya Fedha ifanye haraka kwenda kufanya tathmini kujua ni fedha kiasi gani, ni mali kiasi gani inaweza kuokolewa kwa maana ya kuingizwa kwenye mahesabu iweze kurudi kwenye mfuko sahihi, kwa

maana ya Taasisi ya Serikali kama ilivyoamuliwa na Mahakama kwamba *so far* Serikali ndiyo inamiliki hiyo taasisi.

Mheshimiwa Spika, vile vile CAG akataja kwamba kuna viwanja Morogoro, akataja viwanja viwili ambavyo vina thamani ya zaidi ya bilioni moja ambavyo hata yeye ameshindwa kupata *value* halisi ya hivyo viwanja. Kwa hiyo hajaweza kuvilingiza kwenye hesabu zake. Unaona kwamba ni fedha nyingi ambazo zimechukuliwa na watu, lakini watu wengine wapo, unaambiwa mmoja wa wanahisa wa *Pride* wapo siyo kwamba amefariki hata huyu mzee aliyefariki, lakini wapo wengine. Zimeainishwa *transaction* ambazo zimefanywa na wafanyakazi waliokuwa wafanyakazi wa *Pride, billions and billions of money*, kuna sehemu imeonyesha wafanyakazi 33 walikopeshwa zaidi ya bilioni moja na hawa wafanyakazi wapo siyo kwamba wamefariki, lakini hawa wafanyakazi hawakuwa wanafuata *proper procedures* za kutoa hiyo mikopo. Pia walikuwa wanalipa hela kwa huduma walizopewa ambazo CAG amejiridhisha kwamba zile huduma hazikuwa za kweli hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona kwamba watu waliofanya hiyo biashara wapo, kwa maana watu waoshiriki kuiba hiyo fedha wapo. Nami naungana na maazimio, ni lazima sasa wale watu waende watafutwe na wakamatwe tuone ni watu gani wanaweza kurudisha hicho kiwango cha Serikali ambacho kimepotea, tukumbuke hizo hazikuwa hela za watu binafsi ni hela ambazo zilitolewa na Serikali ya Norway kwa ajili ya Watanzania na wananchi maskini wa Tanzania. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa *interest* ya muda nitaongelea kidogo suala la *TTCL* kama wenzangu walivyosema. Inatia uchungu sana kwamba *TTCL* ambayo tunaitegemea ikiwa ni shirika letu linamiliki mkongo wa Taifa lingeweza kuwekeza kidogo tu, ingeweza kuondoa changamoto pengine tunayoipata ya kuibiwa hata na mitandao mingine ya kibiashara. Wabunge wenzangu wamewahi kulalamika humu ndani kwamba wanakatwa wakati mwingine huduma ambazo hawajaunganishwa,

wanakatwa bando tofauti na muamala walioomba. Kama *TTCL* inge-*stabilize* kidogo ingeweza ku-*address* hizo changamoto tunazopata.

Mheshimiwa Spika, tulisema na kwenye Kamati imeeleza na wenzangu wamesema *TTCL* kwenye *market share* inamiliki asilimia moja tu nyuma ya makampuni mengine yoyote hata yale yaliyokuja juzi *Halotel* inamiliki *ten percent* wakati *TTCL* ikibaki kwenye asilimia moja, tumefikaje huko. Imeonyesha kwamba bajeti ambayo walipanga kwa maana ya bajeti ya mpango kazi wao wa mwaka jana, ambao ulikuwa ni zaidi ya bilioni 671 waliweza kupata bilioni 29 tu, ambayo ni sawasawa na upungufu wa asilimia 96. Kwa hiyo unaweza ukajiuliza ni kwa kiwango gani wanaweza kutekeleza mataminio yao. Kwa maana hiyo hata fedha yenyewe hawana, kwa hiyo, hawawezi kufanya biashara, hawawezi kuwekeza na hawawezi ku-*compete*.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinachekesha *TTCL* wamejiunga na Tigo. Kwa Mikoa ile ambayo hawana wao mawasiliano kwa ajili ya kufanya *roaming*, wao wananunua bando GB moja kwa shilingi 2500 na wanawauzia wateja GB hiyo hiyo kwa shilingi 1500. Hivi hiyo ni biashara gani hata ingekuwa sijui hesabu siwezi kufanya hiyo biashara kichaa haiwezekani. Lakini wameonyesha baada ya CAG ku-*doubt* na kuwauliza wameonyesha kwamba wanafanya *re-adjustment* na *negotiation* upya na badala yake bando moja watauziwa kwa shilingi 1800.

Mheshimiwa Spika, bado tunarudi kule kule, huwezi kununua bando kwa 2500 halafu ukauza kwa 1800 hiyo ni biashara kichaa. Ni lazima tuangalie ni namna gani *TTCL* inaweza kusaidika na kujikwamua ili iweze kuteka soko iweze kukidhi haja ya uanzishaji wake.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ambacho kilikuwa *strange* tuliambiwa kwamba *TTCL* wanadaiwa, *TTCL* ambao ni watoa huduma wanadaiwa na watu wa huduma zaidi ya bilioni 11. Sitaiongelea zaidi kwasababu wenzangu

wameshaiongelea. Tunaona kwamba ni changamoto kubwa sana, sio hiyo tu lakini pia wamekuwa na bando mbalimbali ambazo wanazitoa kama *bonus* kwenye soko. Kuna bando la Chuo ambalo wanaliita *boom*, kuna bando ambalo walitoa kwa ajili ya wafanyakazi wao. Sasa cha kushangaza hizo bando badala ya kutumika na Wanachuo *per-se* wanaunganishwa na watu wengine tofauti.

Mheshimiwa Spika, na kitu kingine ambacho CAG alishangaa, hata ungechukua wafanyakazi wa TTCL nchi nzima, wameunganishwa kwenye bando lao la *promotion* haiwezi kulinganika na idadi ya watu ambao walikuwa wanatumia hilo bando kama wafanyakazi wa TTCL. Kwa hiyo, unaona kuna udanganyifu mkubwa sana hata ndani yao wenyewe. Sasa sielewi hapo, ni kwa namna gani ni lazima tuangalie kama shida ipo kwenye *management* ni kwa nini *management* haiwezi k –*perfor*.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine lazima tuangalie changamoto inaweza kuwa si tu ya fedha, lakini pia ya ubunifu. Kama unafanya ubunifu wa kununua bando kwa 2500 na kuuza 1500 *then* changamoto hapo sio hela, changamoto ni namna ya uongozi, changamoto ni namna ya kufikiria.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia hoja yangu ya mwisho inahusu suala la Maliasili, CAG pia alitupitisha kwa matumizi ya bilioni 1.5 iliyotumiwa na Maliasili bila kuwa imepangiliwa au haiko kwenye bajeti. Mpaka CAG anafanya ukaguzi, anafanya *special audit* kutaka ku-*verify* je, Serikali ilifaidika nini na matumizi yale ya *festival* ambazo zimefanyika. Zimefanyika Dar es Salaam, imefanyika Dodoma, imefanyika na Arusha na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, CAG hajapata jibu, ndio maana anarudia kufanya *evaluation* kwa maana ya kufanya *special audit* kuona ni kwa kiwango gani Serikali imefaidika na hiyo tamasha iliyofanyika. Lakini changamoto anazozii-*address* pia hizo fedha ambazo zinakuwa zinakusanywa nje na bajeti zina changamoto ya kuwekwa kwenye mfumo wa fedha wa

Serikali. Kwa hiyo, inatoa nafasi ya watu kutumia hiyo fedha ya umma, kwa udanganyifu. Inatoa *loophole* ya watu kupiga hela. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimepitia kidogo hapa inaonyesha malipo ya wasanii, kwa kazi iliyofanywa na wale wasanii, kuimba na kufanya nini ilikuwa ni zaidi ya milioni 52. Posho za kujikimu zaidi ya milioni 133, kwa hiyo, watu wamelipana posho hizo 133 kwa kujikimu kwa ajili ya kukidhi ile tamasha. Lakini swali langu kama hiyo ilionekana ni kipaumbele kwa nini haikuletwa hapa Bungeni ili iweze kupitishwa kwenye bajeti ya kawaida? Badala yake mnaenda kukusanya kwenye Taasisi zilizo chini ya Maliasili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nadhani tunajua sheria za bajeti, na Wizara zijikite kwenye hizo sheria, na sisi kama Kamati tumemuagiza CAG aende akafanye *evaluation*, aende akafanye ukaguzi maalum, kuona kama Serikali imefaidika na je fedha hiyo imetumika kama ilivyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ninaweza kuongea kwa sababu nina muda kidogo, ni suala la NIDA waliochangia hapa wote wameeleza. NIDA mwaka hadi mwaka tunaongelea changamoto kwenye NIDA, na nataka nijulize je shida ya NIDA ni nini? Shida ni *management*? Je, kuna *subotage* kwa nini ni mwaka hadi mwaka? Kumekuwa na changamoto ambayo imesababisha hasara ya zaidi ya bilioni 42. Ambayo alieleza vizuri Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati. Kwamba waliagiza mtambo, huo mtambo ulivyokuja ukakuta hauwezi kufanya kazi ya kuzalisha vitambulisho. Ambavyo sawa sawa na vile vilivyokuwa vinazalishwa kwa hiyo unajikuta kwamba mmeleta mtambo ambao uko *redundant*. Mmeingiza fedha za Wapiga kura bila kufanya utafiti, hiyo ni haiwezekani kama ni *management* ambayo iko *very serious* kwanza walipaswa kwenda hata na *sample* husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa unaweza ukaona kumekuwa na changamoto kubwa sana. Mwaka hadi

mwaka tunayoongelea kule *NIDA*, ni lazima tuangalie na sisi kama Kamati tumeshauri, hayo maoni yetu kama Kamati tunaomba Serikali iangalie namna sahihi ya kusaidia hili shirika kwa maana ya kuisaidia *NIDA* isiweze kuendelea kutumia ovyo fedha za watu kwa maana ya walipa kodi. Lakini tukiwa sasa tuweze kupata vitambulisho kwa wakati. Hayo malighafi ya vitambulisho yapo yamejazana pale kwenye *godown* la *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, ukienda leo ninavyoongea utakuta vimetupwa kila sehemu. Hivyo vitambulisho vibovu vinaunganishwa na *material* kwa maana ya malighafi. Na baada ya muda hawawezi ku-*sort* kwa hiyo mzigo utatupwa. Unaona kwamba ni matumizi mabaya ya rasilimali. Lakini ambacho nilikuwa najiuliza wakati nasoma hivi vitu, mtoto wangu mmoja aliniuliza, akasema hivi mama haya mambo yote yamefanyika katika Serikali ya Awamu ya Tano? Mbona tuliambiwa inachapa kazi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hayo naomba muyajue kwamba ni mambo ambayo yanaendelea. Mnaweza kuwa mnapiga kelele huku, kumbe huko nyuma ndio fedha za walipa kodi zinazidi kuteketea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto tumeziona ni nyingi siwezi kuingea hapa, naungana na Kamati kwamba hoja zetu kwa maana ya mapendekezo yetu yapitishwe ili Serikali iweze kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwakilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest, ambaye umepitia na kufafanua zaidi hoja za Kamati, baadhi yake zitapata majibu huenda. Kama hii ya *TTCL* Bodi kukataa kusaini taarifa ya *CAG* labda wana sababu za msingi. Watu wa Wizara wanaweza kutudokeza kidogo, kwa nini Bodi hii inakuwa ina *behave* namna hii. Nimeona ipo kwenye taarifa ya Kamati moja kwa moja.



Mheshimiwa Frank Mwakajoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Hassan Elias Masala atafuata.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kunipa fursa kuchangia taarifa ya *CAG*. Nina mambo kama manne ambayo nitazungumza siku ya leo, na jambo la kwanza kabisa niwapongeze sana na kuwashukuru sana Wananchi wangu wa Mji wa Tunduma kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuniunga mkono, nikiwa natekeleza majukumu ya kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naanza kwanza na *MSD*, Bohari ya Dawa ya Taifa, nakumbuka juzi hapa wakati Waziri wa Fedha anawasilisha taarifa yake ya Wizara ya Fedha lakini pia wakati tunasoma Taarifa ya Wizara ya Afya kulikuwa na deni ambalo *MSD* walikuwa wametoa huduma kwenye Taasisi mbalimbali za Serikali, deni karibu bilioni 147. Hizi fedha zilikuwa zimekopwa na bado hazijalipwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Taarifa ya *CAG* ambayo tunaipitia sasa hivi, kuna deni ambalo ni la muda mfupi karibuni bilioni 27.7 ambalo pia halijalipwa. Na *CAG* ametahadharisha sana kuhusiana na mikopo hii ambayo Serikali imekuwa inatumia huduma za dawa lakini hailipi. Inasema kwamba huduma kama zinatolewa halafu bado inaonekana Serikali haitaki kutoa fedha inawezekana shirika hili linaweza likafa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hali sio nzuri sana kwenye Shirika hili la *MSD*. Na kinachoonekana ukijaribu kuangalia Taarifa ya *MSD* mpaka sasa hivi walikuwa wanahitaji kupata dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 101 ili kuhakikisha kwamba wanatoa huduma bora katika nchi yetu. Lakini wamekosa hizi fedha kwasababu tayari Serikali bado inadaiwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, tunataka Waziri wa Fedha atuambie na haya madeni ukienda kusoma ni madeni

ambayo yameshahakikiwa tayari. Waziri wa Fedha atuambie ni kwa nini mpaka sasa Serikali haitaki kulipa fedha hizi ili mashirika haya ambayo yanaanzishwa na Serikali yaweze kufanya vizuri na kama ambavyo tulikuwa tumeyaanzisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna shida kubwa sana kwa Serikali kutokulipa madeni katika mashirika mbalimbali. Lakini nilikuwa najaribu kupitia mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Nimeangalia kwenye Taarifa ya CAG ya mwaka 2018, Serikali ilikuwa inadaiwa karibuni trilioni mbili na bilioni 975 lakini kati ya fedha hizo tulitegemea kwamba katika mwaka unaofuata, tungeona mabadiliko na tungeona Serikali imeshalipa. Lakini cha kushangaza kwa mwaka huu Taarifa ambazo CAG ametuletea, Serikali imeongezeka deni na inadaiwa sasa hivi shilingi trilioni 2 na bilioni 417.79 kwa hiyo ni fedha ambayo tayari imeshaongezeka.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaunganisha mifuko hii nia na madhumuni tulisema kwamba tunapunguza kwanza matumizi ya fedha kwa ajili ya uendeshaji. Lakini pia tukasema kwamba tunataka kuongeza ufanisi katika Mifuko hii. Lakini kinachoonekana sasa hivi hali imekuwa mbaya zaidi hakuna kinachoendelea kabisa. Serikali inazidi kukopa fedha na CAG ameshauri hapa amesema kama Serikali itashindwa kulipa fedha hizi tasfiri yake ni kwamba hii mifuko inaweza ikashindwa kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, na huduma ambayo inaweza ikashindwa ni pamoja na kushindwa kulipa fedha hizi kwa wastaafu ambao wamewekeza fedha zao. Sasa hii ni hatari sana kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wamelitumika Taifa kwa muda mrefu, anastaafu akiwa anajua kabisa kwamba tayari atalipwa fedha hizo lakini cha kushangaza Serikali imekopa hizo fedha, sasa Waziri wa Fedha anatakiwa kutuambia leo kwamba ni lini fedha hizi zitalipwa ili mifuko hii iweze kufanya vizuri kama ambavyo tulikusudia.

Mheshimiwa Spika, lakini tunajua kabisa mifuko hii ilikuwa inafanya uwekezaji, leo ukijaribu kuangalia fedha za uwekezaji kwa mwaka huu ndani ya miezi 11 baada ya kuunganisha mifuko hii imeonekana kuna hasara, kuna upungufu wa fedha ambazo zimekusanywa kwa asilimia 55. Mwaka 2018/2019 walikuwa wamekusanya bilioni karibu 975 lakini mwaka huu wamekusanya karibuni bilioni mia nne na kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukijaribu kuangalia taarifa hizi unaona kabisa ni jinsi gani ambavyo Serikali imeamua kuasili moja kwa moja Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, na hii inapelekea wasiwasi mkubwa sana kwa CAG kwamba kuna uwezekano mkubwa huko mbele tunapoelekea wakashindwa kuendesha mifuko hii lakini pia wakashindwa kuwalipa wastaafu wetu ambao tayari wamewezeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri Serikali wakati wanakuja ku-*wind up* watuambie ni namna gani wanaweza wakalipa fedha hizi haraka iwezekana ili hii mifuko sasa iweze kuendelea kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza hapa ni kuhusiana na *UDA* pamoja na *UDART*. Ninakumbuka kabisa kwamba mwaka 2013 Shirika la *UDA* liliingia mkataba na *Simon Group Limited*, lakini baada ya kuingia mkataba ule kulikuwa na hisa ambazo zilikuwepo karibu hisa milioni tatu laki sita na kidogo na katika makubaliano ambayo yalikuwepo ni kwamba walikubaliana kwamba hisa zile wanaiuzia Kampuni ya *Simon Group* kwa shilingi 1,675. Lakini kilichotokea hisa zile baada ya kufanya mahesabu zilikuwa na thamani ya bilioni tano karibuni *point* saba.

Mheshimiwa Spika, lakini kilichotokea *Simon Group* hakuweza kulipa zile hisa kama ambavyo ilikuwa imekubalika na badala yake alipewa mamlaka ya kukopa fedha benki kwa kutumia hisa za *UDA* ambayo ni mali ya Serikali. Baada ya kukopa zile fedha walikwenda kukopa fedha kwenye benki ya *NMB* mikopo ambayo walikopa mikopo miwili. Lakini

walishindwa kurejesha ile mkopo na mpaka sasa hivi mikopo ile imeanza kulipwa kwa kipindi hiki. Kitendo hicho tunashangaa sana kwamba mpaka sasa hivi Serikali ina hisa asilimia 85 halafu kampuni ya *Simon Group* ina asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, sasa tunashangaa wamedanganya katika kununua hisa lakini bado pia hisa zao zinazidi kupanda siku hadi siku na Serikali imeshindwa kuchukua hatua wakati kunaonyesha kulikuwa udanganyifu mkubwa katika kuhakikisha kwamba wananunua shirika hili. Kwa hiyo, sisi tunataka kujua kwamba Serikali inachukua hatua gani mpaka sasa kuhakikisha kwamba kama alivyoshauri *CAG* kwamba kwanza hisa ambazo sipo kwa *Simon Group* ziweze kunyang'anywa na kuwekwa ziwe hisa za Serikali na iwe asilimia 100 kuwa na hisa za Serikali. Serikali ina kigugumizi gani kuchukua hatua kwasababu huu ushauri sio si *CAG* huyu tu amefanya ushauri huu ni *CAG* wote waliokuja kufanya ukaguzi kwenye yale mashirika wamejaribu kutoa ushauri lakini Serikali inagoma.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka mwaka uliopita kulikuwa na mgogoro wa Meya wetu wa jiji la Dar es Salaam ilitokea kwasababu ya mgogoro wa mkataba huu lakini Meya wetu ameondolewa lakini tunashangaa watu ambao wamefisadi fedha za umma wamekaa wanaendelea kuvinjari na hakuna kitu chochote kinachochukuliwa. Tunataka Waziri wa Fedha wakati anakuja kuzungumza atuambie ni namna gani mkataba huu utakwenda kuvunjwa kuhakikisha kwamba na wale watu ambao wametumia udanganyifu wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini haya yote yalikuwa yanafanyika wakati mji wa Dar es Salaam unaongozwa na Serikali ya CCM. Lakini sasa hivi tuliokuja kupata adhabu ya kazi hii mbovu iliyofanyika imekuja kupata Uongozi wa CHADEMA. Tunaomba wakati Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali wanatengemea kwenda kulifanyia jambo hili wahakikishie kwamba wanafanyia kazi pia maamuzi yaliyofanyika ya kihuni ya kumuondoa Meya wetu wa Dar es Salaam. Ili Meya aweze kurudi kwa sababu hatuoni sababu

za msingi za kumuondoa Meya wetu wakati tayari waliofanya uhalifu mwaka 2013 na mwaka 2012 ni Meya wa Chama ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba sana jambo hili liweze kueleweka hivyo...

**SPIKA:** Kwani Frank Meya kaondolewa hapa? Si ameondolewa na Madiwani huko sasa ukituambia sisi si inatupa tabu tu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wameondolewa na Madiwani lakini Madiwani hao ambao wamekwenda kumuondoa Meya wetu sababu ambazo zilikuwa zinatajwa ni hizi hizi ambazo hakuwepo kabisa na waliokuwepo wamekaa tu mpaka sasa hivi wanaendelea kuvinjali kama ninavyosema.

Kwa hiyo, wamemuondoa kwa kitu ambacho hakikustahili kabisa wamemuonea kabisa, sasa namna hii hatuwezi kujenga mtu anayekataa fedha zisitumike ambazo ni fedha haramu watu wanasema zitumike halafu anapata adhabu mtu ambaye anajaribu kuisaidia Serikali hiki ndicho ambacho tunakizungumza.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kampuni hii pia ya *Simon Group* pamoja na mkataba wa *DART* kulikuwa na magari ambayo yalikuwa yamekubalika kwamba yanunuliwe magari 140. Lakini mpaka juzi *CAG* anakwenda kufanya ukaguzi yalikuwa yamenunuliwa magari 138 kwa hiyo, magari mawili yalikuwa hayapo. Lakini pamoja na hayo magari mawili ambayo yalikuwa hayapo wakati wananunua kati ya hayo magari 85 kwenye kampuni ambayo walinunua haya magari walikubaliana kwamba mwenye kampuni aliyowauzia magari atafanya matengenezo ya magari hayo, ndani ya miezi 36 bure na atatoa *spare* bure na wakasema kwamba hizo spea watazipeleka kwenye hayo makampuni.

Mheshimiwa Spika, lakini spea hizo zilikuwa na thamani ya dola laki mbili na elfu sitini na saba, lakini mpaka *CAG*

anakwenda kufanya ukaguzi tayari walikuwa wamekabidhi spea za dola elfu tisini na tisa tu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado kuna *spare* za dola laki moja na elfu sitini saba bado zinadaiwa. Kwa hiyo, kuna ufisadi wa kutosha...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** ...katika mikataba ambayo inaingia na Serikali hii. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, Mheshimiwa Aisharose, kabla ya Mheshimiwa Aisharose Waheshimiwa Wabunge kila anayesimama anasifu kazi nzuri sana ambayo imefanywa na CAG na bahati nzuri katika *Galery* ya Spika tunaye ndugu Kichele ambaye ndiye CAG wetu naomba mtambue uwepo wake. (*Makofi*)

Karibu sana CAG tunakushuru sana kwa taarifa nzuri ambayo imewezesha kamati yetu ya PAC kufanya kazi yake vizuri na kwa kweli kazi yako na taarifa yako ndiyo msingi wa Mjadala wa Bunge hili wa siku mbili. Kwa hiyo, tunakushuru sana tunakupongeza endelea kuchapa kazi. (*Makofi*)

Ahsante sana, Mheshimiwa Aisharose Matembe atafuatiwa na Hassan Elias Masala.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nimshukuru sana Mwenyenzi Mungu kwa kuendelea kutujalia uzima na kuendelea kuchapa kazi kwa maslahi mapana ya watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wajumbe wenzangu kwa kuchambua taarifa hii kwa kina na kwa dhamira ya kuyaokoa mashirika yetu ya Umma. Nakupongeze wewe kwa kazi nzuri unayoendelea kuifanya

kwa ushauri na miongozo na ni imani yangu kwamba Wana-Kongwa watakuchagua kwa kushindo kwa kazi nzuri hii unayoifanya. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya kufufua mashirika yetu ya Umma. Ni ukweli usiopingika kwamba mashirika haya yalikuwa yanachungulia kaburi, lakini sasa mashirika haya yanafanya kazi na yameimarika. Nawaomba sana Watendaji wote waendeleo kufanya kazi kwa juhudi na tija ili sasa yaweze kuwa na maslahi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye mashirika yafuatayo: *TANESCO*, *REA* na *NSSF*. Toka kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, *TANESCO* imekuwa ikifanya kazi nzuri na kutoa huduma bora kwa Watanzania, lakini imekuwa ikikwamishwa na deni kubwa la shilingi bilioni 454 ambalo inadai Taasisi za Serikali na watu binafsi. Baadhi ya Taasisi hizo ambazo *TANESCO* inadai ni Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili, *JWTZ*, Jeshi la Polisi, Magereza pamoja na *DAWASA*. Hayo ni baadhi ya mashirika ambayo *TANESCO* inadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 205 ambazo ni nusu ya deni hilo zinadaiwa Taasisi za Serikali ambazo Bunge hili limekuwa likikaa na kupitisha Bajeti zikiwepo za uendeshaji wa mashirika hayo, iweje leo washindwe kulipa gharama hizo? *TANESCO* ni kama mashirika mengine, inahitaji fedha hizo ili iweze kujiendesha katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, taarifa za hesabu za *TANESCO* za kila mwaka zimekuwa haziko vizuri kutokana na deni hilo. Hivyo basi, ninaishauri Serikali iweke mkakati maalum wa kuhakikisha mashirika yanayodaiwa yanalipa deni hilo mara moja na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mheshimiwa wetu Rais ni kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa ni nchi ya viwanda;

kwa kukwamisha *TANESCO* ni kukwamisha shirika letu; kwa kuikwamisha *TANESCO* ni kukwamisha nitihada za Mheshimiwa Rais. Pia naishauri Serikali kuendelea kuwekeza katika teknolojia ili kuuza umeme wake kwa njia ya Luku kwa mashirika yote. Hii ikiwa kama ni mkakati wa kudhibiti madeni.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia ni Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*). Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala wa Umeme Vijijini kusambaza umeme lakini kumekuwa na changamoto katika hesabu zake. *REA* walitoa kazi kwa kampuni ya *SIMEC International* kwa ajili ya ushauri wa kitaalam ambao iliwataka *SIMEC International* kuandaa nyaraka za zabuni kwa wakandarasi 29 na iliwapa kiasi cha shilingi bilioni 1.083 kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa mkondo wa umeme katika vijiji 7,893.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza kampuni ya *SIMEC* haikufanya kazi hiyo na badala yake *TANESCO* na *REA* waliweza kuwapa kazi wakandarasi 29 kufanya kazi hiyo. Hapa kuna maswali mengi ya kujuliza. Kulikuwa na sababu gani ya kutoa kazi hiyo kwa mshauri huyo na huyo mshauri asiweze kuifanya kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, kingine cha kushangaza, fedha hizo zililipwa zote kiasi cha shilingi bilioni 1.083 na hivyo kukiuka Sheria za Manunuzi ya Umma ambapo sheria hiyo inamtaka mtoa huduma kulipwa kiasi cha fedha na baada ya kumaliza kazi yote, basi aweze kulipwa fedha zote, lakini yeye alilipwa fedha zote.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa sasa tumejifunga mikanda na tumekuwa tukitekeleza miradi yetu wenyewe kwa fedha zetu za ndani, sasa kupotea kwa hizo shilingi bilioni moja ni sawasawa na kuitia hasara Serikali. Naishauri Serikali ifanye uchunguzi wa kina kubaini ni nani aliyefanya mchezo huo na watakaobainika kufanya mchezo huo hatua kali za kisheria zichukuliwe na kiasi hicho cha fedha kirudishwe. Vipo vijiji vyangu vya Mkoa wa Singida ambavyo havina umeme. Nina imani kwamba pesa hii ikirudishwa itaweza kupelekwa



kule katika vijiji vyangu vya Mkoa wa Singida na kupatiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya CAG, Kamati ilibaini kusuasua kwa uzalishaji wa Kampuni ya *Mkulazi Holding* iliyokuwa inamilikiwa na Shirika la *NSSF*. Msingi wa kuanzishwa kwa kampuni hii ilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa sukari na kuondokana na kero ya ukosefu wa sukari nchini. Pamoja na hasara hiyo ambayo Kamati ilibaini katika uwekezaji huo, naishauri Serikali, huu ni wakati muafaka sasa wa kuhakikisha kiwanda hicho kinafanya kazi, mitambo iwepo ili kuepuka hasara ambayo imeweza kujitokeza.

Mheshimwa Spika, natambua *NSSF* ina uongozi madhubuti chini ya Mtendaji Mkuu, Bwana Erio William na Mheshimiwa Rais hajakosea kumweka Mtendaji huyu. Niseme tu, ukiangalia makusanyo kwa mwezi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 55 hadi kufikia shilingi bilioni 98. Nampongeza sana Mtendaji Mkuu pamoja na timu yake kwa kuhakikisha mifumo ya *TEHAMA* inakaa vizuri ambapo hapo awali mifumo hiyo ilikuwa haijaka sawa. Hii ni hatua kubwa sana ni imani yangu kwamba tukiwapa muda wataweza kufanya kazi nzuri ya kuliboresha Shirika letu hili la *NSSF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aysharose Matembe. Nilishakutaja Mheshimiwa Hassan Elias Masala na atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kupata nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii au risala hii ya CAG. Naomba niungane na wenzangu kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo umekuwa unaifanya lakini pia nitumie nafasi hii kukushukuru kwa namna ambavyo binafsi nimepata fursa ya kujifunza toka nimekuwa Mbunge kwa sababu ni awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza umeniweka kwenye Kamati ya Sheria ndogo. Sikuwa Mwanasheria lakini nimepata nafasi ya kujifunza mambo mengi sana juu ya mchakato wa kutunga sheria na namna ya kuzichaka, lakini pia kama haijatosha umenipa nafasi ya kujifunza mambo ya kiuhasibu kwa kuwa kwenye Kamati hii ya PAC.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Viongozi wetu wa Kamati wakiongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Naghenjwa na Makamu wetu wa Kamati Mheshimiwa Aeshi kwa Uongozi na namna ambavyo wametumia ili kutimiza majukumu ambayo ulitukabidhi.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania. Mambo mengi ambayo yanafanyika ndani ya miaka hii mitano hakika sisi ambao tunatoka huko kwenye Majimbo ya pembezoni tutakuwa watovu wa fadhila kama hatutaweza kusema neno la shukurani kwake na tunaendelea kumwomba ili aweze kutimiza na kutufikisha kule ambako tunaamini ndiko ambako tulikuwa tunahitaji kwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo naomba sasa nijielekeze kwenye hoja kwa baadhi ya maeneo ambayo sisi kama Kamati tumetumia muda mwingi sana kuyachambua. Kwa msingi huo, kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati naomba niungane na Wajumbe wenzangu kuunga mkono na kuendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wengine wakubaliane na mapendekezo ambayo tumeyatoa katika hoja zote 15 ambazo sisi imetuchukua muda takribani wiki tatu tunazipitia na kutoa mapendekezo katika Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nimeona nitumie nafasi hii kutoa tu mapendekezo ya ziada kwenye baadhi ya hoja nne ambazo waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa sehemu nyingine na wao wamejaribu kuzichangia. Eneo la kwanza ni kwenye eneo la madeni ya TANESCO. Kwa sisi ambao tunatoka kwenye Majimbo ya pembezoni kumekuwa na

changamoto kubwa sana ya wananchi wetu; moja, kuona namna ambavyo wanaweza kuunganishiwa umeme wa uhakika, lakini kumbe sasa tunakuja kupata sababu ambazo wakati mwingine *TANESCO* wanashindwa kutoa huduma kwa sababu tu ya madeni ambayo baadhi ya Makampuni, Mashirika na pia baadhi ya wadau kumbe wanashindwa kulipa. Kwa hili tunampongeza sana *CAG* kwa kuonyesha bayana ni kitu gani ambacho wakati mwingine kinakwaza *TANESCO* kushindwa kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kiasi cha deni shilingi bilioni 454 ambazo mchanganuo wake Serikali ni zaidi ya shilingi bilioni 205; ukienda kwa binafsi ni zaidi ya shilingi bilioni 199. Yako maelekezo Mheshimiwa Rais alishayatoa, lakini utakubaliana nasi kwamba pia tulishawahi kutoa mapendekezo ya kuona hatua zichukuliwe sasa kwa wale wote ambao ni wadaiwa sugu kama ilivyo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tuliwahi kupendekeza kwenye baadhi ya maeneo hasa kwa wakati ule nakumbuka tukijadili suala la mikopo ya wanafunzi, moja ya maeneo ambayo Serikali imefanya kazi kubwa sana ni kuhakikisha inakusanya madeni kupitia Bodi ya Mikopo. Hili limewezekana, walio wengi wamelipa madeni yao.

Mheshimiwa Spika, sasa tulifikiri *strategy* zilizotumika na Bodi ya Mikopo zingeweza pia kutumiwa na watu wa *TANESCO* kuona namna ya kukusanya deni hili ili wananchi wetu waweze kupata huduma sasa kwa karibu zaidi badala ya kuendelea kulimbikiza deni lakini pia kuendelea kuchafua hesabu ambazo mpaka leo haziwezi kufutika kutokana na changamoto ya deni hili.

Mheshimiwa Spika, sasa mependekezo ambayo nilifikiri baadhi wameshayasema ilikuwa; moja ni kwamba tufikirie namna ya kukata au kusitisha huduma. Ukiziangalia Taasisi zote zinazotajwa hapa, ni zile ambazo zinatoa huduma muhimu sana kwa wananchi wetu. Sehemu kama hospitali, sehemu kama vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama,

unapoanza kufikiria namna gani; na kuna wakati tulishawaita baadhi ya wahusika wa hayo maeneo. Ni kama tayari kunaingia sasa uwoga wa kwamba unawezaje kwenda kukata umeme Jeshini? Kwa sababu wanafanya kazi kubwa ya kutoa ulinzi kwa nchi yetu, lakini Serikali ina namna yake ya kuzungumza na ina namna yake ya ku-*reconcile* ili baadhi ya mambo yaende.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa ushauri kwa Serikali na kwa wahusika waone namna wanavyoweza kutengeneza utaratibu mzuri, lakini moja, tuanze na hatua hiyo basi ya kusitisha huduma ili wale ambao wanadaiwa walipe hili deni na wananchi wetu waweze kupata huduma katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, *strategy* ya pili ambayo pia ingeweza kutumika kwa watu binafsi tunatumia Luku; hujalipia Luku, huwezi kupata huduma. Sasa sijajua ni kwa nini Serikali au *TANESCO* isingeweka utaratibu wa kuona namna sasa hawa wadaiwa wote nao pia waingie katika mfumo huu wa kutopata malipo au kutopata huduma kabla ya kufanya malipo. Nafikiri kwa kufanya hivi *automatically* tutakuwa tumeondoa huu utata wa nani alipe, nani asilipe na vitu vya namna hiyo. Haya ukisoma kwenye *report* yetu hatukuyaingiza lakini niliona tuongezee ili tuweze sasa kuona namna ya kukusanya deni hili kwa lazima.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo niliona pia nitoe mchango wangu pamoja na kwamba tumeshazungumza kwenye Kamati, ni kwenye eneo la umeme vijijini. Nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sehemu kubwa na kazi kubwa ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Spika, Nachingwea nina vijiji 137, ndani ya kipindi hiki cha Awamu ya Tano zaidi ya vijiji 40 vinapatiwa umeme vijijini, lakini kumbe Serikali ingekuwa na namna nzuri ya kusimamia matumizi ya fedha katika eneo hili kadri alivyobainisha *CAG*, unaweza ukaona kumbe tulikuwa na uwezo wa kusambaza umeme hata kwa vijiji zaidi ya 70 kwa awamu hii moja peke yake. Hii ni kwa sababu utaona kuna

matumizi ambayo hayakuwa ya lazima na Mjumbe mwenzangu aliyepita amezungumza lakini pia kwenye Kamati tumezungumza.

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa ya CAG utaona kulikuwa na matumizi ambayo hayakuwa na ulazima. Ametafutwa *consultant* wa kufanya kazi ambayo kimsingi ni kama haikuhitajika. Sasa hili jambo itakuwa ni hujuma ambayo tu imefanyika ya makusudi ambapo nilikuwa nashauri Serikali ione namna ambavyo inaweza kuchukua hatua katika eneo hili. Fedha hii ambayo imetumika nje ya utaratibu ambayo ni zaidi ya *1.8 billion* ikiridishwa kupitia hii kampuni ambayo ilipewa kufanya kazi ya *consultancy*, basi kumbe inaweza ikasaidia kusambaza umeme wa ziada katika baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, hili niliona sisi kama Kamati lakini na wewe kupitia Bunge lako, basi lione namna ambavyo linaweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo niliona nitoe ushauri wa ziada ni eneo hili la *NIDA*. Yamejadiliwa mambo mengi katika eneo hili, lakini tumevutana sana tukiwa kwenye Kamati yetu juu ya kuliendea jambo hili linalohusiana na *NIDA*. Wako wenzangu wamezungumzia kwenye *aspect* ya mitambo. Hili jambo tumelifanyia kazi kama Kamati, lakini ukija kwenye baadhi ya maeneo utaona kuna namna fulani ya uzembe ambayo Bunge lako lingelidhia mapendekezo yetu ya kuchukua hatua kwa uongozi wa *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, utaona hapa kuna suala la utunzaji wa malighafi za kuzalishia vitambulisho. Leo nipo hapa Bungeni napokea kutoka simu Nachingwea, kutoka kule vijijini wananchi hawana vitambulisho, simu zao zimefungwa, wanapanga foleni kwa ajili ya kuja kufuata huduma pale Mjini.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwa watu wa *NIDA* hawana mashine za kufanyia kazi, hawana *manpower* ya kufanyia kazi ambayo inatosheleza maeneo husika, lakini

kumbe kuna watu huku wamepewa dhamana wanashindwa kutimiza wajibu wao. Ukiangalia ni uzembe wa makusudi, kwa sababu kama unashindwa kutunza malighafi, umezijaza stoo zinaharibika wakati kuna wananchi kule vijijini wanatapa shida. Jambo hili halivumiki lakini pia halieleweki malengo yake hasa ni nini? Kwa hiyo, tutaomba mwongozo wako na Waheshimiwa Wabunge...

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa Msekwa.

**SPIKA:** Ndiyo, Taarifa Msekwa.

### T A A R I F A

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Hassan Masala kwamba siyo tu *NIDA* wameshindwa kutoa vitambulisho, yapo baadhi ya maeneo kwa mfano Mtwara Mijini hivi sasa wana zaidi ya mwezi wamefunga kabisa kufanya hiyo huduma pamoja na kwamba sisi Bunge tunaendelea na Bunge hapa, Taasisi kubwa ya Serikali, lakini wao pamoja na umuhimu wao na ulazima wa kuwapa vitambulisho Watanzania wamefunga kutoa hiyo huduma kwa kigezo kwamba sasa hivi kuna *Corona* Tanzania. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Hassan Masala aipokee taarifa kwamba ni kweli kabisa hawa watu ni wababaishaji hapa nchini Tanzania.

**SPIKA:** Unaipokea Taarifa Mheshimiwa Masala!

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba nipokee taarifa ya Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwa sababu anachokizungumza ndicho kitu ambacho kinaendelea kwenye maeneo ambayo na sisi tunatokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili tulipe uzito, kwanza hatua zichukuliwe kwa Menejimenti ya watu wa *NIDA*, wametuingiza hasara kubwa sana.

Wametuingiza hasara kwenye mashine, wametuingiza hasara kwenye kuleta teknolojia ambayo sidhani kama waliifanyia uchunguzi kabla hawajaingiza ndani ya nchi yetu. La tatu, wanashindwa kusimamia dhamana waliyoakabidhiwa kwa kushindwa kutunza vifaa ambavyo kimsingi vingeweza kutusaidia. Kwa hiyo, hili eneo niliona niliweke katika mtindo huu.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo niliona nalo pia nichangie ambalo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia ni kwenye eneo la matumizi ya fedha ambayo yako nje ya Bajeti kupitia watu wa Maliasili. Tulimwita *Accounting Officer*, tulizungumza naye kwa kirefu sana. Bahati nzuri au bahati mbaya wakati jambo hili linafanyika ni kama *Accounting Officer* hakuwepo Ofisini, yule mtu *proper* ambaye alikuwa ni Katibu Mkuu, lakini waliokuwepo ni kama walikuwa wanajaribu kukimbizana na jambo hili kwa hujuma ya makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, tulijaribu kuomba tuone faida zinazoshikika au zinazopimika juu ya matumizi ya fedha hii ya *1.5 billion* lakini kimsingi hakuna maelezo yoyote ya ziada. Sasa *justification* ya matumizi ya fedha ya Serikali ambayo yamekuwa na taratibu zake za Kiserikali, Kikanuni na Kisheria ni kama hapa hazikuzingatiwa kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, ili kutoweka kumbukumbu mbaya ya kuweza kuacha watu wengine kutumia mamlaka zao vibaya na kuidhinisha kutumia fedha ambazo ni za nje ya utaratibu tulifikiri kupitia hiki ambacho *CAG* amekibainisha basi tumsaidie na tumtie nguvu kama ambavyo umemsimamisha hapa. Nilifikiri tukifanya hivi heshima yetu sisi kama Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali itakuwa imetendewa haki zaidi, ukiangalia matumizi yaliyoenda kwa wasanii, ukiangalia matumizi ambayo yamefanyika kulipa makampuni mengine utaona kabisa kuna kitu kilikuwa kinakimbizwa ambacho hakikuwa na sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika hapa nafikiri inatakiwa tuende mbali zaidi, kulikuwa na aina fulani ya matumizi mabaya ya

madaraka ambayo yalikuwa yamejitokeza wakati jambo hili linafanyika. Tulimtaka Afisa Masuhuli atueleze wakati ule tunamwita, yeye kama mtu ambaye anasimamia sheria na taratibu, hatua gani amezichukua kwa wale wote waliokuwa wamelifanya jambo hili nje ya utaratibu? Kimsingi utaona kama kuna kulindana na jambo hili limeachwa mikononi mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kupitia Bunge lako na mapendekezo ambayo tumeyaleta, basi tunaomba tupate nguvu ili wale wote waliohusika na kutumia fedha hizi nje ya utaratibu, basi tuone hatua bayana zinachukuliwa ili kuweza kuwatia nguvu watu wengine ambao wamekuwa wanasimamia na ili tuhakikishe wananchi wetu wanapata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Elias Masala. Nilishamtaja Mheshimiwa Ali Hassan King na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuweka kuwa wazima na kuweza kutizimiza wajibu wetu kama Bunge kuweza kujadili matumizi ya Serikali, ambayo fedha zake pengine kwa njia moja au nyingine zimeonekana hazikwenda sawa na tija iliyotarajiwa ambazo zilipitishwa na zillidhinishwa na Bunge lako hili Tukufu. Nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze katika hoja ya Kamati ya kiasi ambacho ni kikubwa kilichotarajiwa kukusanywa na TRA lakini kwa bahati mbaya kwamba kiasi hicho kilipata changamoto. Na katika muktadha huo nitazungumzia thamani ya zile *tax arrears* ya jumla ya Tanzania *shillings* bilioni



303 lakini pia thamani ya Tanzania *shillings* bilioni 84.6 ambazo hizi hazikukusanywa kutokana na Bodi za Rufaa na Mashitaka za TRA hazijakutana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwenye hii Idara ya Ushuru wa Forodha ambayo kumetejwa hiyo amount ya *tax arrears*. Pamoja na mapendekezo ya Kamati ambayo yametoka na maelezo ya wajumbe tofauti ambao wameeleza hapa katika kiasi hicho mara nyingi sisi kama Bunge tunaweza hapa tukaja mwaka wa mbele unaokuja tukaja tukapitisha hapa *tax amnesty*; kwamba kuja kutoa misamaha ya kodi kwa wale waliochelewa kulipa kodi. Sasa hapa sababu iliyotajwa na Kamati ni kwamba wafanyakazi wa TRA katika suala hili la ushuru wa forodha hawakufuatilia kwa karibu utaratibu wa forodha na kutofanya usuluhishi; hii ndiyo iliyokuwa sababu ambayo iliyotolewa. Sasa kama sababu ilikuwa hiyo ina maana kwamba hii sababu ndiyo iliyotukosesha kupata hayo makusanyo ya bilioni 303.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wangu nilikuwa na ushauri. Kwanza ufanyike uchunguzi (*investigation*) katika kosa hili kwasababu tukiangalia kwamba hawa watu wameajiriwa pale na lengo lao ni hili kwahiyu wanakosaje kutimiza zile taratibu?

Mheshimiwa Spika, lakini kingine tuangalie kama watakuwa hawana *imprest* katika hili kwasababu hapo mbele tutakapokuja kusema kwamba tunaweka *amnesty* ina maana kwamba kile tulichokusudia tukikusanye kama tuliweka labda pengine kutakuwa kuna *fine* na *interest*, kwa maana hiyo zitakuja zitakosekana kutokana na hii gap ambayo itakuja kupitishwa ya *tax amnesty*. Kwa hiyo hizo *transactions* kwanza ziangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu lingine nashauri tutakapokuja kupitisha *tax amnesty*, kama tutagundua haya mapungufu pengine labda yalikuwa ni kwa makusudi kufanya ku-*delay*, kwa maana hiyo hiki kiwango au hizi *transaction* zisije zikaja zikapata hiyo *tax amnesty*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kingine, Serikali nayo ingekuwa karibu zaidi na kuangalia wadanyakazi wake kutokana na uwezo wao. Kwasababu tumewaajiri wao kwa uwezo wao wangeweza kufanya vitu hivyo, lakini sasa hawakufanya, wamechelewa na hawakufanya huo usuluhishi kwahiyu tumekosa hicho kiwango cha fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na yote, kuna msemo wa Kiswahili unasema kwamba "Mhalifu mchinjeni sheria yake mpeni". Kwamba inawezekana pengine walikuwa na *transactions* nyingi, inawezekana pengine makusanyo yalikuwa makubwa lakini walipitiwa katika eneo hili, kwahiyu uchunguzi ni lazima ufanyike kwasababu katika nchi hii ushuru wa forodha ni miongoni mwa *amount* kubwa inayochangia mapato ya Serikali hasa ya kodi; kwa maana hiyo hapo tujaribu kuwa makini na tujaribu kutazama.

Mheshimiwa Spika, nilikusudia niliseme hilo kwasababu kuna kitu inaitwa *time value of money*. *Time value of money* katika *theories* zake inasema kwamba *a shilling of today is more worth than a shilling of tomorrow or next year*. Kwasababu fedha hizi kama zingewekezwa au zingegharamia miradi katika miaka hii basi zingepatikana na thamani nzuri kuliko zitakapokuja kulipwa kama zitagharamia miradi kwa wakati huo. Hilo moja katika upande wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, lakini katika upande wa *TRA* kuna bilioni 84.6 ambazo zinatokana na vikao vya kikodi kutokukaa; vikao ambavyo tunaambiwa kwamba sababu Wajumbe wake huwa wanakosekana. Kuna Makamu Mwenyekiti hajachaguliwa lakini pia kuna wajumbe 10 ambao hawajafika. Mimi nilikuwa nashangaa, hivi kweli Tanzania tukakose sifa ya kuwa na Wajumbe katika Bodi hii?

Mheshimiwa Spika, nishauri kwa mamlaka zinazohusika kama hili tatizo lipo la kuteua Makamu Mwenyekiti na kupeleka hawa wajumbe wengine 10 basi wapelekwe, kwasababu bilioni 84 ni pesa nyingi sana. Kwahiyu kama tutafanya hivyo tunaweza tukafanya miradi mingine ambayo imetukabili katika nchi yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije katika hili suala la vitambulisho. Suala la vitambulisho kusema kweli hata mimi hapa nilipo sina Kitambulisho cha Taifa; na Kitambulisho hicho cha Taifa mimi nilianza kuandikisha tangu mwaka 2014 nikiwa mfanyakazi wa Wizara ya Fedha kule Zanzibar. Tumeandikisha hivyo vitambulisho tangu mwaka huo kila mwaka ukienda unapigwa danadana. Sasa tangu mwaka 2014 hawa taasisi hii ya vitambulisho ilikadiriwa na *National bureau of statistics* (watu wa takwimu) ilikadiriwa kufanya vitambulisho milioni 27, lakini hadi Aprili vitambulisho vilivyotoka ni milioni sita. Kwahiyo hapa utaona hapa hi *gap* imesababishwa na nini? Sasa kumbe huku ndiyo haya mambo ambayo yamefichuliwa na CAG.

Mheshimiwa Spika, ukitama katika vitambulisho, watu wa TCRA walikusudiwa zisajiliwe line milioni 43 lakini line zilizosajiliwa zilikaribia milioni 43, lakini Je, vitambulisho vilivyotumika hapa ni vipi? Utakuja kukuta kwamba watu wamesajiliana vitambulisho, wamesajiliana hizi line kupitia hivi vitambulisho ambacho si chake. Kwahiyo watu waliosajili hivi wanahesabiwa ni makosa, lakini hili kosa ni la nani? Kosa ni la ofisi ya vitambulisho na si la wananchi; ingawaje wananchi wao ndio wamekwenda kule wakafanya hilo kosa la kusajiliana line lakini kosa la kusajiliana line ni kosa la ofisi ya vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja ambao napenda sana kuutumia; ikiwa baba amewaambia watoto wake baada ya dakika 10 nataka nyote muwe mmeshalala, lakini kuna wengine wako *mile* 10 au *mile* 100 nyuma je, watawahi kulala ndani ya nyumba? Watoto waliowahi kufika mwanzo ndiyo watakaopanga mito kumdanganya baba yao kwamba na hawa wwamesharudi. Kwahiyo hawa watoto waliopanga mito kumdanganya baba yao na hawa waliopangiwa mito tukiwafanya wana makosa in maana kwamba tutahukumu sivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii amri ya kwamba kila mmoja aisajili line imekuja mahali ambapo vitambulisho havijakamilika. Wangetupa kwa ile ile takwimu tu, kwamba

visajiliwe vitambulisho kwa miaka hiyo milioni 27, lakini vitambulisho vilivyotoka ni milioni sita; na namba nyingine za vitambulisho zimetoka lakini vitambulisho havijatoka. Kwahiyo, nilikuwa naomba Idara ya vitambulisho pia ibebe huu msalaba wa kwamba, kwanini watu wamesajili kwa kutumia vitambulisho visivyo vyao? Na hilo kosa lipo lakini watabebeshwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo hapa kwenye *NIDA* ni lazima waje watueleze na Serikali ifanye uchunguzi kuna makosa mengi yanatokea kutokana na hivi vitambulisho kumbe matumiiz hayakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, kingine nje kwenye ufanisi wa *TPA*. Pamoja na ukaguzi huu uliofanywa na maoni haya ya *CAG* ambayo ameyapeleka, na fedha hizo ambazo zilizosemwa hapa na *CAG*, ambazo ziko shilingi bilioni mbili na bilioni 1.8, lakini mimi nilikuwa naomba *CAG* aende *further* zaidi. Bandari yetu ndiyo iliyotufanya tukajenga yale madaraja Dar pale. Tumejenga *flyover* kwasababu ya Bandari, tuna Ubungo *interchange* kwasababu ya Bandari, tuna mradi huu wa reli ya mwendokasi kwasababu ya Bandari lakini tuna mradi wa njia nane za kutoka Kimara mpaka Klbaha kwasababu ya Bandari. Kwa maana hiyo thamani ya miradi hii ni kwasababu ya vitu ambavyo vitapita bandarini. Sasa, kama ufanisi wetu katika bandari haujakaa sawa ina maana kwamba tunaweza tuka-*incur costs* nyingi na Bandaroi isituletee tija.

Sasa nilikuwa naomba ufanyike huo uchambuzi wa kutazama tija ambayo itapatikana kwasababu miradi mingi hii ya hapa inaitegemea bandari; utanuzi wote huu tunaofanya wa njia ni kwasababu ya Bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King. Nilishamtaja Mheshimiwa Dkt.Shukuru Kawambwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa fursa hii ya kuchangia hoja iliyo mezani lakini nitangulize kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na kutuwezesha kufanya shughuli zetu za Kibunge kwa kipindi hiki chote cha kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kukupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo unaendelea kuifanya ya kulingoza Bunge letu kwa umakini na kwa ufanisi. Kazi uliyofanya ni kubwa kwa kweli tunakushukuru mno, na kama walivyosema Wabunge wenzangu waliotangulia tunategemea wananchi wa Kongwa wataithamini kazi hiyo na kuweza kukurejesha tena katika nafasi hiyo uweze kuitumikia zaidi taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ufupi sana nichukue fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti kwa kuitumikia Bunge lakini kwa kukusaidia vizuri sana katika kuliendesha Bunge hili; na niwapongeze Watumishi wa Bunge kwa kulihudumia Bunge vizuri na kutuhudumia sisi Wabunge vizuri kiasi cha kutuwezesha kufanyakazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kwahivyo naomba nichukue fursa hii kuunga mkono mapendekezo ya Kamati lakini pia kuwashawishi Wabunge wenzangu kuweza kuyapitisha mapendekezo haya kuyakubali na kuitaka Serikali basi ifanyie kazi mapendekezo haya kwa ukamilifu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kuongeza sauti katika baadhi ya maeneo ambayo tumeyachambua na kuyatolea mapendekezo na Kamati yetu. Mmojawapo katika hoja hizi ni uwekezaji wa *NSSF* katika Kampuni ya Mkulazi Holding. Kama taarifa inavyosema Mkulazi haijafanya vizuri, na huu ni uwekezaji mkubwa wa Mfuko wetu wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Mpaka tarehe 30 Juni, 2019 Mkulazi imepata hasara ya jumla ya shilingi bilioni

8,870,000,000; ni hasara kubwa. Hii pesa ni sawa sawa na asilimia 30 ya uwekezaji katika Kampuni hiyo. Sasa hili ni tatizo kubwa kwasababu uwekezaji huo; maana tunahesabu sasa *NSSF* sasa iko hatarini kupoteza pesa kwa vile wao Kampuni hii ya Mkulazi wanaimiliki kwa asilimia 96, asilimia zilizobaki nne ni za Magereza, kwahiyo kiasi kikubwa cha fedha zinatokana na *NSSF*. Sasa ni muhimu sana kwamba Mkulazi ianze uzalishaji, kwasababu hasara hii imekuja kwa kiasi kikubwa au mchango mmoja mkubw ani kuchelewa kwa uzalishaji wa sukari katika kampuni hiyo. Uzalishaji huo ulitegemewa ufanyike katika msimu wa Mwaka 2018/2019 lakini haukufanyika, mwaka 2019/2020 haukufanyika, na sasa kama itaendelea hivyo kutokufanyika maana yake baada ya miaka michache pengine mtaji wote ule wa *NSSF* utakuwa umeliwa na hela za wachangiaji wa *NSSF* zitakuwa zimepotea.

Mheshimiwa Spika, mimi nitegemee kwamba *NSSF* kama wawekezaji watasimamia kwa nguvu zao zote kuhakikisha kwamba Mkulazi inaanza uzalishaji; na ikiwezekana ianze uzalishaji katika msimu huu unaofuatia wa mwaka 2020/2021; iweze kuanza kuzalisha sukari ili mahitaji yetu ya sukari yaweze kukidhiwa na uzalishaji huu zaidi lakini pia kuepuka hasara ambayo inaweza ikaipata *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkulazi hili jambo ni muhimu sana na *NSSF* kwa ujumla kwasababu *NSSF* imewekeza katika miradi mingi na mpaka hivi sasa tunafahamu kwamba katika miradi kadhaa ambayo *NSSF* imewekeza haijaweza kurejesha tija ile ambayo tulikuwa tunatarajia; kwa maana kwamba fedha ya wachangiaji wa mfuko huu iko hatarini.

Sasa niitake na niombe Serikali ikiongozwa na *NSSF* yenyewe kufanya tathmini ya kina ya mradi huu ili ione namna gani bora zaidi itakayoweza kupatikana kwa ajili ya kuendesha mradi huu ili kuepukana na hasara. Kwasababu hasara hii ikipatikana na hasara inayoweza kupatikana katika miradi mingine ambayo haijaleta tija, lakini pia kwa kutambua kwamba *NSSF* ina fedha ambazo imeikopesha Serikali ambayo bado haijarudishwa; hapa mchangiaji wa

*NSSF* kwa maana ya wastaafu hawa watakuwa kwenye hatari moja nzito sana kwamba pale watakapokuwa wamestaafu basi na hela zao hazipo kule. Wamefikia muda ambao wanazihitaji sana hizo pesa lakini pesa zile hazipo na kipindi cha kustaafu ni kipindi kigumu bila ya kuwa na fedha ya kukukimu maana yake huwezi ukaendesha maisha kistaarubu na kiufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, naomba nitilie mkazo tu katika maoni ya Kamati kwamba... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shukuru.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** ...kwamba *NSSF* ihakikishe kwamba mradi huu unakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza?

**SPIKA:** Wanasema ya pili...

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Ya pili?

Mheshimiwa Spika, basi naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri iliyofanya, ninaunga mkono maoni ya Kamati na naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono mapendekezo haya na Serikali iweze kuyafanyiakazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia haya maoni ya Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe mwenyewe kwa hii miaka mitano inayokwisha, na kwa kweli wakati fulani tulikuwa tunakuomba na kuna kipindi ulipopelekwa India mimi nikawa nalala usingizi naumwa sana; lakini tulikuomba ukafika ulikofika na Mungu akusaidie mpaka kwenye Bunge litakalokuja na uendeleo kuwepo. Niwaombee viongozi wote waliopo na kusema kweli nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa msimamo wake wa kutokoa katika janga hili la corona. Msimamo tu wa kututoa hofu tu umetusababisha watu wengi wawe na uzima wa milele kwasababu hofu ilikuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nimekiona hospitalini hapa nilipokuwa napitapita; niombe Wizara ya Afya ituambie maana yake sasa inaonekana watu wanaogopza zaidi Jeneza la maiti ya corona kuliko watu wenyewe kujikinga. Sasa wanapokwenda watuambie maiti ya corona ina ugonjwa wa Corona au inakuwaje, ili tuweze kujua kwamba tunapokuwa tunazika sasa uangalifu uko wapi. Uko kwenye Jeneza au uko kwa watu ambao tunazika watu, ili tuweze kujua kinachoendelea huko mbele ili watu waweze kuendelea kuzika watu wao kama Mheshimiwa Rais alivyosema kwa heshima.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia hapa matatizo yaliyopo kwenye makusanyo ya TRA. Huwa najiuliza, kwa mfano; ukiangalia TRA yale madeni, madai ya mashauri wanayosema ni bilioni 84.6. Haya madai ukiangalia vitabu vyote vya bajeti, mimi tangu nimeingia hapa Bungeni naliona; madai! Madai! Madai!

Mheshimiwa Spika, siku moja nilimuuliza mtaalam mmoja wa *TRA* ananiambia kwamba wakati fulani madai haya yanakuwepo kwasababu hakuna bodi ya kushughulikia madai haya; wenyeviti wa Kamati hizo za madai unakuta hawapo. Sasa najiuliza, kama wananchi wa kawaida wa ushirika wakila hela TAKUKURU iko pale inakusanya hela, kama korosho wakila hela TAKUKURU wanakusanya hela, ni kwanini mashirika ya umma na madai mbalimbali ya *TRA* TAKUKURU hapo haioni au kuna nini?



Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni vizuri sasa tukaamua haya mambo, maana yake ukiangalia bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, mwaka wa fedha 2017/2018, mwaka wa fedha 2018/2019 na mwaka wa fedha 2019/2020 mambo ni yale yale, ya *TRA*; ukusanyaji mbovu, ukwepaji wa kodi na vitu vingine madai na mashauri bilioni, bilioni, bilioni, bilioni.

Mheshimiwa Spika, sasa najjuliza, kama tuna shida ya kupata fedha kwenye maeneo mbalimbali, tuna majengo ya shule, bado maboma yako wazi; tuna zahanati, ziko wazi; sasa hizi fedha zinakaa miaka nenda, rudi, kila bajeti tunazona humu ndani. Hiyo Bodi inayosimamia haya mashauri inaundwa na nani? Inaundwa na Mheshimiwa Waziri au tumwombe Mheshimiwa Rais aingilie kati kwenye tatizo hilo hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa niishauri hii Wizara kama inayohusika na Mheshimiwa Rais kama Wizara hii inaonekana imeshindwa kutekeleza wajibu wa madai haya ili tujue. Maana yake juzi juzi hapa walisema kwamba wale watu wanaodaiwa wamepewa muda wa kwenda kujitoa kwenye yale madeni yao kulipa au kupunguziwa lakini bado bilioni 84 ziko hapa. Ukija *TRA* kuna milioni 303, bado zinadaiwa kwenye madai, sasa ukiangalia *TRA* ukusanyaji, *TRA* madai, *TRA* mashauri, kwa hiyo nafikiri kwamba ni vizuri sasa tufike mwisho wa mambo ya *TRA* tujue kwamba ni kitu gani kinaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *NIDA*, sasa huwa najjuliza kwa nini Mashirika ya Umma yanakuwa na shida sana kuliko Mashirika ya *Private*. Ni kwa sababu watu wetu wengi tunawapeleka kutumikia mashirika mbalimbali kwa kufuata kisomo chao bila kuangalia maadili yako. Kwa nini Mashirika ya *Private Sector* yanakuwa *result oriented* lakini huku kwetu hakuna kinachofanyika. Uende *ATCL* matatizo, uende Bandari matatizo, uende *TANESCO* matatizo, kwa nini? Kwa nini sasa tusifanye utaratibu wa kufundisha watu maadili ili wajue kwamba kutumikia Taifa ni pamoja na kujitoa mhanga. Tunakaaje na watu kila shirika bovu, shirika bovu.

Mheshimiwa Spika, hivi inawezekanaje leo watu wangu wa Bunda wanateseka sana na mambo ya *NIDA* hawana vitambulisho, hawana nini, hapa kuna bilioni 42 zimetumika hovyoy, zimenunulia vifaa vya hovyoy. Bilioni 42 ukizipiga kwenye hesabu ya kawaida hivi ni vituo vya afya 84 *cash* na zahanati 210 lakini zimetumika vibaya. Watu wanateseka na vitambulisho, watu hawana vitambulisho, hela zimeliwa, wamenunua vitu vibovu na watu utakuta bado wanaendelea kuwepo. Kwa hiyo nishauri, Waziri yeyote anayehusika na Wizara, kama hatua hiyo kama kila siku tutakuwa tunaletewa mambo yale yale. Kwa mfano Bunge lijalo tena tutakuta hoja hiyo hiyo, Bunge linaendelea na hoja hiyo hiyo, linaongeza hoja hiyo. Nadhani ufike wakati sasa tutengeneze utaratibu maalum hapa Bungeni, kwa maana kama wameshindwa kuamua huko, tuamue wenyewe hapa, kama tukiweza kuamua, tunaweza kutenda mambo mazuri kwenye jambo kama hili.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya Mashirika ya *PSSF* na *NSSF*, haya mashirika mimi sisemi kwamba fedha haipo, najua yana fedha, lakini sioni mfumo maalum ambao unamfanya mtu ambaye ametumikia Taifa hili miaka 30, anapostaafu anapewa fedha yake kwa wakati. Watu wanateseka sana kwenye mashirika haya, kwa nini tusitengeneze mfumo maalum kwa mashirika haya, siku ukipewa barua yako ya kustaafu unapewa na *cheque* yako. Shida iko wapi kwa sababu fedha ametoa miaka yote na fedha ni ya kwake siyo ya kuomba, siyo hiari, lakini leo watu wanateseka, wanateseka. Nafikiri sasa Waziri anayehusika na mambo haya ya Mifuko aangalie utaratibu maalum wa kuwapa watu fedha yao wakati wanastaafu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *Pride*, sasa mtu anasema fedha ya *Pride* ilikuwepo ikaenda ikarudi, ikaenda ikarudi, fedha ya umma. *Pride* bado ipo, benki bado zipo eti hiyo nayo imekuwa hoja! Suala la kutamka tu fedha kesho irudi kwenye benki yake, anayekataa ni nani kwenye Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa nini hatuna sauti ya kusema fedha za umma zirudi? Mbona za watendaji wa Kata wanakamata, za nani wanakamata, hizi za watu

wakubwa hawa ni akina nani ambao fedha za umma zinaliwa mabilioni hawarudishi? Ni akina nani hawa ambao leo wanaweza kushinda Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mambo mengine haya tuamue kwenye Bunge hili, tuwe tunaamua kwamba hili bwana hatulitaki tena tunataka liishe, likiisha Waziri ambaye hakushughulika na jambo hili tumshughulikie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati na Kamati imefanya kazi nzuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere. Nilishakutaja Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami kuchangia kwenye mjadala huu muhimu. Nianze kwanza kwa kuweka *record* kwamba, ni kwa masikitiko tu kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano kwa miaka yote mitano or *rather* minne wameshindwa kukusanya mapato kama ambavyo tumekuwa tunaidhinisha *projection* zao zimeshindwa ku-*reflect the reality* uhalisia *except* kwa mwaka 2015/2016 walau walivuka kwa 0.13 na nadhani ni kwasababu ya malimbikiko ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ripoti ya CAG amebainisha kabisa kwa mwaka 2018/2019, *projection* ya Serikali ilikuwa ni trilioni 18.2, lakini wakakusanya tirioni 15.7, wakaenda *short off* 2.5. Nimeanza na *preamble* hii kwa sababu kutokukusanya mapato na sababu alizozielezea CAG zina-*reflect* kutokulipa madeni ya wakandarasi na kuweza kule athari kwenye fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ile *report* utaona kwamba TANROAD waliweza kupigwa penati ya bilioni 225 kwa sababu hawajalipa madeni ya wakandarasi kwa muda muafaka. Hizi bilioni 225 tunavyoongea sasa hivi nchi yetu

ina uhaba mkubwa, kwa hiyo kama wamesema wamejenga vituo vya afya 300 kwa miaka 5 hizi bilioni 225 ambazo zinapotea tu kwa uzembe na kutokuwepo na usanifu na Wizara ya Fedha kutopeleka kwa wakati. Bilioni 225 ukigawa kwa milioni 400 ambazo ukipeleka katika vituo vya afya, tuna vituo vya afya 563, tungejenga vituo vya afya 563.

Mheshimiwa Spika, ukisema upeleke kwenye maboma, madarasa ambayo Watanzania, wanajichangisha kuku, mbuzi wanajenga Watanzania maskini, tuseme boma la darasa zuri la bilioni 20, wangejenga vyumba vya madarasa 11,250 na zaidi. Hizi bilioni 225 kwenye adha ya maji ambayo akinamama wanatembea, nikichukua tu *experience* ya ndugu yangu hapa Kitwanga, lakini huu ni mradi wa fedha kutoka India kwa kule, Tarime wataleta walau bilioni 14 kuweza kujenga maji kutoka Ziwa Victoria; tukigawana zaidi ya miji 15 ingeweza kupata utatuzi wa kudumu wa maji kwenye miji hiyo hizi bilioni 225.

Mheshimiwa Spika, sasa awamu hii wanasema hapa kazi tu, ufanisi na uwajibikaji, tungependa kabisa haya mambo yasitokee kwa sababu hizi ni fedha za walipa kodi maskini. Mtanzania maskini analipa hizi kodi, zinaenda kutumika kwa uzembe kabisa. Niombe Bunge lako liweze kukemea hili na kusema kabisa kama wanaingia mkataba basi walipe *on time*, kama wana makusanyo ambayo wanasema yanakuwa na *surplus* walipe *on time* hili Taifa lisiingie hizi hasara za mabilioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye *NIDA*, kwenye ripoti ya *CAG* na kwenye taarifa ya ripoti ya *PAC* wameainisha kwamba dosari mbili kuu; utunzaji wa hizi malighafi ambazo ni haffu, hizi malighafi milioni 42; hizi malighafi ambazo ni milioni 5.4 na kitu ambazo wamesema zingeweza kutumika kwa siku 677 kuzalisha vitambulisho 8,000 kwa siku, lakini zaidi hizi malighafi za milioni 42 zimeletewa mtambo ambao siyo *compatible*, huo mtambo ambao umenunuliwa haviendani kuweza kutumia hizi malighafi ili kuzalisha vitambulisho. Sasa haviingiliani kabisa, vifaa vya vya uzalishaji uweke 42 bilioni,

unanunua mtambo ambao hauji kutumia hivyo vifaa vya uzalishaji kuzalisha vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, wote tunajua kwa sasa hivi Watanzania wanapata adha kubwa kutokuwa na vitambulisho, CAG amesainisha vizuri kwamba walisajili vitambulisho milioni 21. Katika vitambulisho milioni 21 vilivyosajiliwa, Watanzania waliopewa namba za vitambulisho milioni 17, Watanzania milioni 4.5 na kitu hawakupata namba za vitambulisho. Katika hivyo milioni 17 waliopata namba ni vitambulisho milioni sita tu, wakati tuna Watanzania ambao *legible* kupata vitambulisho zaidi ya milioni 30 na kitu. Leo unasema una milioni sita umewapa tu vitambulisho, wakati unajua kila unapokwenda unadaiwa kitambulisho cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe rai yangu, mosi, uweze kufanyika ukaguzi maalumu (*forensic auditing*) katika hii, ni kwa nini walinunua mitambo ambayo siyo *compatible* na malighafi zilizoko? Pili, kama Serikali imeshindwa hii *project* ya vitambulisho vya Taifa ni bora ivifute kabisa turudi huko tulipokuwa mwanzoni, bila vitambulisho vya taifa ili tuendelee kutumia kama ni kitambulisho cha kazi, kama ni leseni ya udereva, kama ni kitambulisho, sababu Watanzania wanateseka, hii adha tu ya simu Watanzania wengi sana wameteseka. Kwa hiyo kufanyike ukaguzi maalum kuweza kujua ni nini kipo nyuma ya pazia kuhusu matumizi ya hizo fedha ambazo wamenunua limtambo ambalo haliendani na malighafi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeona kwamba kuna taasisi mbalimbali za umma na binafsi ambao zinatumia taarifa za *NIDA*, lakini ripoti imeeleza *NIDA* hawana mkataba bayana kwa watumiaji wa hizi taarifa. Kwa kufanya hivyo ina maana kuna mapato mengi sana yanapotea. Kwa hiyo hili nalo, liweze kuchukuliwa kwa uzito na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, hii Serikali kulikuwa na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto Dodoma, lenye kugharimu 1.7 bilioni. Eti hizi fedha zikafanyiwa *transaction* kutoka Dar zikaenda Singida,

wakisema kwamba Dodoma hakuna Makao Makuu ya Hazina, hakuna Hazina Ndogo yaani kuacha benki kule na hapa hakuna Hazina, wakati tunavyoongea, tunajua tuna hazina hapa ipo. Sasa wanafanya *transaction* kutoka Dar kupeleka Singida halafu wanapakia fedha bilioni 1.7 kwenye mabegi yanakuwa *escort* na gari kuja Dodoma. Mtu yeyote yule ukimwambia kwa sasa hivi ilivyo hawezi akakubaliana kama hiki kitu kilifanyika. Kama kweli kilifanyika pia hapa kichunguzwe *what was behind it*, kwa sababu tuna hazina hapa. Kwa nini wapeleke Singida halafu wazilete kwa mabegi kuleta Dodoma.

Mheshimiwa spika, kitu kingine, ilibainishwa kwamba *TBA* waliingia hasara ya 8.85 billion kwa sababu walikuwa na mkataba wa kujenga jengo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi hapa Dodoma, wakakatishwa kwamba wamejenga ziada ya makubaliano. Kwa hiyo wakakataliwa kulipwa lakini ikawa *sub contract* kwa SUMA JKT, wengi hapa tunajua *TBA suffocated*, kwanza inalundikiwa miradi mikubwa sana na Serikali, halafu Serikali haipeleki fedha. Kwa hiyo unakuta inatumia kwa mfano wametakiwa kujenga mradi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inatumia fedha walizonazo kuweza kujenga hilo, halafu baadaye ukikatili ukaacha kulipa unawapa SUMA JKT wakati hujamlipa hata hiyo fedha, kwanza ni Serikali wenyewe, maana hili shirika ni la Serikali, wanajiingiza hasara wao kwa wao.

Mheshimiwa Spika, niombe kupitia Bunge lako Tukufu kama tunataka *TBA* iendelee kuwepo tuweze kuwasaidia, mosi, mtaji; lakini pili tuangalie *labour force* yao wana rasilimali watu wa kutosha, kuliko kufanya shirika litakuwa lina-*operate under loss*, bora tuliondoe tubaki tuwe tunatumia mashirika mengine kama mnavyoona sasa hivi katika Awamu ya Tano SUMA JKT ime-*take charge* kuweza kufanya miradi ya ujenzi, basi bora tuivunje hii *TBA* tuwache *SUMA JKT wa-proceed* kuliko haya ambayo tunafanya na huku Serikali inapata hasara.

Mheshimiwa Spika, kingine, kwenye ripoti ya *CAG* imeonyesha kabisa kwamba kulikuwa na makusanyo ya *TRA*

kwa mwaka 2018/2019 ya bilioni 7.06 ambayo ilikuwa ni tozo ya mafuta, wamezikusanya lakini hawakuweza kuzipeleka kwenye Mfuko wa Barabara. *TRA* kukusanya hizi bilioni na kuacha kupeleka kwenye Mfuko wa Barabara ina maana tutaendelea kuona barabara mbovu kwa sababu kwenye Mfuko wa Barabara ndiyo tunapata za kufanyia kazi kwa kuwa zingine zinaenda kule *TARURA*. Sasa ni lazima Bunge lako Tukufu liweke msisitizo leo kwamba kila *single cent* ambayo inakuwa imekusanywa iweze kupeleka kwenye huu mfuko. Sasa *TRA* inakusanya *billions of money*, halafu inakaa nazo bila kupeleka kwenye mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, wamezungumza sana, kwa kweli nisingetaka kuzungumza sana kuhusu *TTCL* maana yake ni kama wamesha-*exhaust*, lakini nizungumzie usugu wa Serikali kutokulipa madeni siyo tu kwa *TANESCO* kama ilivyoainishwa hapa. Wabunge wamezungumza kuhusu madeni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutokulipwa, lakini hata hapa unaona *TANESCO* wameainisha zaidi ya bilioni 205 ambazo taasisi za Serikali zinadaiwa. Hapa ni *TANESCO* tu hujapitia kwenye mamlaka ya maji, nayo inadai *billions of money* ambayo ni taasisi ya Serikali, inashindwa kulipa, kwa hiyo ningependa tuitake Serikali *at once* kupitia hizi taasisi mbalimbali basi waweze kulipa haya madeni ili hizi taasisi zingine kama *TANESCO*, Mamlaka za Maji ziweze kujiendesha, lakini pia wakandarasi binafsi waweze kulipwa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wengi sasa hivi hata wengine wanashindwa kutoa huduma kwenye taasisi za Serikali kwa sababu Serikali imeshindwa kulipa madeni kwa hao wakandarasi. Kuna wengine walichukua mikopo benki wanaamua hata kujitoa uhai wao kwa sababu watakuja kuuza rasilimali ambazo waliziweka kama dhamana wakati wanachukua mikopo. Kwa hiyo nitoe rai kabisa, kwa mfano huu wa madeni ya *TANESCO*, basi Serikali ihakikishe inalipa madeni ya wakandarasi ili kuacha kupata hasara kama nilivyoainisha mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, pia hii ya *REA*, kuweza kum-*assign* mkandarasi mtaalam wa ushauri kwa ajili ya miradi ya *REA*,

*whether* bilioni moja *point something*, halafu baadaye hawatumii, hata hiyo ripoti haijakamilika wanaenda na kuanza ku-*assign* wakandarasi wa kwenda kujenga miradi ya *REA* vijijini. Kama ambavyo Kamati imependekeza niweke tu msisitizo kwamba ni kweli, ni wakati sasa tuweze kujua ni kwa nini tunapoteza fedha za walipakodi maskini bilioni moja *point something* kuweza kwenda kum-*assign* mtu, halafu hafanyi hiyo kazi, halafu unamlipa yote. Bilioni moja ukigawa kwa madarasa, tunaweza kujenga zaidi ya madarasa 500.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuweze kukazia hayo na kuitaka Serikali hii ambayo inasema inafanya mambo kwa ufanisi, inawajibisha watendaji ambao hawafanyi mambo kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi, waweze kutuambia haya yote ambayo yameainishwa na *CAG* kwenye hii hii Serikali ya Awamu ya Tano yamewezekanaje kufanyika. La kusisitiza zaidi ni kwamba, zifanyike *forensic audit* pale niliposisitiza na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia zote. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Matiko. Nilishakutaja Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Elibariki Kingu, halafu sasa atafuata upande wa Serikali.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Taarifa ya Kamati. Pia nikushukuru kwa kunipanga kuwa Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, nimejifunza mengi katika Kamati hii ambayo kwa kweli ni jicho la Bunge kuangalia Mashirika ya Umma na Serikali kwa ujumla jinsi inavyotumia fedha ambazo zinapitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja kwamba naridhika na taarifa hii pamoja na mapendekezo ya Kamati. Yako mambo ambayo Kamati imeshauri ambayo kimsingi yakifanyiwa kazi tunaweza kubadilisha kabisa sura ya mashirika ya umma katika uendeshaji na utumiaji wa



fedha. Tunalo tatizo la kutokuwa na muda wa kuchukua hatua na kurekebisha upungufu. Ni vizuri tufike mahali tuwe na muda kwa sababu haiwezekani kila mwaka shirika hilo hilo linarudia kuwa na hoja hizo hizo halafu hoja hizo hazifanyiwi kazi. Inaonekana sasa kwamba sisi kama Bunge maagizo ambayo tunayatoa na ushauri kwa Serikali ni kama tunapoteza muda. Kwa hiyo niombe sana haya mambo ambayo sisi kama Kamati na Bunge kwa ujumla tunashauri ni vizuri yakafanyiwa kazi kwa muda.

Mheshimiwa Spika, tumeona upungufu *NIDA, NIDA* wananchi wana shida kubwa sana kule vijijini sasa hivi wengine walipigwa picha kule vitambulisho vyao havijaja na kwasababu hiyo imefika mahali wananchi wanaambiwa kwenda kupiga picha makao makuu ya wilaya kilometa 130 wengine kilometa 170 ili wafike makao makuu ya wilaya, lakini ukija kuona hapa kuna vifaa havijatunzwa vizuri vinaingiza hasara Serikali halafu hawa watu ambao walipaswa kuvitunza vizuri hivi vifaa hawajachukuliwa hatua. Kwa hiyo, niombe sana tunaingia hasara kubwa na kuhangaisha wananchi kumbe mamlaka zenyewe, mashirika haya hayasimamii vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumeona hapa fedha ambazo zinapotea kwenye mashirika lakini fedha hizi ni nyingi sana na tumeona pia mashirika haya yanatumia fedha nje ya bajeti wakati yana muda wa kuandaa bajeti kulingana na mahitaji yake halafu tunafika mwisho watu wanatumia fedha nje ya bajeti hili haliingii akilini hata kidogo. Tunao wataalamu waliobobea ni vizuri wakawa wanaandaa bajeti ambazo haziji tena kuingiliana kutumia fedha nje ya bajeti. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kamati yetu imetoa ushauri kwa Bunge na Bunge ni vizuri ukaliona huu ushauri kwamba unafaa ili hatua ziendelee kuchukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ni jicho la kutuonyesha kwamba madhaifu ambayo yanapatikana katika mashirika yetu ni haya, sasa *CAG* anapotubainishia sisi kama kamati sisi kama Bunge kwa ujumla lazima tufike mahala sasa kwamba haya mambo ambayo jameshauriwa na *CAG*

yafikie mwisho. Kwa hiyo niombe sana tuna mashirika yetu haya lazima tuendeleo kuyasimamia na lazima yafate taratibu na kanuni zilizowekwa za utumiaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bonaventura Kiswaga naona kura zinaendelea kupigwa na muendeleo sasa bahati mbaya kuna wale wenzetu ambao wamezoea kupiga kura ya hapana nawakumbusha tu na ziko nyingi hapa nazona za hapana sio za Bunge za hilo kundi. Inapofikia mahali ambapo ni taaria ya kamati ni taarifa yenu Wabunge sasa mtu mwingine kazoea kusema hapana nazona tu hapa, sasa unasema hapana unatarajia nini sasa wakati Wabunge wenyewe ndio mnaleta taarifa hii taarifa ni yenu na ikija ya LAAC pia ni yenu. Kwa hiyo, tunapopiga kura tuwe tunakuwa na umakini kidogo kuna taarifa ambazo ni zetu wenyewe. Mheshimiwa Elibariki Kingu nilisema atakuwa wa mwisho halafu tuanze kusikia upande wa Waheshimiwa Mawaziri. (*Makofi*)

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi kuweza kushiriki kutoa mchango wangu kufuatia ripoti ya CAG na taarifa hii ya PAC. Nianze kabisa kwa dhati ya moyo wangu kwanza kabisa kumpongeza sana kaka yangu Kichere CAG wetu ambaye kipindi CAG huyu anateuliwa na Mheshimiwa Rais zilitoka kejeli nyingi zikifikiri ya kwamba anateuliwa kwa lengo la kuja kuilinda Serikali dhidi ya ubadhirifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa sababu ripoti iliyotokana na kazi za mikono ya CAG mpya kaka yangu Kichere imedhihirisha *beyond reasonable doubt* kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ina dhamira ya dhati kuhakikisha uadilifu na matumizi sahihi ya *Public Fund* yana-adhere to the Principle of Rule of Law. Kwa maana ya kwamba, wengi walidhani Kichere atakapoingia kwenye ofisi hii atakuja kufumbafumba macho na mimi kwasababu ni Mbunge tena ninayetokana na chama hiki leo ninasema

Kichere umetufanyia kazi iliyotukuka Taifa na nchi vinajivunia na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hakuyumba na Spika wetu pia hukuyumba kuhakikisha kwamba Bunge lako unalilinda na kudumisha nidhamu ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye mchango wangu nataka nijikite kwenye maeneo makubwa matatu; la kwanza Serikali yetu ni Serikali ya watu wachapakazi na waadilifu. Lakini tuchukue tahadhari kwasababu siyo *Public Servant* wote wana maadili na hawana tamaa ya kuiba fedha za umma. Siku tukilogwa tukafikiri ya kwamba uadilifu wa Rais wetu ndio uadilifu wa nchi tutakuja kukuta hii nchi imebaki mabua.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano ukiangalia kwa upande wa *TRA* wiki iliyopita nilichangia nikasifu sana utendaji wa Kamishna mpya wa *TRA*, katika *Revenue Collection*. Lakini nataka nikwambie hii nchi bado ina wezi, majambazi bado wapo kwenye *Public Service* na ninataka nikudhihirishie ukisoma ripoti ya *CAG* ukaja uka-*compile* na ripoti ambayo imetengenezwa na Kamati ya *PAC* angalia kwenye maeneo yafuatayo na kama nasema uwongo fuatilieni kwenye ripoti za miaka zaidi ya kumi muangalie wapi wafanyabiashara wasio waadilifu wakishirikiana na baadhi wa *Public Servant* namna gani wanaiba fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, angalia maeneo ambayo nchi inaibiwa nataka nikwambie la kwanza ukisoma ripoti ya kamati namba moja anasema kwenye lile jedwali namba 2 bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi *on transit goods* lakini hazikuwa na udhibitisho wa kutoka kwenye nchi.

Mheshimiwa Spika, nataka niliangalie Bunge lako tukufu hapa ndipo nchi inapoibiwa na haya nimekuwa nikiona toka nikiwa kwenye *Public Service* watu wanaagiza bidhaa wanasema zinakuwa *on transit* zinazuzwa ndani ya nchi kodi haikusanywi, watu wanapiga pesa hatua gani zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, la pili anasema mafuta yaliyoagizwa kutumika hapa nchini bila kuwa na udhibitisho wa malipo ya kodi na riba, hii imekuwaikitokea *every single year*. La tatu, bidhaa zilizoagizwa na kupatikana kuwa na dosari katika mchakato wa forodha haya ni makusudi wengi tunafanya vi biashara vidogo vidogo, wafanyabiashara wasio waaminifu wanafanya haya na wakienda pale kwa watu wa forodha wasio na mapenzi na nchi watu wanapiga pesa.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine bidhaa zilizoagizwa kwa malengo ya kuuzwa nje ya nchi lakini zikabaki hapa nchini. Nataka nikwambie takwimu hizi zinaonyesha mapato ya bilioni 712 fedha hizi zingekuwa *taxed* Serikali ilikwa na uwezo wa kupata *revenue* ambayo ingeweza kusaidia ndoto za Rais wetu kumaliza kujenga hata vituo vya afya kwa zaidi ya mikoa hata saba.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie natoa ushauri *TRA* pamoja na kazi nzuri mnayoifanya Bunge lako linakwenda *extra miles* kwa ushauri wa kamati waanzishe kitengo cha kufanya *monitoring* ya *export of import* kwa maana ya kwamba mnapo-*import* mizigo ambayo *intension* yake ni *destination* za mataifa mengine tuwe na kitengo kinacho-*monitor transaction* yote. Tukiacha hilo nchi hii itaendelea kupigwa tutaendelea kujadili ripoti hapa watanzania wataendelea kuumia na watu wataendelea kutajirika na kufisadika kwa maslahi ya kuwaumiza watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili Wizara ya Utalii, *let us be fair* tuwe *fair* kwa maslahi ya nchi maana kuna wengine wanafikiri ya kwamba tukizungumza hapa tunakuja ku-*attack personality*, uzalendo wa Rais usichukuliwe kama kichaka cha watu kufanya matendo ya kifisadi kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, narudia uzalendo wa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli baadhi ya Mawaziri ninawashauri kaka zangu msichukulie uzalendo wa Rais kuficha mambo yenu yanaweza yakali-*cost* hili Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna dharura gani kaka yangu bilioni moja zitumike kwa mambo ya *Festival* bila Bunge lako kuarifiwa kulikuwa kuna uharaka gani, tuwe tu *reasonable* matumizi ya nia njema *let us be good hope* hatukatai nia njema lakini tukiruhusu mambo haya watapatikana mawaziri ambao watatumia nafasi hii wataiba fedha za umma wata-*embezzle Public Fund* kwa *expense* ya kutumia mgongo wa uadilifu wa Rais, haya lazima tuyasema kwasababu tumebeba dhamana ya kuwasemea watanzania katika jambo hili.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, jambo la tatu...

#### T A A R I F A

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu Mheshimiwa Frank amesimama taarifa

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Kingu nikijaribu kupingana kidogo na taarifa ya kamati kwamba kutokana na upotevu au matumizi mabaya ya 1.5 bilioni kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, nafikiri wasiseme kwamba wanatakiwa wafanye *special audit* kwa sababu mtu aliyefanya ukaguzi huu *CAG* amefanya kazi kubwa sana, nani atakuja kufanya ukaguzi zaidi ya *CAG* aliyeufanya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri Serikali ichukue hatua kama ambavyo ameshauri *CAG* katika ukaguzi wake ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu pokea taarifa

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naipokea taarifa Serikali ichukue hatua, ninaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunayazungumza haya hatu-*attack personality* na ninaomba tukitoka hapa habari ya kununiana tuache *we are here for the interest* ya nchi kama kuna mambo yatakuwa yanafanyika tukaogopa kuyasema tutakuwa tunamtwishia Rais mzigo mzito na sisi kama Bunge tutakuwa tunaogopa jukumu letu la kikatiba la kuisimamia Serikali pale ambapo baadhi ya watu ambao sio waaminifu wanakuwa hawafanyi mambo yanavyotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nataka nitoe ushauri nimesoma Ripoti hii ya *PAC* ukiangalia haya mambo hayafanyiki tu kwa hii Kampuni ya *SMEC* ambayo imepewa kama *consultancy firm* imepewa kazi lakini tena nashukuru kamati wameita *Nugatory expenditure*. Fedha zimepewa kwa Kampuni ya *Consultancy* wamefanya kazi ushauri haujatumika bilioni moja za watanzania zimelipwa makampuni 29 yakapewa kazi yakaenda kuanza kufanya kazi *out of the scope* ya kazi ambayo ilikuwa imefanywa na mshauri. Mambo haya nilikuwa nategemea leo hapa tunapozungumza Taasisi yetu ya Kupambana na Rushwa TAKUKURU nilikuwa nategemea hapa Kampuni ya *SMEC* imeshaitwa kuhojiwa na watumishi wote wa *REA* walioshiriki kufanya mambo haya wameshaitwa kuhojiwa na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, haya mambo tukiyafanya maana halisi ya kusema tunamsaidia Rais tuta-*interpret* kwa vitendo na Serikali yetu itakwenda mbele kwasababu si hoja kwamba Rais wetu ni mwadilifu sana lakini baadhi ya watu wanaweza wakatumia uadilifu wa Rais kufanya mambo ambayo yakaja yakalumiza Taifa na kazi nzuri inayofanywa na Rais wetu wakaitoa doa.

Kwa hiyo, sisi Wabunge tutakuwa tayari kumlinda Rais wetu kwasababu amefanya *commitment* kubwa ya kulisaidia Taifa watu wameona uadilifu wa Rais lakini ninaomba watu baadhi wasio waadilifu wasidandie uadilifu wa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja ahsante. (Makofi)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, leo naomba mchango wangu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa uhai na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu. Lakini nikupongeze wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Naibu Spika mkishirikiana na Wenyeviti wetu kwa kuliongoza Bunge letu kwa umakini na weledi mkubwa. Hakika mmezitendea haki nafasi zenu, Mungu awape umri mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wa leo naomba niungane na Kamati kuiomba Serikali kuzingatia maoni na maazimio yote ya Kamati kwani kasoro nyingi zilizoibuliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni masuala yanayozuilika ikiwa kuna uwajibikaji wa pamoja Serikalini. Kwa hali ilivyo sasa inaonesha kuna kasoro kubwa ya mashirikiano kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine ndani ya Serikali. Jambo hili limekuwa likichangia kwa kiasi kikubwa kuchelewa kwa kufanyika maamuzi mbalimbali, na hivyo kukwamisha baadhi ya miradi kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Idara au Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuwa chini ya Mkurugenzi au Mkuu wa Taasisi husika ni kasoro nyingine. Naomba kuishauri Serikali kuona umuhimu wa Idara hii iwe ni Idara inayojitegemea kuliko kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja zinazojirudia mara kwa mara kila mwaka katika ripoti za *CAG* na zilizo nyingi zake hazina sababu za kuwepo kwake, hapa ninamaanisha kuwa zimesababishwa na utendaji mbovu wa baadhi ya watumishi wa taasisi husika. Hivyo naishauri Serikali kuwa na utamaduni wa kuwachukulia hatua wale wote wanaosababisha kuwepo kwa hoja hizi. Mfano wa taasisi hizi kama vile *BOT, NSSF, TTCL, PSSSF* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi za umma zinazofanya uwekezaji katika miradi mbalimbali nchini, lakini mingi ya miradi hii aidha, imeshindwa kukamilika kwa wakati au hata

pale ilipokamilika imeshindwa kuleta tija iliyokusudiwa. Kosa kubwa linalofanywa katika miradi hii ni la kiutafiti, miradi hii huanza kutekelezwa kabla ya kufanya utafiti wa kutosha juu ya faida ya uwekezaji husika na hivyo kujikuta hakuna faida ya moja kwa moja kwa uwekezaji husika. Mfano wa miradi hii ni kama ile ya *TBA, NHC, NSSF* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe mchango wangu kwa kuiomba Serikali kuongeza uwajibikaji na umakini katika kusimamia miradi mingi ya Serikali ili kuepuka hoja za ukaguzi zisizo za lazima. Pili Serikali ikayafanyie kazi maoni na ushauri wa Kamati na Bunge Zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naunga mkono maazimio yote yaliyoletwa na Kamati kwa 100%.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa umuhimu wa *NIDA* na vitambulisho kwa wananchi, hivyo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) pamoja na uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ya *CAG* kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) umebaini mapungufu katika maeneo makubwa mawili. Maeneo hayo ni dosari katika utunzaji wa malighafi za kuzalisha Vitambulisho vya Taifa zenye thamani ya shilingi bilioni 42 na eneo la pili ni kutokuwepo kwa mikataba kati ya *NIDA* na watumiaji wa taarifa za *NIDA* hivyo kuikoshesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, katika dosari ya utunzaji wa malighafi ya vifaa vya kutengeneza Vitambulisho vya Taifa, masuala yafuatayo yalibainika:-

(a) Kutokuwepo kwa taarifa sahihi za mahitaji ili kubaini mahitaji halisi ya vifaa vya kutengeneza vitambulisho (*poor management of stock levels*); utunzaji ulikua hafifu ndio maana vitambulisho vilikuwa vinazagaa hivyo ili kupunguza upotevu huu wa malighafi Serikali iweke mkazo katika kutunza pesa za wananchi.



**SPIKA:** Ahsante sana kama nilivyosema sasa tutahamia upande wa Serikali lakini tukumbushane tu kwamba hoja za *CAG* zilikuwa ni kadhaa lakini kamati imeibua hoja kumi na tano na kuzipa ukipekee na Waheshimiwa Wabunge wameongezea na nyingine ziko hoja zinazohusu *TRA* ziko zinazohusu *REA* na utendaji wake wa kazi, ziko zinazohusu bandari na zinazohusu manunuzi, *NIDA*, utunzaji mbaya wa malighafi, *TANESCO* shirika kubwa namba moja katika nchi, *Pride Tanzania*, Maliasili, Benki za Serikali, *PSSSF*, *Mzinga Holding*, *Stamigold*, Bodi za Mazao, masuala ya *liquidity*, *BOT* yenyewe, *Mkulazi Holding* na *TTCL* hizi zimekuwa *highlighted* kipekee. (*Makofi*)

Lakini Waheshimiwa Wabunge wamechangia na maeneo mengine na maeneo mengine Serikali itafanyia kazi kwasababu yamo katika taarifa za *CAG* moja kwa moja japo hazikuibuliwa kipekee kila hoja kwamba ije hapa ndani.

Kwa hiyo Waheshimiwa Mawaziri sasa karibuni sana tuanze na Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafatiwa na Mheshimiwa Angelina Mabula, tujitahidi kutumia dakika kumi *or less* karibuni sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu hoja ya *PAC*. Kwanza uniruhusu nikushukuru sana na nikupongeze sana kwa umakini nimekuwa nikisikiliza mijadala hapa Bungeni kamati mbalimbali inaonyesha umahiri wako wa kuliongoza Bunge kwa kuunda kamati ikizingatia weledi katika kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru pia katika utumishi wangu kwenye kamati nilitumika kwenye Kamati ya *PIC Public Investment Committee* ninao uhakika tuliokuwa nao kwenye kamati tulifanya kazi nzuri kwasababu kamati ilikuwa ni mpya tulitengeneza *base* nzuri ambayo siku hizi nafurahi kuona wakiendelea kutoa taarifa nzuri, kwa hiyo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa vile CAG yuko hapa kipekee nimshukuru nilitumika kwenye ofisi hii kwa miaka 25 nimekagua miaka 15 na miaka 10 nilifanya kazi ya *Finance* nilikuwa kama Mhasibu Mkuu Ofisi ya CAG na ninaamini kabisa sikuangusha ofisi kwasababu niliunda hesabu vizuri, nilifanya kazi vizuri sana lakini leo CAG ukiwa hapa kwa niaba ya Ma-CAG wengine niliofanya nao kazi napenda nitumie nafasi hii nikushukuru wewe pamoja na watumishi wa Ofisi ya CAG. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naona hapa kuna kazi kubwa mnayoifanya nimesoma ripoti nyingi sana nimeona mmetoa hati 1082 sio kazi ndogo lakini bado pia naona taarifa nyingi sana zingine za *performance audit* nimeziona na kuzisoma na zingine zinaendelea kutushauri kama Serikali na ninaamini kazi unayoifanya utaendelea kuifanya Mungu akubariki akupe afya njema wewe na timu yako muweze kufanya kazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nianze na moja la ushauri kwenye taaluma kwasababu nimeona wataaluma hapa wakizungumza katika Bunge wako wengi sana hapa lakini kuna wakati mwingine katika uchangiagi na sisi tunao maadili ya *ki-professional* watu wamekuwa wakitoka kwenye mstari na nikaona labda saa nyingine niseme hapa iko haja ya kuwa na *concuss ya Professional* hapa kwasababu tunahitaji kusaidia nchi tunahitaji tusaidie Bunge kupitia taaluma zetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Kigua mara nyingi akizungumza hapa tumemwona akitoa michango mizuri lakini wapo wengine pia naona kwamba iko haja ya kukaa kama timu ya kuona kwamba tunasaidia Bunge lako kwa vile CAG yupo hapa na wakati fulani tumezungumza pia na Bodi ya *NBA Chief Executive* tuone tunaona umuhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado pia tuna masaa ambayo tunahitaji tuyapate kama *Professional* kwasababu Wabunge hapa wanachambua ripoti naona iko haja tukishirikiana wapate masaa yale ya *CBD* kwa maana ya kwamba wanafanya kazi nzuri yatambuliwe ili wapate masaa

hayo ki-*professional*. Niliona niliseme hivyo wako CPA wengi hapa naona Mheshimiwa Hasunga yupo hapa, Mheshimiwa Kigua, Mheshimiwa Jamali, Mheshimiwa Ruge, Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Mgalu na wengine ambao sio rahusu niwataje lakini wako watu wengi naamini tukijiunda kama timu tunaweza kusaidia Bunge lako. Niliona nitoe kama ushauri tunapokwenda mbele ya safari ipo haja kukaa kama timu moja (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nichangie mawili kwa maana ya upande ule wa TPA kwa maana ya Mamlaka ya Bandari lakini na lile la TTCL. Nimeona Waheshimiwa Wabunge wamechangia lakini nipongeze sana kamati imekuja na maazimio ambayo naona ni maazimio ambayo yameungana na ushauri wa CAG na lakini maazimio ambayo yanaweza kutekelezwa na Serikali. Kwa hiyo, tumekuwa na ripoti hii nzuri na kwa muda mfupi sana wametoa ripoti nzuri kwa kweli nimefurahi sana kuona hivyo kwasababu naona maazimio ambayo yapo kwenye upande wa Mamlaka ya Bandari tunashauriwa kwamba twende kutekeleza manunuzi yetu kwa kuzingatia sheria na sisi kama Wizara Serikali tumejipanga na tumeanza kulishughulikia yale mapungufu ambayo tumeyaona ambayo pia CAG ameshauri lazima tusukume tuone sheria hizi zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo kuona kwamba lazima tuwe na umakini wa hali ya juu kutekeleza kwamba Sheria ya Manunuzi lazima tutekeleze kama Serikali. Pia tuna ushauri kutoka kwenye kamati ufanyike ukaguzi maalum ambao pia nafahamu yako makandokando kidogo yanaendelea kule na hata wakati mwingine mchangiaji mmoja hapa alizungumza juu ya baadhi ya watu ambao wamesimamishwa kazi lakini kwasababu suala hili la kiutumishi lina utaratibu na mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu tu Mheshimiwa Ruge, alizungumza hapa kwamba tunasimamia vizuri kuona kwamba haki za watumishi zinabaki pale pale, lakini yale ambayo yamejitokeza kule ambayo yanaendelea kwa nia

ya kuboresha, kwa nia ya kuona matatizo yaliyojitokeza, lazima tuyafanye kwa uangalifu ili kuona mtumishi anapata haki yake na Serikali pia inayaona na kuyachukulia hatua mambo ambayo tunayaona yana shida.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa *TTCL*, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Amelisukuma suala la *TTCL*. Tunafahamu umiliki wake ulikuwa ni wa ubia lakini Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake na msimamo wake sasa *TTCL* ni chombo ambacho tuko nacho kwenye Serikali kwa asilimia 100. Hii ni hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, hata saa nyingine niseme yale yaliyojitokeza kwenye Bodi nilitaka niyaseme kidogo, niruhusu niyaseme; yaliyojitokeza ni kwa sababu pia ya mabadiliko ya umiliki wa lile shirika. Kwa sababu ukiangalia ripoti za fedha zinvyo-*flow*, hizi zina-*include* na ripoti za nyuma wakati umiliki ule ulikuwa kwenye ubia.

Mheshimiwa Spika, sasa Mwenyekiti wa Bodi aliyemteua Mheshimiwa Rais ni mtu mahiri sana kwa sababu alimteua mtu aliyekuwa *Internal Auditor General*, akawa Mwenyekiti wa Bodi. Sasa wakati taarifa inakuja kwenye mikono ya Bodi, nayo Bodi inalo jukumu lake kama Bodi, waliona yako mambo ambayo kwenye *opinion* niseme kwamba *opinion* inavyotolewa *CAG* yupo hapa anaweza akaona kama nitakuwa nakosea lakini nina uhakika na ninachozungumza.

Mheshimiwa Spika, tunapata *certificate* ambayo ni *unqualified*. Hii *unqualified* kwa namna nyingine tunaweza tukasema *unmodified*; hii ndiyo *clean certificate*. Ikitoka ile unajua kwamba *CAG* au mkaguzi anavyopita kwenye hesabu anaona hesabu zimekaa sawasawa, ripoti zake na *information* ziko vizuri. Sasa hii ni *unmodified*.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye ile *qualified opinion*, ina maeneo mawili; ina *adverse* ambayo sasa hapa ina mambo ambayo ni *specific* ambayo mkaguzi anayaonesha kwamba *except for this one*. Anavyokuwa

ameyataja, ninaamini Bodi kwa wakati ule waliamini labda wangeenda kwa muda wangeweza kuya-clear haya mambo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kati ya mambo hayo, kulikuwa na taarifa ya makusanyo ambayo ilikuwa inahitaji *reconciliation*, ilikuwa na shilingi bilioni 1.7, lakini kwa maelekezo ya Bodi ile walifikiri kama wangewahi tungeweza ku-clear. Mpaka ninapozungumza *unreconciled item* kwenye makusanyo ni shilingi milioni sasa 81.7 kutoka kwenye shilingi bilioni 1.7. Uone kwamba Bodi ilikuwa inafikiria kwamba ingeyatoa haya ambayo ni *except for* kwa mujibu wa ripoti labda tungewahi muda wa kusaini CAG, saa nyingine tungeona kwamba hata hiyo *opinion* ingeweza kubadilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, pia kulikuwa na suala la madeni ambayo tunadaiwa na madeni ambayo tunadai. Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa kwamba tunadaiwa shilingi bilioni 11 na tunadai shilingi bilioni 91, lakini ukiangalia haya madeni, yameenda ku-include kipindi kile ambacho taasisi yetu ilikuwa iko kwenye ubia ambapo kimsingi ilihitaji kuchanganua ili tuweze kwenda na saa nyingine tupate *opinion* tukizingatia kwamba shirika letu ni la kibiashara, pia *opinion* ina umuhimu sana kwenye biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo haya nafikiri baada ya kutokea kwamba Mwenyekiti wa Bodi alipewa majukumu mengine, tukaingia kwenye shida hii iliyotokea. Nilitaka niliseme hilo na kwamba kwenye *governance* nashukuru Bunge lako linakwenda vizuri kwenye utawala bora. Nashukuru pia kwenye taasisi znyngine tunazo *management* zinafanya kazi yake vizuri, tunazo Bodi zetu zinafanya kazi vizuri, tuna *Audit Committees* zinafanya kazi vizuri, kuna *Internal Auditors* wanafanya kazi vizuri lakini na *External Auditors* kwa maana ya CAG.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie tu CAG, yuko hapa, sisi kama Serikali tunapenda kufanya kazi kwa uhuru

na CAG afanye kazi kwa uhuru, lakini tuunganishwe na mawasiliano mazuri, mahusiano mazuri na ushirikiano mzuri. Ndiyo hiki nataka kusema kwamba tunaendelea kumpa ushirikiano CAG ili sasa tuone kwamba hata mashirika yetu, hesabu zetu zinakwenda ku-*depict the true picture* ya mashirika yetu.

Mheshimiwa Spika, hili lililotokea naliombea radhi, nasi kama Serikali, Wizara yangu, Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo, yale ambayo yanahitaji kuyarekebisha yakae vizuri na hesabu zetu zikae vizuri, tutaendelea kuyawasilisha kwa CAG kwa ajili ya kufanya *verification*. Ninataka nimuahidi tu CAG, niahidi PAC na Bunge lako kwamba tutaendelea kutoa ushirikiano mzuri kwa nia hiyo ya kuona kwamba kile kinachotokea kwenye mashirika yetu kinakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilitaka niyaseme tu hayo kwa sababu nimeyaona lakini niseme kwamba taarifa za CAG ninazisoma sana na ninayo taarifa hapa ya CAG aliyotoa kwenye vyombo vya habari, yako mambo mengi mbali na haya ambayo yapo kwenye Ripoti ya PAC, yako mengi ambayo kiutendaji tunahitaji tuyasukume na kuyasimamia.

Mheshimiwa Spika, niseme tu ninamuahidi CAG na Bunge lako, hata yale ambayo hayakuingia kwenye Taarifa ya PAC, sisi kama Serikali tutaendelea kuyashughulikia tuone kwamba yanakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hapa. Niendeleo kusema tu, nitaendelea kuona namna nzuri tuunganishe *professionals* hawa, kwa sababu ninasikia uchungu ninayovyoona mtaaluma na tumekula viapo vya kuzungumza vitu ambavyo vina mantiki kama CPAs, sasa siyo vyema sana wakija hapa wengine wanakuwa na msingi kama wa kupotosha huku wakiwa wamekula viapo, siyo vyema sana. Nisingependa kuwataja lakini ninaona tukiwa na *caucus* yetu tutaweza kufanya marekebisho makubwa na kulisaidia Bunge lako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Elias Kwandikwa. Tunakushukuru umewaombea radhi hawa *TTCL*, lakini ni vizuri hiyo Bodi wakaandika kwa *CAG* na ikiwezekana hata sisi tukapata *copy* kwa sababu tabia wanayoionyesha ya kugomea masuala yanayohusu utaratibu ni tabia ambayo ikisambaa ni *deleterious*.

Pia huku bandarini nako kama walivyosema Kamati, tunaendelea kusisitiza. Kamati imekuwa ikilalamika kwa muda mrefu sana kuhusu bandarini, kwamba kuna mikataba ya ovyo, kuna watu wanafanya mambo wanavyotaka. Ni pa kupaangalia kwa kweli ninyi kama Wizara mkatazama; unakuta *professional* bandarini anahamishiwa Kongwa; natoa mfano usiokuwa halisi lakini halisi; ambako hata bandari hakuna.

Sasa wewe mtumishi wa bandari unamhamishia Kongwa, maana yake nini? Tena watumishi ambao kama ulivyosema wewe mwenyewe, *professional*/kwa maana hiyo.

Kwa hiyo, *professionalism* vilevile, pamoja na kwamba hapa Bungeni umetushauri vizuri sana na huko Wizarani vilevile nako mlinde hizi *professions*. Kama mtu hana kosa alilolifanya, anaonewa tu ovyo kwa sababu ya *professionalism* yake, ni wajibu wenu kama viongozi wa Wizara kuliangalia hili. (*Makofi*)

Idara zote zinakuwa na watu wanaokaimu, karibu zote huko bandarini; *What is that?* Huyo ndiyo ng'ombe mkubwa tunayemtegemea kiuchumi,. Mliangalie hilo. Hizi hamisha hamisha za ovyo ovyo, za kupanga safu, nazo wamekuwa wakilalamikia sana Kamati. Tuangalie maeneo hayo. (*Makofi*)

Nilisema anayefuata ni Mheshimiwa Angeline Mabula na atafuatiwa na Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata kuwa mmoja wa wachangiaji katika hoja iliyoko Mezani. Pia nikupongeze wewe na timu yako kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo analiongoza Taifa hili katika hatua ambazo tunakwenda na Taifa linapata heshima zake kama Taifa. Nami nitoe pongezi kwa CAG kwa kazi kubwa aliyofanya. Sisi kama Serikali tumepokea ushauri na mapendekezo yake pamoja na Kamati ambayo wametoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninalo moja ambalo ninataka kulitolea ufafanuzi; Mheshimiwa Halima kabla hatujaenda kwenye mapumziko ya Sikukuu ya Iddi alitoa hoja moja ambayo inahusiana na suala la Shirika letu la Nyumba la Taifa kutokana na miradi yake mikubwa ya kimkakati ambayo ilikuwa inajengwa na pengine inakwenda kwa kusuasua kama ambavyo alisema; na akawa na wasiwasi kwamba ile miradi miwili iliyoko Kawe pengine inaweza isitekelezwe kama ambavyo walikuwa wanatarajia.

Mheshimiwa Spika, napenda tu nilihakikishie Bunge lako kwamba Shirika letu la Nyumba la Taifa sasa linao uwezo mzuri wa kuweza kufanya kazi kwa kutumia pia nguvu za ndani. Hiyo miradi mikubwa anayoisema, alitaja ile miwili; *Seven Eleven* ile ya kule Kawe na *Golden Premier Residences* ambayo yote iko Kawe, lakini tunayo *Morocco Square* pamoja na ile ya *Plot 300* ya *Regent Estate*. Miradi hii iko katika *stages* mbalimbali katika ukamilishaji wake. *Morocco Square* iko asilimia 90; *Seven Eleven* iko 35 na *Golden Premier* iko 43, na ile *Plot 300* iko asilimia 11.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kwamba kulikuwa na kusuasua kwa miradi ile, uongozi wa Shirika uliteua tume au timu ya wataalam mbalimbali kutoka sekta mbalimbali ambao walipewa kazi ya kupitia miradi ile yote na walipitia kwa undani kuanzia kwenye mikataba yake lakini



pia na kuangalia namna ambavyo fedha zilizokuwa zimetolewa kwa ajili ya miradi hiyo zimetumika na kuona pia kama kazi iliyofanyika inakwenda sambamba na pesa iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, pia walikwenda mbali zaidi na kuangalia namna sasa ya kuweza kukamilisha miradi ile kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa. Tume hii iliundwa Januari, 2019 na ilimaliza kazi yake mwezi Aprili, 2019 na walitoa taarifa yao. Moja ya hadidu za rejea walizokuwa wamepewa ilikuwa ni kufanya pia uchambuzi wa mikataba yote ambayo ilikuwa inasimamiwa katika ujenzi, lakini kupitia pia na michoro mbalimbali ambayo ilikuwepo na pia kuona kama ile miradi pengine ilikuwa na tija kulingana na hali halisi ilivyokuwa. Mapendekezo yote waliyoyatoa waliyawasilisha kwenye Bodi na Bodi iliyapitia yale mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua yale mapendekezo Bodi ilikubaliana na mapendekezo ya ile Kamati na ikaja na mkakati sasa wa kuweza kukamilisha miradi ile kwa kutumia pesa za ndani ya shirika. Sasa hivi kama mnavyofahamu shirika lenyewe linafanya kazi kubwa sana ya miradi mkubwa ya Serikali ambayo imeaminiwa na miradi yote ile inaingiza pesa ndani ya shirika.

Mheshimiwa Spika, pia kuna nyumba ambazo tayari zilikuwa zimeshauzwa, kuna wengine walikuwa wanalipa kidogo kidogo. Kwa hiyo, shirika linaongeza nguvu katika kukusanya yale madeni na pia katika kuhakikisha kwamba pesa zinazolingia zote katika miradi sasa zinatumika katika kukamilisha ile miradi. Ile miradi miwili itaendelea na wakandarasi, kwa maana ya ule mradi wa *Morocco Square* na ule wa *Seven Eleven* na ile mingine miwili itajengwa na kampuni tanzu ya ndani ya shirika.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hayo yote pia ilifanya mapitio ya ile mikopo yote ambayo ilikuwa imetolewa kwa maana ya kufanya *loan restructuring* ili kuwa na muda mrefu zaidi wa kuweza ku-*service* ile mikopo. Pamoja na

kusimama shirika halikuwahi kukwama kulipa ile mikopo, ilikuwa ikilipa yote ili kuweza kuepuka riba.

Mheshimiwa Spika, vilevile waliweza kufanya *loan restructuring*, sasa wameongezewa muda na katika kufanya hivyo, kumekuwa na *saving* ya kila mwezi ya shilingi 1,102,612,000/= ambazo zinapatikana baada ya kuwa wamefanya *loan restructuring*. Kwa hiyo, katika utaratibu huo tuna uhakika kwamba kazi itakwenda kufanyika vizuri na miradi ile itakwenda kutekelezwa kama ambavyo tumekusudia, japokuwa sasa itachelewa kulingana na mikataba ile ya mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii yote haijalitia hasara shirika kwa maana ya kwamba imesimama kwa muda mrefu halafu imechelewa pengine tulikuwa na hofu tungeweza kupata labda riba kubwa katika mabanki, lakini kutokana na hicho kilichofanyika, madeni yanalipwa vizuri na muda umeongezwa na kasi itakwenda. Kwa hiyo, wataanza katika kukamilisha lile jengo la *Morocco Square* ambalo liko asilimia 90. Tuna imani likikamilika lile litakuwa tayari linaingiza pesa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, *Victoria Palace* tayari lilishajaa na watu walishanunua na pesa ile pia imeweza kufuatilia kwa wale ambao walikuwa bado hawajakamilisha, ndiyo wanazidi kufuatiliwa ili waweze kuamilisha. Kwa hiyo, mapato ya shirika bado yako mazuri hayajayumba na wameweza kufanya kazi ile ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, hasa wa Kamati husika kwamba Serikali tunajali sana na tunahakikisha shirika hili halianguki na linafanya kazi yake kwa tija kama ambavyo limeundwa kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, tunapenda kuwahakikishia usimamizi wa sasa unaendelea vizuri na kasi ya ufuatiliaji wa miradi unafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tuko katika utaratibu mzuri ambao baada ya muda siyo mrefu utaona

*changes* kubwa zinaendelea kwa sababu tayari ule usimamizi ulioko uko vizuri. Na mimi nawashukuu sana Kamati kwa sababu walilionna hili na wamekuwa wakipigia kelele pia hata siku za nyuma wakiwa na wasiwasi kwamba pengine shirika lingeweza kukwama.

Naomba niwathibitishie, pengine sasa shirika linakwenda kuwa imara zaidi kuliko vile tulivyokuwa tunafikiria. Lilianza, likasuasua, likapanda, halafu likashuka, sasa hivi liko kwenye chati ambayo ni nzuri. Nami niwatoe hofu kwamba miradi inakwenda kukamilika na tutakwenda kufanya kile ambacho kimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie hayo tu kulingana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Halima akiwa na hofu ya miradi. Hata hivyo, katika pesa nyingine ambazo tunatarajia ni kutokana pia na mauzo ya hati fungani, shilingi bilioni 30 kwa miaka mitano, nayo itakwenda kuleta pesa nzuri ambayo itakwenda kusaidia pia katika kuendesha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Angeline Mabula. Ni kweli na tunakushukuru sana kwa maneno ya kututia moyo kuhusiana na Shirika letu la *National Housing* kwa sababu wasiwasi ulishakuwa kwa watu wengi kwa kweli kwamba vipi tena? Maana barabara zile kila mtu akipita pale akitazama majibu unayapata mwenyewe, huna haja ya kuongea. Hata hivyo, umetutia moyo kwamba sasa wamejipanga na wanakwenda kuwa watu wapya zaidi, basi muwasaidie wawe hivyo.

Hapa Dodoma watengeneze *Tower* hata moja kama zile. Habari ya kutuletea vyumba viwili na sebule Dodoma, hatutaki sisi, hizo tunajenga wenyewe. Waje wafanye kitu zaidi ya *PPF* ili tuone kweli hawa *National Housing* wamefufuka, lakini mkijenga hivi vidogo vidogo vya chumba na sebule hatuwezi kujua kama *National Housing* ipo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wafanye kitu ambacho anayekuja Dodoma anaona kwa macho kwamba hii ndiyo *National Housing Corporation* mpya. Hizi nyumba za chumba na sebule tunaweza wenyewe wa Dodoma hapa hapa.

Mheshimiwa Naibu Waziri Nyongo, karibu sana. Atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa umahiri wa kuendesha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue fursa hii kwa makusudi kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa umahiri wake wa usimamizi wa Sekta hii ya Madini na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kupitia Sekta hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukutaarifu wewe na Bunge lako na Watanzania wote kwa ujumla kwamba leo tarehe 26, mwezi huu wa Tano muda wa mchana tumepokea hundi ya fedha kutoka Kampuni iliyokuwa inaitwa *Barrick* sasa hivi tunaita Twiga; hundi ya malipo ya fedha kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 100 ikiwa ni sehemu ya makubaliano tuliyokubaliana nao kupitia Kamati ya Maridhiano iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Prof. Kabudi, kiasi cha dola milioni 300 ambazo tulikuwa tumekubaliana na leo wamelipa dola milioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yale yaliyokuwa yakisemwa kwamba kishika uchumba hakilipwi, ni kanyaboya, ni maneno matupu, leo fedha hizo zimelipwa na tunavyozungumza, fedha hizo zimeshaingia Hazina na ziko tayari sasa kwa ajili ya kupeleka maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa pika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa umahiri wake...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilitarajia habari hii angalau ingepigiwa makofi Waheshimiwa, eeh!

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Tutumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuzuia yale makinikia. Matunda tumeanza kuyaona baada ya makubaliano, sasa wameanza kulipa na hii kwa kweli ni fursa na ni faraja kubwa kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kupokea fedha hizo na Mheshimiwa Dkt. Mpango yuko tayari kabisa sasa kuanza kuzitumia zile fedha kwa ajili ya kupeleka maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unajua Mheshimiwa Nyongo ukisema milioni 100 kidogo Watanzania hawapati picha hasa, yaani ni kama ngapi hivi?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, dola milioni 100 kwa kiwango cha kubadilisha fedha cha leo kwa mujibu wa *BOT* ni sawasawa na bilioni 250. *(Makofi/Vigelele)*

**SPIKA:** Hapo nakushukuru sana, maana yake angalau Wanyamwezi sasa wameelewa ni shilingi ngapi. *(Kecheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Fedha hizo baada ya muda siyo mrefu, zile dola milioni 200 zinazokuja ni sawasawa na shilingi bilioni 500. Kwa hiyo, baada ya kulipwa fedha hizi zote tutakuwa tumepata shilingi bilioni 750 kwa maana ya malipo kamili ya kishika uchumba ambacho kilikuwa tayari kutolewa na Kampuni ya Barrick. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote, Wabunge wote tulioko humu sifa hizi tumpelekee Mheshimiwa Rais wetu kwa umahiri wake wa kuamua kustopisha yale makinikia na leo wameanza kulipa na tunakwenda mbele na sisi kama Wizara ya Madini baada ya maridhiano kupitia Kamati ya Maridhiano, tuko tayari kushirikiana na Kampuni hii

kuhakikisha kwamba tunakwenda kuchimba madini yetu na madini haya yanakuwa na mchango mkubwa na kuleta toja kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendeleo kukushukuru wewe, lakini vilevile niishukuru kamati yako.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *STAMIGOLD* imezungumziwa katika hoja za *CAG* na kampuni hii ya *STAMIGOLD* ni kampuni tanzu ya Kampuni ambayo ni ya *STAMICO* kwa maana ya kwamba, ni kampuni au shirika la Taifa ya Madini.

Mheshimiwa Spika, *STAMIGOLD* tuliikuta ikiwa katika hali mbaya sana, tuliikuta ina madeni makubwa, ilikuwa na madeni zaidi ya bilioni 64. Leo tumeanza kupunguza madeni hayo, lakini tumeyapunguza kwanza kwa kuhakikisha kwanza tunahakiki madeni hayo, kuangalia madeni hayo kama kweli yalikuwa ni kweli, kwasababu tulikuta kuna hali ya wizi wa kupindukia. Tulichukua hatua na hatua mojawapo tuliweza kukaribisha wenzetu wa *PCCB* kutusaidia katika kazi hii, na waliweza kufuatilia na kuhakiki na kuweza kuyafuta madeni yale yote ambayo tuliyaona yalikuwa na madeni ya ukakasi na ya kubambika.

Mheshimiwa Spika, wakati *CAG* anafanya ukaguzi nikubaliane kwamba, kuna hoja nyingine nakubaliana nazo kwamba *CAG* alipofika pale alikuta kwamba, kuna baadhi ya madeni ambayo *STAMIGOLD* ilikuwa inadaiwa na madeni hayo yalikuwa na *documents* zake, lakini *documents* hizo nyingi zilikuwa kwa *PCCB* kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi. Na madeni hayo waliona kwamba hawayaoni katika zile *documents*, na kwa kweli ni halali kuripoti kuonesha kwamba, kuna madeni makubwa, lakini sababu ni kwamba baadhi ya *documents* zilikuwa ziko upande wa *PCCB* wakizifanyia kazi. Kwa hiyo, kuna baadhi ya madeni kweli, hayakuonekana na hilo tunakubaliana, lakini katika majibu yetu ya msingi kwa maana ya kupeleka katika zile *technical team* tumeyajibu vizuri na kuanzia hapo tuinaweza tukaenda vizuri kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile *STAMIGOLD* hii ni kampuni ya kufanya biashara, inafanya biashara kama kampuni nyingine zinazvyofanya biashara. Wakati mwingine tunakubaliana sheria ya manunuzi (*PPRA*) kuna wakati mwingine inakuwa inachelewa na wakati mwingine kampuni hii inavyofanya kazi kibiashara kuna maamuzi mengine wakati mwingine inabidi tuyachukue kwa haraka ili tuweze kuendana na jhali ya kibiashara ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kulikuwa kuna bwawa la maji machafu lilikuwa limejaa na maji yanataka kutiririka kwenda kwenye maeneo ya wananchi na ni maji yenye sumu. Tunge sema tusubiri utaratibu wa manunuzi moja kwa moja tungeweza kuchelewa...

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** ...na baada ya kuchlewa ina maana maji haya ingebidi mradi huu usimame. Kwa hiyo, kuna baadhi ya hoja za *CAG* amehoji...

**SPIKA:** Unatoa Taarifa, Mwongozo?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Basi, subiri inapokuwa hakuna anayeongea halafu utatoa Mwongozo wako; endelea tu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwahiyo hizi taratibu za manunuzi wakati mwingine kibiashara kwa mtu anayefanya biashara kwa mfano sisi Kampuni ya *STAMIGOLD* inachelewesha maamuzi, na sisi tunataka kwenda kiushindani na tunataka kufanya kazi kibiashara. Kwahiyo kuna wakati mwingine tunachukua maamuzi ya haraka ili kluhakikisha kwamba, mradi huu unafanya kazi kwa faida. Hauwezi ukakubali maji yatiririke tukisubiri taratibu wakati tunahitaji kufanya maamuzi ya haraka kuzuia sumu

isitiririke kwa Wananchi. Kwahiyo haya ni mambo ambayo inabidi tukae na CAG na kuweza kueleweshana na kuweza kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge imehoji vitu viwili vikubwa au vitatu kwamba, madeni yaliyopo hayana *justification* ya nyaraka.

Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza nyaraka nyingi zilikuwa upande wa PCCB. Lakini vilevile kamati imeeleza rasilimali ilizonazo STAMIGOLD na madeni waliyonayo. Madeni tuna bilioni 52, rasilimali tulizonazo ni bilioni 39. Kwa haraka haraka ni kwamba, STAMIGOLD haiwezi kulipa madeni inayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini rasilimali za kwenye migodi sio *processing plant*, sio magari, sio mitambo, sio *crushing machines*. Rasilimali kubwa kwenye migodi ni *reserve* tuliyonayo chini. Tuna *reserve* kubwa ya dhahabu katika Mgodini wa STAMIGOLD.

Katika *hard rocks* tu tuna wakia zaidi ya 71,300. Kwenye visusu kwa maana ya *tailings*, zile *process* ilikuwa ikifanyika mwanzoni zile *tailings* tumezipima kupitia maabar ambazo ziko *accredited* kimataifa. Tuna wakia zaidi ya laki mbili ziko pale ambazo tunakwenda kuzi-*process* ambazo zina thamani ya zaidi ya dola za kimarekani milioni 360. Kwahiyo ukiangalia Ripoti ya CAG ni kweli itaonesha kwamba, *processing plants* zetu ni ndogo, unakuta *processing plant* ina gharama ndogo, lakini *reserve* iliyopo chini ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo tungeweza kuzungumza kwamba, kama CAG ana wataalam wa kuweza kuangalia *reserve* tuliyonayo tuna *reserve* kubwa na rasilimali tuliyonayo kubwa ambayo ni *untaped*, ni kubwa kuliko madeni tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa haraka haraka ni kwamba, STAMIGOLD ina uwezo wa kulipa madeni tuliyonayo.



**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo asante sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Asante sana kwa kutupa matumaini kuhusu *STAMIGOLD*, lakini pia kwa taarifa nzuri ya Ndugu zetu hawa Twiga kuanza kuilipa Serikali fedha hizi ambazo zitatusaidia sana katika maendeleo ya nchi yetu. *Engineer Stella Manyanya*.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, niliomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Eeh, palikuwa na Mwongozo, ndio Mheshimiwa.

#### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa namsikiliza Naibu Waziri wa madini amesema kwamba, kilichosababisha kukosekana kwa taarifa kumpatia *CAG* ni *documents*, kwamba zilikuwa *PCCB*:-

Mheshimiwa Spika, Bunge lako linaangaliwa *live*. Hivi Wizara, na ndiyo maana *CAG* amekataa hizo hoja zao, kwamba inakuwaje kwamba, *documents* ulizokuwanazo wewe ndio hizo tu umpe *PCCB* halafu wewe huna *records*; ni jambo ambalo halikubaliki katika masuala ya kiutendaji.

Kwa hiyo naomba asirudie, asiendelee kulidanganya Bunge kwa sababu, *CAG* alishakataa hizo hoja zao kwamba, *document* ziko *PCCB* kwa sababu wao kama taasisi wanao uwezo wa kuwa na *copy* ya hizo *document* na ukampa *CAG* akafanya kazi zake. Kwahiyo asilidanganye Bunge kwa sababu, Bunge liko *live*. Hapa tunachozungumzia ni maslahi ya nchi hii ili fedha za umma zitumike vizuri. Ahsante.

**SPIKA:** Basi sijui, Mheshimiwa Naibu Waziri unataka useme chochote hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge. Ni kwamba, CAG anapohitaji *documents* nadhani kila mtu anaelewa hapa, anahitaji *documents original* ambazo zinaonesha *validity* ya ile taarifa. Sasa kama *documents* ziko kwa PCCB, nadhani ni suala la *coordination* tu, kwamba *documents* zitoke PCCB zije kwa CAG aweze ku-*verify* na aone kama deni lipo, basi utaratibu unaweza kwenda. *Copy* sidhani kama zinaweza kukubalika kwa ajili ya kazi hiyo ya ukaguzi, ahsante sana.

**SPIKA:** Asante sana. *Engineer* Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini pia, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uhai. Niwashukuru pia Kamati ya PAC chini ya Mwenyekiti wao kwa taarifa hii ambayo wameileta. Mimi naamini kwamba lengo la kamati pamoja na Serikali linafanana ni kuhakikisha kuwa fedha zote zinazopatikana na zinazotengwa kwa ajili ya kazi fulani zinatakiwa zitumike vizuri kwa manufaa ya Taifa letu. Pia nampongeza CAG kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na hivyo kutuwezesha sisi kuona maeneo ambayo tumefanya vizuri na maeneo ambayo yana mapungufu yaweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, nikianza na sual la mshauri, *SME International PTY Limited*, ambayo ilipewa kazi ya kufanya tathmini ya mwanzo au usanifu wa mwanzo pamoja na ubunifu kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika vijiji 7,834:-

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kabisa kwamba lengo la Serikali hii toka ilipoingia madarakani ilikuwa ni kuhakikisha inaendeleza kazi ya kusambaza umeme kwa haraka sana katika vijiji vilivyosalia na hiyo, pia ilikuwemo katika ilani ya uchaguzi. Kwahiyo tarehe 20/10/2016 Serikali kupitia REA iliingia makubaliano na mshauri huyu ili aweze kufanya kazi hiyo ya kupata makadirio ya awali ya namna

ambavyo itaweza kusambaza umeme katika hivyo vijiji 7,834. Na hiyo ni utaratibu wa kawaida; kwamba unapotaka kusambaza umeme si kwamba utaanza na *actual design*, unaanza na ule utaratibu wa kupata makadirio ya awali ili sasa hata utakapoweza kutangaza tenda watu waweze kuomba kulingana na yale makadirio yaliyopo. Yaani lazima awe na kitu ambacho kinamuonesha anaenda wapi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika makadirio hayo kimsingi ni kwamba, katika ile taarifa ya awali fedha iliyoonekana itahitajika kutumika kwa vijiji hivyo, ilikuwa ni nyingi kuliko ule uwezo uliokuwepo kwa wakati huo. Kwahiyo Serikali kwa uharaka uliokuwepo hawakungojea tena mpaka ipate ile ripoti kamili kwa sababu, tayari ilishapata picha. Iliwatumia makandarasi sasa kwenda katika yale maeno ambayo iliona ianzenayo kulingana na mahitaji ya haraka yaliyopo (*priority*). Makandarasi 29 walipewa hiyo kazi ya kufanya usanifu wa kina wa kuweza kupeleka umeme.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, pale unapofanya makadirio yale ya awali au *design* ya mwanzo huwezi kujua kwamba lazima hapo unapopita kutakuwa labda kuna bonde au kuna mlima au kuna kitu gani; yaani inategemeana; kwasababu mtu anaweza hata akafanya *design* kwa kutumia hata *GPS Coordinates* akapata picha, lakini huwezi kujenga kabla hujapata hali halisi ya eneo unalopeleka huo umeme kwa sababu, kuna sehemu nyingine unaweza kukuta kuna kona ile kona peke yake itakupa gharama kubwa zaidi kwa sababu, utahitaji nguzo, utahitaji *stay* au *gryphone*, na vitu vingi ambavyo vinahitajika kwa ajili kuiwezesha ile kona uweze kupitanayo.

Mheshimiwa Spika, au unaweza kukuta kuna mto mkubwa labda pengine una na matope ambayo hata nguzo na *design* utakazoweka zitakuwa ni tofauti; kwahiyo hicho ndicho kilichokuwa kimefanyika. Kwahiyo, makandarasi walipokuwa wanaomba zile tenda walitumia ileile ripoti ambayo huyu mshauri mwelekezi alikuwa ameifanya. Na pamoja na hiyo ni kwamba huyu mshauri elekezi alilipwa fedha za awali takribani shilingi milioni 433 na sio zote ambazo

zilitoka kadiri ya gharama yake ambayo ni ya shilingi takribani bilioni 1.083.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, hata hivyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Frank Taarifa ya nini?

### T A A R I F A

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya *CAG* kwenye upande wa *REA* kwa matumizi ya bilioni 1.5 hatulalamiki kwa nini Serikali iliamua kuwaweka wakandarasi 29. Hoja yake ni kwamba, kwa nini fedha ililipwa ilhali taarifa haijatoka na kazi zikaendelea kwa wakandarasi ilhali bado, yani alilipwa fedha kabla taarifa haijatoka, halafu bado wakandarasi wakaendelea na kazi kabla *consultant* bado hajakabidhi hiyo taarifa, hiyo ndio hoja ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka mzungumzaji atuambie ni kwa nini *REA* waliamua kutoa hizo fedha kabla shughuli ambayo walikuwa wameshalipa fedha 1.5 haijakamlika? Asante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Taarifa hiyo unaipokea?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; niseme tu kwamba, sio taarifa kuipokea isipokuwa niendeleo kumpa ufafanuzi labda alikuwa hajanielewa:-

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba, taarifa yake siipokei kwasababu hakunisikiliza. Ninachosema ni kwamba, ile taarifa ya awali iliyotolewa sisi tuna kiu ya kuhakikisha tunapeleka umeme mapema iwezekanavyo. Taarifa ya huyu mkandarasi ya awali tumepata, lakini ile ya

mwisho imechelewa, lakini wakati huohuo tumeshapata picha na tunafahamu kwamba, tuna uwezo wa kuwatumia makandarasi waweze kufanya hiyo *survey* ambayo ni *actual* na tuweze kufanya kazi; ulitaka tusebiri huyo mpaka lini wakati sii tuna ahadi kwa Wananchi ya kupeleka umeme mapema? (*Makofi*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, wajibu wetu sisi ni kuhakikisha kwamba, umeme unawafikia Wananchi kwa wakati, kwa kadiri ya ratiba tuliyoitaka. Na hilo pengine ninyi mlifikiria kwamba, sisi tutashindwa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** ...sisi tumehakikisha kwamba, kwa kutumia hawa makandarasi tumefanya *actual design* na Wananchi wanaendelea kufaidika na umeme sasahivi. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, hiyo ndio hali halisi na kwa sababu, TAKUKURU bado wanafanyia kazi hiyo taarifa, basi tutaendelea kusubiri...

**SPIKA:** Taarifa ya mwisho, hiyo, iwe ya mwisho, Mheshimiwa Esther; Sekunde tu Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Stella, *Engineer* Stella sekunde tu, Taarifa ya mwisho sasa hii.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, asiseme sisi, sisi tuko hapa tunachambua Taarifa ya CAG; CAG ameweka *query* kwamba, kuna fedha ilitoka *1.1 billion*, kwa ajili ya kumpa mkandarasi kutoa utaalumu. Sasa wameshalipa tena yote, hapa anaelezea kwamba wamefanya nusu wakaamua ku-*proceed*; wamelipa hela yote, lakini *fun enough* walikuwa wanasubiri huo ushauri

kutoka kwa mtaalam huyo mkandarasi, *consultant*, ili waweze ku-*asign* sasa, wa-*base* kwenye ile ripoti waweze kutafuta makandarasi hao 29 waende *field*; lakini CAG aka-*pose* kwamba, kabla hawajapata hiyo ripoti wakawa tena wamewa-*assign* wale wakandarasi, sasa *why*?

Mheshimiwa Spika, ndio maana tunataka *forensic audit* kwa nini walitoa zile *1.1 billion* tujibu hapa. Atujibu hapa, ni kwa nini walilipa hizo fedha halafu hawakuweza kupata ripoti yenyewe ambayo wamemlipa? Yaani *you are paying me, you are paying for nothing*, sija-*produce* hiyo ripoti ambayo umenilipa halafu unaendelea. Kwahiyo inaonesha kwamba, *there was no need* ya mimi kutoa huo ushauri wa kitaalamu; atujibu asikimbie-kimbie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella, ukishavuka hilo kuna la *TANESCO* na muda naona unakwenda, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni sawa. Mfano mwepesi ninaoweza kumuambia Mheshimiwa Mbunge aliyekaa ni kwamba, ni sawa na tulivyoshauriwa tufanye *lockdown*, mwenye maamuzi ya kufanya *lockdown* na kutokufanya *lockdown* ni wewe unayeshariwa. Yule ambaye alikuwa anatushauri sisi amechelewa kutupa ushauri, tunao uwezo wa kutumia njia ya haraka ili kufika pale tunapotaka kufika kwasababu sisi ndio tulio na kazi.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu fedha, kwa taarifa ambayo mimi najua ni kwamba, fedha ambazo zimelipwa ni aslimia 40 mpaka sasa, ila mkataba walisaini ulikuwa wa shilingi bilioni 1.083 na kuendelea. Kwahiyo, kwa misingi hiyo ninachotaka kukueleza ni nini, sio tu suala la kung'ang'ania, lakini kimsingi taarifa iko kwa TAKUKURU inafanyiwa kazi, tutapata matokeo.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu madeni ya *TANESCO*; katika madeni ya *TANESCO* ninachotaka kusema tu ni kwamba, tunaendelea kuwashauri na kuwaomba wale ambao ni wateja wa *TANESCO* kuweza kulipa hizo bili kwa

wakati. Hata hivyo mpaka sasa *TANESCO* imejitahidi sana kukusanya madeni yake; na madeni yanayodaiwa si yale *current* ni yale ambayo yalikuwa ni malimbikizo ya nyuma wakati taasisi zilipokuwa zinapitia changamoto kubwa na hasa taasisi zile za huduma.

Mheshimiwa Spika, huwezi kukata umeme kwa taasisi kama Muhimbili. Huwezi kukata umeme kwa taasisi kama ya maji hata kama ina hali ngumu ya kifedha, lakini kuna makubaliano tayari ambayo yameshaingiwa ambayo wanalipa kupitia bili zao katika yale madeni ya nyuma. Kwahiyo niendeleo tu kuwasisitiza kwamba, hizo taasisi ambazo zinadaiwa ziendeleo kuheshimu makubaliano yaliyoingiwa na *TANESCO* ili kuweza kulipa madeni hayo kwa wakati kama ambavyo imekubalika.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Wizara ya nishati imefanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha nchi hii inapata umeme kwa wakati na inatoa huduma bora kwa wananchi wa Tanzania. Sasahivi umeme unaenda mpaka vitongojinini huko unaenda!. Jamani mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Spika, na tunakushukuru kwa jinsi ambavyo umekuwa ukisisitiza kuhakikisha kwamba Wizara hii inapewa bajeti ya kutosha na kuweza kuwafikishia umeme Wananchi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya nasema ahsante sana; na niseme tu kwamba Ripoti ya *PAC* katika maeneo ambayo ni ya kuimarisha tutayafanyia kazi, asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hili la *REA* lina shida mkalifanyie kazi vizuri, sijalielewa vizuri, lakini hoja yake inaonekana ni kama vile wale ma-*consultants* walilipwa kabla ya kumaliza kazi, yaani iko hapo. Kwa nini umlipe mtu ilhali kazi hjamaliza, iko hapo tu nafikiri, lakini wangeendelea na kazi ya kuweka makandarasi na kusonga mbele ili ku-*catch up it is okey*, lakini

sasa hajakuletea *you pay*, iko hapo tu, lakini watajibu hawa waliolipa hawa watajibu tu wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kujibu hoja hii iliyoko Mezani kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye kipengele ambacho kinaangukia kwenye Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu na mimi nitumie tena fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ametoa uongozi, ametoa *blue print* kwenye hili jambo la janga la *corona* lililokuwa linaendelea kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, mimi ni msomaji na nimefuatilia mataifa mengi sana, wameiona dira ambayo Rais wetu ameitoa. Na kwa wale ambao walikuwa wanadhani ni mambo ya kubezana-bezana kama walivyozoea nadhani wamepata aibu baada ya kuona wale wanaowaamini katika kusahihisha mawazo yao wameona wakiweka vema msimamo ambao Rais Magufuli aliuchukua kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi neno Magufuli likitokea kwenye taarifa ya aina yeyote ile, Mataifa yote wanasimama kwanza watafute watafsiri wajue anatoa dira gani katika siku hiyo anayoiongea.

Mheshimiwa Spika, nikuombe pamoja na ratiba kubananabanana kwa kweli utafute siku tutengeneze Azimio liingie kwenye historia kwamba Rais wetu ametoa dira, ni vile tu muda hautoshi lakini ningekusomea kimoja kimoja ambacho alikuwa akisema leo, siku tatu baadaye Mataifa yote wanaenda kufanyia kazi na wanagundua kwamba alichokisema ni cha kweli.



Mheshimiwa Spika, wengine walikuwa wanataja Marais wa maeneo tofauti tofauti kwamba wanajitokeza asubuhi, jioni na mchana, lakini waliyokuwa wanayasema yalikuwa sawasawa na watangazaji wa kwenye TV, lakini leo hii Rais alikuwa akitokea akatoa hotuba, dunia nzima wanakaa wanatafakari na wanaona kwamba huyu ni Rais ambaye ametoa uongozi tena katika kipindi ambacho dunia iko kwenye taharuki na hiyo ndiyo maana halisi ya kutoa uongozi. Ametoa *blue print*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Tanzania imekuwa kwenye ramani ya kuonesha uongozi wa dunia nzima kama ambavyo Mwalimu Nyerere alikuwa akihutubia UN, kipindi Mwalimu Nyerere anahutubia UN, hata wale waliokuwa kwenye sehemu ya *cafeteria* kunywa chai walikuwa wanakimbia mbio kurudi wamsikilize Mtanzania huyu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, niwaombe Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, kwenye hoja hii tuliyonayo mezani wajue kwamba ni utaratibu wa Kiserikali. *Audit queries* zinapotolewa ni utaratibu wa kiserikali kwamba *queries* zinatolewa na baada ya hapo zinatakiwa zitafutwe taarifa zile ambazo zilikuwa zinakosekana kwa wakati huo ambapo zilikuwa zinatakiwa. Kwa maana hiyo Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge wasichukulie *conclusion* kwamba *audit query* ndiyo upotevu, wizi na ndiyo kila kitu. Ni utaratibu wa kiuhasibu ambapo baada ya hapo, *reconciliation* zitafanyika na kile ambacho kitakuwa kimekosa taarifa mpaka mwisho kabisa kwamba kimekuwa *confirmed* na taarifa za kiuchunguzi ndicho ambacho kitatakiwa kifanyiwe utaratibu ule wa kisheria. Sheria zitachukua mkondo wake kama ambavyo unajua Mheshimiwa Rais wetu hata kama kusingekuwapo na sheria yeyote inayoelekeza kuhusu upotevu wa mali ya umma, niwahakikishie Watanzania kwamba bado hatua zingechukuliwa na mali ya umma ingekuwa katika mikono salama kwa sababu mambo ya uadilifu na mambo ya kukemea upotevu wa fedha kwa Rais wetu imeandikwa kuanzia moyoni sio kwenye vitabu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *discrepancy* ambazo zinajitokeza katika baadhi ya maeneo ni uhitaji wa *reconciliation*. Kwa mfano, nikienda kwenye hoja iliyokuwa imetolewa kwenye hii Kampuni ya Mzinga, utaona kuna hoja ilikuwa imetolewa kwamba kampuni hii ukienda kipengele cha (c), inasema kampuni hii haina Bodi ya Wakurugenzi hadi sasa kinyume cha masharti ya uanzishwaji wake. Hii ilikuwa ni taarifa ya zamani kama nilivyosema, lakini hivi tunavyoongea kampuni hii ina bodi na Mwenyekiti wa Bodi, itifaki ya majina ya Kijeshi izingatiwe, *Comrade* Ndomba mstaafu anasaidiwa na *Chief of Staff* na Mtendaji Mkuu anakuwa Katibu wa taasisi hii na wajumbe wa Bodi wapo na wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hili lililokuwa limeandikwa kwamba imekuwa haina uwezo wa kujiendesha na inaendeshwa kwa hasara. Kipindi kile ilichotajwa ilikuwa katika kipindi cha uanzishwaji wake, lakini kampuni hii mtakumbuka kwamba imeshafanya kazi kubwa, imeshafanya kazi nzuri. Kuna kipindi kilichopita yalikuwepo tu matatizo ya ucheleweshwaji wa malipo ya kazi ilizokuwa imezifanya ndipo ikajulikana kama vile inaendeshwa kwa hasara. Ingekuwa inafanya biashara tungeweza kusema inaendeshwa kwa hasara kwa maana haikuweza kutengeneza fedha kutokana na kile ilichokifanya, lakini kwenye historia yake imetengeneza fedha. Ni kama ilivyokuwa ada kwenye taasisi nyingi, vipindi vilivyopita kulikuwa na kulala kwa madeni ambayo kwa sasa upungufu ule umeendelea kufanyiwa kazi. Kwa sababu imekuwa ikifanya kazi njema, naamini hata huo upande wa fedha, kipato chake kitaimarika kwa sababu kazi zake zinazofanyika ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaona kuna sehemu nyingine iliandikwa kuhusiana na mambo ya kiutendaji...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo. Ni vizuri tuwe tunajaribu kuangalia Kamati imependekeza nini *exactly* ili twende pamoja. Kwa nini nasema hivyo? Kamati imesema hivi: *“Kamati imechambua na kubainisha hali isiyoridhisha ya utendaji wa Kampuni ya Mzinga Holding Company ikiwa ni*

*pamoja na Kampuni kupata hasara mfululizo na hasara hiyo inasababishwa na mifumo."*

Kwa hiyo basi, wanashauri Bunge tuazimie kwamba: *"Shirika la Mzinga lifanye mapitio ya Mpango Mkakati wake ili kutathmini iwapo kampuni tanzu ya Mzinga Holding Company iendelee kutekeleza majukumu yake kwa muundo wa sasa au ivunjwe na kuunganishwa na shirika mama kwani shughuli zao zinashabihiana."*

Mheshimiwa Waziri, hiyo ndiyo *issue* ambayo iko mezani. hawaongelei Bodi, wanaongelea habari ya mfumo. Kama ninyi mnaona mfumo ulioko sasa unatosha, sawa, lakini hapa Kamati wanapendekeza kwamba tuangalie kama tunaweza tuka-*merge* au tukafanyaje ili kuondoa hizi hasara ambazo ni *serial*.

Karibu Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimeielewa hoja yako. Nilikuwa na-*derive*, kwa sababu hizi ni *conclusion* na masuala yale walivyoyasemea mpaka wakafika hapa vigezo vyake nimeviona walipokuwa wanaongelea taasisi hii. Kwa mfano, waliposema inakosa ufanisi, walielezea kwamba kuna miradi yake ambayo hajakamilika, walitaja Mradi kama wa Nyamagana, Mradi kama wa Jengo la Nyumba ya RASSingida, Mradi kama wa Makambako, pamoja na Mradi kama wa Jengo la DAS, Ikungi. Ndicho nilichokuwa nakisema sasa, ukienda kwenye taarifa za sasa, haya majengo wanayoyasemea yalishakabidhiwa na kwa sababu tuko Bungeni humu na yanatokea katika maeneo yetu, kwa mfano, haya mawili yanatokea Mkoa wa Singida ambako na mimi natokea...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, amesimama Mwenyekiti wa PAC, tumsikilize.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza kwa maelezo uliyomwelekeza msemaji wa sasa ambayo nafikiri angekuelewa. Hata hivyo, akumbuke kwamba baada ya Ripoti ya CAG kutolewa, Serikali inapewa siku 21 ya kujibu na kutoa hizo *verification*, lakini zaidi ya hapo, hawa Mzinga waliitwa kwenye Kamati na hawakuwa na majibu ya kuridhisha na ikumbukwe hii miradi tunayosema ni ya huko nyuma sana sio kwamba ni ya mwaka huu tunaouzungumzia wa fedha. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sana usilipotoshe Bunge hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti anachokisema na hiki ninachokisema, yeye mwenyewe anasema ile ilikuwa miradi ya zamani sana, sasa hiki ninachosema hii ni taarifa ya sasa. Hii ndiyo taarifa ya sasa, kwa hiyo kama zilishapita hatua zingine za miaka iliyopita ama vipindi vilivyopita na yeye apokeee ile iliyo taarifa ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kile ulichosema kuhusu muundo, kuna utofauti sana wa *setup* za taasisi hizi za mashirika hasa haya ya umma. Ni kwamba mashirika haya na si hili tu yako na mengine huu unakuwa mkono wa kufanyia kazi wa taasisi ya kiserikali, kwa maana hiyo hii *setup* inakuwa imetengenezwa kukidhi haja ya taasisi kufanya shughuli hizi kama hizi tunazozifanya.

Mheshimiwa Spika, ukisema uirudishe kwenye taasisi mama na hizi taasisi, asili yake kama unavyojua kuna taasisi zingine majukumu yake hayakuwa haya ambayo yanafanywa na mkono wake wa kufanyia shughuli hizo. Kwa mfano, ukichukua taasisi mama kwenye vyombo hivi, utakuta kwamba majukumu yao ya msingi ya vyombo haikuwa kufanya shughuli zile ambazo wametafuta mkono wa kufanyia shughuli za aina hiyo kwa maana hiyo *set-up* yake ya aina hii ni *set-up* sahihi inayoweza Taasisi mama kufanya majukumu ya msingi ya uanzishwaji wa taasisi na ule

mkono wake wa kufanyia shughuli hizo za biashara ama shughuli hizo za kikampuni uweze kufanywa na hiyo taasisi ambayo imepewa majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye taasisi hizi, kipindi cha miaka 10 kuanzishwa kwake inakuwa na vipindi vya mpito. Vya kwanza ni vya kutengenza namna ya kujipanga kwenye majukumu hayo na mengine ni yale ya kujimarisha kwenye shughuli ile, ndiyo maana utaona hata mipango kazi yake iliyokuwa inatengenezwa walianza kwanza na mipango ya muda mfupi na hata majukumu yake waliyokuwa wanatekeleza wameanza *effectively* katika baadhi ya majukumu, hawakwenda na yote kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo niliombe Bunge lako Tukufu liliridhie taasisi yetu hii iendelee kwa muundo huu uliopo kwa sababu tayari wameshafanyia maboresho mengi ambayo yanatofautisha na kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Spika, ni mambo mengi ambayo ukipitia kimoja baada ya kingine utaona kwamba yaliyokuwa yanajitokeza kama upungufu umeshafanyiwa marekebisho na sasa tunakokwenda tunaamini itafanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi. Ukirudisha zile taasisi zao mama ukazipatia majukumu haya yanayofanywa na mashirika haya ambayo ni mashirika ya kufanyia kazi, maana yake utaenda kwenye mchanganyiko wa taasisi mama kwenye majukumu ya msingi ukachanganya na haya ambayo yanatumika kimsingi katika shughuli hizi za kiuzalishaji.

Kwa hiyo ule uliokuwa unajitokeza kama upungufu utaendelea kufanyiwa kazi na kama nilivyosema yale ambayo mengine yatahitaji ufafanuzi wa kina zaidi Serikali itaendelea kutoa ufafanuzi kama ulivyoelekeza katika moja ya eneo ambalo taarifa inatakiwa sasa itolewe rasmi inayoelezea *status* ya sasa. Yale yaliyokuwa yanajitokeza ya mwanzo ni tofauti na sasa ambavyo imeshafika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Ninyi mtulie! Kwenye kushauri ninyi mbona mlishashindwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hiyo ni kengele ya pili. Sasa ushauri wa Waziri ni tofauti kidogo na hiki kilichokuja hapa, lakini kwa kuwa hawakuwa wameleta *amendment* ushauri wetu unabakia Mheshimiwa Waziri na ni ushauri ambao wala hauna shida endapo... maana sina *background* ya kutosha kuhusu jambo hili, lakini endapo kuna hasara mfululizo na walichopendekeza tu ni muangalie mpango mkakati uliopo huenda unahitaji *tying up* ya hapa na pale. Yaani ni ushauri ambao hauna, uko tu vuguvugu, wala hauna *controversy* yoyote, *just in case* ni kweli kwamba kuna hasara za namna hiyo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Simbachawene nilikutaja na atafuatiwa na Mheshimiwa Hasunga.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu, lakini pia nikupongeze wewe kwa kazi nzuri unayofanya ya kulisimamia Bunge katika kipindi hiki cha lala salama. Nadhani unatujenga vizuri na nadhani tutaenda na kurudi salama.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeguswa kupitia taasisi inayoismamia ya *NIDA* na nianze kabisa kupongeza sana kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya *PAC* kwa kufanya uchambuzi makini na kutoa maoni yake ambayo mwanzo kabisa niseme sisi kama Wizara tunayachukua yote kama ulivyoshauri juu ya *NIDA* katika maeneo yale mawili.

Pia kazi yenu nzuri imefanywa kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Ofisi ya *CAG*, kwa hiyo nimpongeze sana Mtendaji Mkuu wa Ofisi hii ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali bwana Charles Kichere pamoja na

wasaidizi wake kwa kufanya kazi nzuri ambayo imesababisha Bunge nalo kufanya kazi nzuri ambayo sisi nasi Serikali tunaipokea kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyoguswa yanahusiana na *NIDA* na la kwanza linahusiana na mikataba yaani *data sharing agreement*. Kutokana na *data* hizi ambazo sasa *NIDA* tunazo ni biashara ambayo tunataka kuwauzia watumiaji wengine na kwa hiyo kulikuwa kuna maoni makubwa, mtakumbuka kwamba yalitolewa hata humu Bungeni na kupitia Kamati mbalimbali lakini yalikuwa yanahitaji pia mchakato, maana tusingekwenda kwenye kuanza kuuza hizi *data*, bila kuwa na mfumo wa namna ya kuzitunza hizo fedha na namna ya kuzitumia. Sasa katika hili, Wizara inayokusanya mapato au kuridhia tozo zozote zile hapa nchini ni Wizara ya Fedha. Kwa hiyo tarehe 20 Februari, Wizara ya Fedha ilipitisha na kukubaliana na tozo hii kupitia kwa Wizara yetu na kwa hivyo mchakato ule ukakamilika.

Mheshimiwa Spika, tangu tarehe 20 hadi leo hii Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini pia kwa ku-*consult* Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ametukubalia tupitisha mikataba 63 ambayo ameidhinisha. Hadi sasa mikataba iliyosainiwa na makampuni au na taasisi nyingine ni mikataba saba na mikataba 14 imekwishapelekwa kwa wadau. Kwa hiyo tunaamini tukiendelea hivi tukifika, wakirejesha basi na sisi tunapeleka mikataba hii inasainiwa na tunaamini kwamba ziko fedha nyingi sana zitakazokusanywa na kupelekwa Hazina kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo eneo hili ni eneo la chanzo kizuri sana cha ukusanyaji wa mapato na sisi tumefika hadi hatua hiyo. Kwa hiyo pamoja na ushauri mzuri wa Kamati, hii ndiyo *current status* ya hili eneo na niwapongeze mara nyingi wametuambia na kupitia Kamati ya Bajeti pia walituambia suala hili, tumefika hatua hii, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la pili linahusiana na utunzaji wa malighafi za kutengeneza vitambulisho vya Taifa (*raw cards*). Hizi *raw cards* tumeziwekea utaratibu mzuri wa

kuzitunza, zina namna yake ya kuzitunza, lakini pia hizi *raw cards* si kwamba zilinunuliwa nyingi bila kuzingatia mahitaji. Mahitaji kwa *target* yetu ya mwaka 2019/2020 ilikuwa ni kutengenza vitambulisho, kutoa vitambulisho kwa Watanzania milioni 24 na hadi sasa tumetoa vitambulisho milioni sita. Hizi *raw cards* tulizonazo mpaka sasa ni milioni 4,800,000. Kwa hiyo hata hizi zenyewe hazitoshi, inabidi tununue kadi nyingine ili tuweze kufikia *target* ya milioni 24.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa tumeipata ni pale mitambo iliposindwa kufanya kazi vizuri, ile ya zamani. Hivi sasa kama nilivyosema wakati wa bajeti ya Wizara yetu, tumejitahidi na Serikali imetoa fedha, mitambo mipya imenunuliwa kutoka Ujerumani ambayo tumeifunga, lakini hata ile mitambo ya zamani tumegundua kwamba ilikuwa inaweza kuendelea kufanya kazi kama ingekuwa imetunzwa vizuri na yenyewe hatuna nia ya kuitupa. Tunataka na yenyewe tuikarabati ili ifanye kazi kwa sababu shughuli ya utoaji wa vitambulisho ni shughuli endelevu, kila siku watu wanazaliwa wanafikia ule umri wa kupewa vitambulisho, basi wataendelea kupewa vitambulisho. Kwa hiyo hatudhani kwamba kuna haja ya kuitupa ile kwa hiyo, mitambo hii yote tutaitengeneza ili iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa hizi *raw cards* ambazo zilikuwa zitumike kwenye mashine ile ya zamani, tumetengeneza mfumo mpya, tumekuja na *module* ambayo inaweza ikatumika hata kuzalisha vitambulisho kwenye mashine hizi mpya. Tulitaka kuchezewa tu kidogo kwamba zile *raw card* haziwezi kutumika kutengeneza vitambulisho kwenye mashine mpya lakini wataalam wamefanya tuliyoweza kufanya na niwapongeze sana *NIDA* kwa kweli ni vijana wetu *IT Specialists* wameweza kuja na utalam huo wakasema hapana, kwa nini waseme hizi haziwezi kuzalisha vitambulisho huko na wameweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunasubiri tu wale waliotu-*supply* ile mitambo, wale Wajerumani, waje lakini kwa sababu ya *corona* walikuwa wamesita kuja na hivi sasa anga limefunguliwa wanaweza wakaja wakati wowote. Mitambo



hii mipya itaanza kufanya kazi na uwezo wake ni mkubwa, kwa saa moja inatoa vitambulisho 4,500. Kwa miwili itatoa vitambulisho 9,000 kwa saa moja. Kwa masaa 16 kwa kila siku, tunaweza tukatoa vitambulisho 144,000 kwa siku moja.

Kwa hiyo tukifufua na mashine zile za zamani tutaweza kuzalisha vitambulisho kama 12,000 kwa siku. Kwa maana hiyo tunaweza tukahitaji siku 115 tu, ambayo ni kama miezi minne kuzalisha vitambulisho milioni 18 vilivyobakia. Kwa hiyo tuna uwezo mkubwa isipokuwa tu mambo haya ya *corona* yametucheleweshwa, lakini tunaamini sasa jibu limepatikana.

Mheshimiwa Spika, hatua kali kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe tumezichukua, *NIDA* tumeisafisha, pametulia sasa, ile vurugu vurugu iliyokuwepo haipo tena. Watanzania wako wengi, wale waliokuwa wanavurugavuruga pale tumewaondoa, tumewapeleka sehemu nyingine, pale tumeleta watu wengine na shughuli inaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu tena na kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake dhidi ya janaga hili la corona. Na kusema ukweli heshima ya Taifa lolote lile inabebwa na kiongozi wake na msimamo wa kiongozi wa Taifa ndiyo msimamo wa nchi. Unapokuwa na kiongozi wa aina ya Rais Dkt. Magufuli anayekubali kusimama na kutofautiana na taasisi nyingi, vyombo na watu wengi na msimamo wake ukaigwa baadaye, hii ni heshima kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa hivyo Watanzania tuna kila sababu ya kujisifu na kutembea kifua mbele kwasababu tumetoa *leadership* ya dunia katika wakati ambao kuna *confusion*. Wapo watoaji wa maoni mbalimbali duniani walisema katika jambo hili la corona hivi nani anatoa *leadership* ya dunia? Kwa hivi sasa uki-*way* katika Marais wa dunia, aliyetoa *leadership* ni Mheshimiwa Rais Magufuli ambaye kila alichokisema ndicho kinachokuja baadaye kinatokea lakini sasa amesaidia dunia sasa inajadili ukweli juu ya masuala kama haya; masuala ya afya za dunia itajadili

ukweli lakini *study*yake itatoka Tanzania na imeletwa na Rais wetu, tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe binafsi uliposimama kidete ukasema lazima Bunge tutaendelea. Hivi kama sisi Wabunge tungekimbia ndani ya Bunge halafu wananchi huko wangekimbillia wapi? Na wao wangeanza kutukimbia sisi maana wangesema sisi ndiyo tumeondoka na corona humu. Kwa hiyo, msimamo wako na wewe pia utakumbukwa kwamba ulisimama na kusimamia Bunge katika kipindi kigumu ambacho kulikuwa kuna *confusion*.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilikupigia simu nikakwambia Mheshimiwa sasa tunakwendaje hapa, ukaniambia mdogo wangu hapa mambo yatakwenda; tunaomba Mungu mambo yatakwenda. Na kweli leo hata barakoa wengine hatuvai, tukitoka hapa tunapiga chai yetu ya tangawizi na nini tupo sawa, tukipima tupo vizuri na nyungu tunapiga, maisha yanaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niseme haya, nikupongeze wewe lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa mshikamano tuliouonesha katika kipindi cha janga hili na sasa linaendelea kupungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja na mapendekezo yaliyotolewa na kamati na sisi tumeyapokea, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kweli umetukumbusha jambo muhimu kipindi hiki cha corona tutasimulia kwa kweli miaka ijayo jinsi ambavyo hata Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka tulivyotingishika ilikuwa tunaulizana hapa hivi inakuwaje hapa. Ilifika wakati palikuwa pagumu kweli lakini kwasababu tunaye kiongozi Mkuu wa Nchi ambaye alikuwa amechora mstari ameweka dira kila tukifanya *reference* anasema tusonge mbele na ndiyo maana nikawaambia Waheshimiwa Wabunge shughuli hii itakwisha. (*Makofi*)

Na kwa kweli tumejaribu kwa njia mbalimbali, pitia kanuni hivi twende hivi na tunavyoona kama tarehe 19 mwezi huu unaokuja kama vile itakwisha yaani hii shughuli yetu hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu na kwa kweli tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uimara. Jambo kama lile/mtihani kama ule ukabaki imara inataka kweli uwe na rehema za Mwenyezi Mungu siyo rahisi kabisa, mahali ambapo hata miti mikubwa imetepeta mataifa makubwa yametingishika sasa hivi wanalumbana wengine wanafukuzana kazi, wengine wanaachia ngazi kwasababu ya hiyo *lockdown*; wengine wanadai fidia huko na kadhalika. Kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu halijapita hili janga lakini *so far so good*, Mheshimiwa Waziri Hasunga. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi katika hoja chache ambazo nitaweza kufafanua.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikupongeze sana kwa kusimamia majadiliano haya na jinsi watu ambavyo wameweza kujadili katika Bunge hili Tukufu na hasa kwa kuzingatia kwamba tunazungumzia usimamizi wa mali na fedha za umma, kwa kweli umefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa ndugu yetu Kichere kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi kifupi na ripoti nzuri sana ambayo kwa kweli ameifanya. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Kichere na wakati anateuliwa watu wengi waliamini kwamba amekwenda kuzuia hataweza kufanya kazi *objectively*. Lakini kwa *issues* ambazo zipo kwenye ripoti hii zinaonesha kabisa kwamba Kichere yupo *objective* na taasisi ya *CAG* ni *independent* na anafanya kazi kwa uhuru kwa kweli ule ambao Bunge tunatarajia. Na kwa kweli hili ni jicho letu na sisi kama Bunge tuna kila sababu ya kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Kamati ya PAC na naomba niseme tu kwa kipindi kifupi hiki na hasa uliposema mwanzoni wakati tunaanza Bunge hili ukasema kazi hailali, PAC na LAAC muhakikishe mnachambua hizi ripoti mnaleta ripoti kipindi hiki, wengi tuliamini kwamba hawataleta ripoti lakini ripoti waliyoleta ni nzuri sana; tunawapongeza sana. kwa kweli PAC mmefanya kazi nzuri sana, mmechukua *issues* za msingi *issue* zile ambazo kwa kweli ni *strategic* na sisi Wabunge tuna kila sababu ya kuwapongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yamesemwa kuhusiana na Wizara ya Kilimo na mimi niyatasema na hasa sana suala la Bodi za Mazao. Wamesema Serikali ilianzisha Bodi za Mazao kwa ajili ya kusaidia kuhakikisha zinaongeza tija, zinasimamia masoko, uongezaji wa thamani ya mazao. Pia kuhakikisha kwamba kilimo cha nchi hii kinakuwa, ni kweli kabisa huu ndiyo msingi wa kuanzisha bodi. Na kwa kweli Bodi za Mazao katika Wizara ya Kilimo tulizonazo zipo 9 na kila bodi inasimamia zao fulani kasoro bodi ya 9 ndiyo inasimamia mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, bodi ni nyingi na hoja ya CAG ni kwamba bodi hizi zimekuwa ni utitiri na nyingine uwezo wake wa kimapato umekuwa ni mdogo na naomba nikiri kabisa kwa ripoti jinsi walivyoisema na walivyoichambua nakubaliana. Kwa mfano Bodi ya Chai wamesema mapato yake kwa mwaka mzima mapato yalikuwa shilingi milioni 649.4 lakini ukilinganisha na matumizi ya milioni 818. Ni kweli kabisa, ukichukua bodi ndogo kama ya pareto wana mapato milioni 248.8 kwa mwaka lakini matumizi milioni 264 kwa mwaka, ni kweli kabisa. Kwa hiyo, ukiangalia bodi nyingi, bodi zetu kwa kweli mapato yao ni kidogo na ufanisi umekuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ili kuweza kuleta mabadiliko makubwa, tulianza kufanya mabadiliko kupitia sheria yetu, kwanza tulipitia sera na tumeanza kupitia sheria zetu ndiyo maana sasa hivi tupo kwenye mchakato wa mwisho wa kuunganisha bodi hizi ili tuje sasa na mamlaka za kusimamia mazao. Tunafikiria badala ya kuwa na bodi 9, tuwe

na mamlaka mbili; mamlaka ya kwanza isimamie mazao ya kimkakati na mamlaka ya pili isimamie mazao ya nafaka, mchanganyiko na mazao ya bustani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hizi mamlaka zisimamie kuanzia hatua ya kwanza mpaka kwenye masoko na uongezaji wa thamani ili kusudi sasa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa ni nchi ya viwanda tuweze kufanya hivyo. Naamini kabisa kwa mapendekezo haya na sisi kama Serikali tunakubaliana kabisa na sisi tunalifanyia kazi na Bunge hili lingekuwa na nafasi ningesema hata wiki mbili hizi naweza kuleta hiyo sheria hapa ya kuunganisha hizo bodi ili tuwe na mamlaka sasa za kusimamia mazao. Kwasababu tumejipanga tunaendelea, ipo ndani ya michakato na michakato ipo kwenye hatua nzuri kabisa za kuweza kukamilisha. Na hii itatusaidia katika rasilimali hizi chache sasa tuwe na uhakika namna ya kuzitumia kama ni rasilimali watu, rasilimali fedha na kila kitu kiweze kutumika ipasavyo, hii itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Bunge kwa ujumla ni kwamba tunapitia Sera, sheria mpya ambayo itaunganisha tutakuwa na sheria moja ya kilimo ambayo pamoja ndani ya hiyo kutakuwa sasa na mamlaka za mazao mbili ambazo tutazianzisha kama sheria hiyo itapita kama ambavyo tunapendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunakusudia kwamba sasa hivi kuangalia eneo la mazao ya bustani ambapo kwa sasa hivi fedha nyingi sana ndiyo zinapatikana na watu wengi sana wanakwenda katika hii sekta. Nchi kama ya Kenya sasa hivi wanaingiza zaidi ya Dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka kutokana na hii sekta, sisi tunaingiza kwa mfano mwaka huu tumeingiza milioni 779 Dola za Marekani. Kwa hiyo, tunafikiri tukiwekeza kwa eneo tulilionalo tukaweka vizuri tukawa na mamlaka ya kusimamia haya, tunaweza tukafanya vizuri na tukaona mchanago mzuri utakaoweza kutolewa katika hili. Kwa hiyo, mimi katika hilo naomba niseme tunakubaliana na mawazo ya kamati.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo la pili kwa ruhusa yako linahusu Wizara ya Maliasili na Utalii na hili linahusu matumizi ya fedha bilioni 1.5. Ni kweli wenzangu wa maliasili wamenomba nilifafanue kidogo, kwa ruhusa yako naomba nitoe ufafanuzi kidogo. Katika kukuza na kutangaza utalii wa nchi yetu na katika kuongeza mazao ya utalii na kuhakikisha watalii wanakaa kwa muda mrefu nchini ili waweze kutumia hela nyingi zaidi, Wizara ya Maliasili na Utalii iliamua kuanzisha tamasha maalum lililojulikana kama *Urithi Festival*.

Mheshimiwa Spika, tamasha hilo wakati tunalianzisha tuliweka kwenye bajeti, si kweli kwamba hela hazikuwepo kwenye bajeti, kwenye bajeti ziliwekwa lakini hela zilizowekwa kwenye bajeti hazikutosha; ziliwekwa shilingi milioni 50. Ilipoenda kwenye utekelezaji wataalam wale walipoenda kwenda kutaka kutekeleza tuliamua kuwa na vituo sita vya kuendesha tamasha kwa muda wa mwezi mzima, tuliamua kwamba tuendeshe siku saba Dodoma, siku saba Zanzibar, siku saba Dar es salaam, siku saba Arusha, siku saba Karatu na siku 7 kule Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika siku zote hizo kilichokuwa kimeamuliwa ilikuwa ni kwamba wenzetu walipokuja na bajeti mara ya kwanza ilikuwa ni bilioni 5.4. Tulipoangalia bilioni 5.4 tukasema haiwezekani kwa tamasha hili, tukapunguza na Mheshimiwa Waziri alipopata matatizo akawa anaugua nilimfuata mpaka hospitalini nikamwambia naomba unipe mamlaka tukate kila kitu ili watumishi hawa wajitolee ili hili tamasha lifanyike na kweli aliruhusu tukakata mpaka ikabaki bilioni 1.4 na nikawaambia watumishi wa Wizara wajitolee lakini ilifanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa sehemu kubwa ilikuwa ni nini? Watu wanahoji kuhusu wasanii. Tamasha maana yake unahitaji kuvuta watalii, ili uvute watalii lazima ulete wasanii ili wale wanapotumbuiza pale ndiyo watu watavutiwa. Unahitaji kutangaza utalii na utamaduni lazima uwalete watu wa aina mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali waje na utamaduni wetu kuja kuuonesha na ndicho kilichokuwepo lakini kubwa zaidi lazima itangazwe *live* kwenye TV, redio na

magazeti yote, kazi ilikuwa ni kubwa. Kwa matangazo yale ya mwezi mzima *live* ni kwamba... (*Makofi*)

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Unaweza ukakuta kwamba mpaka hadi kwa wastani ni kila tukio...

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga kuna taarifa ya Mheshimiwa Mollel.

## T A A R I F A

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa Mheshimiwa Hasunga taarifa kwamba ishuru siyo wasanii, ishuru ni pesa kutumika nje ya bajeti; hilo ndiyo swali letu kubwa kwa nini pesa zimechukuliwa nje ya bajeti na siyo hivyo tu, imechukuliwa kwenye taasisi ambayo kinidhamu ya pesa hairuhusiwi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba tu anisikilize naenda hukuhuko anakosema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nataka kusema watalii walitumika na vyombo mbalimbali vilitumika kwa ajili ya kutangaza hili. Sasa hoja ilikuwa ni kwamba fedha zilitumika nje ya bajeti. Ambacho nimeambiwa ni kwamba kweli bajeti ilikuwa haitoshi lakini utaratibu wa Serikali uliopo ni kwamba kwanza walikuwa na mfuko wa kuendeleza utalii, fedha za mfuko wa kuendeleza utalii ndiyo zilizotumika; zimechangwa na mifuko mbalimbali zimewekwa kule hiyo tulivyoona kwamba hazitoshi zilichukuliwa zile fedha kuja kusaidia kutangaza huu utalii.

Mheshimiwa Spika, la pili; fedha za taasisi hizi za uhifadhi zimetenga fedha kwa jili ya ku-*promote* utalii, zile fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ku-*promote* utalii ziliombwa kuja kusaidia kuanzisha hili tamasha.

Mheshimiwa Spika, la tatu, na kitu ambacho ni cha muhimu tarehe 19 Juni, 2019 waliandika barua ambayo ninayo hapa na ipo kwenye kumbukumbu ambayo baada ya kuona kwamba zile fedha za ziada zilitumika hazikuwa kwenye bajeti maana yake ilitakiwa wafanye *reallocation* wakaomba hazina kibali cha kufanya *reallocation* na *reallocation* ikawa approved. Sasa kama *reallocation* ilikuwa *approved* sijaona tatizo lakini bado ninachotaka kusema sina... (Makofi)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa...

**WAZIRI WA KILIMO:** ...maana kwamba matumizi yalivyotumika inawezekana ni halali au siyo halali; bado nakubaliana na maoni ya kamati kwamba waende wakazihakiki waangalie matumizi yake kama yalikuwa sawasawa lakini kama ni suala la kibali cha *reallocation* barua hii ya tarehe 19 Juni, 2019 ilienda hazina ikaomba *reallocation* ili kuthibitisha sasa kwamba fedha zile zinahamishwa na zinatumiwa katika ku-*promote* utalii.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hoja ambayo wanasema kwamba hawajaona matumizi/faida, huwezi ukatangaza utalii leo ukaona faida leo, inachukua miaka; hii ni *investment*. *Investment* hii matokeo yake tunaweza tukapata baada ya miaka 3/5 na ndiyo maana mwaka huu pamoja na kuwepo kwa corona Mheshimiwa Rais ameshatangaza amesema *booking* za utalii kuja Tanzania zimejaa, inawezekana ni kwasababu ya *Urithi Festival* imechangia katika kutangaza hivi vivutio kwa hiyo watu wengi watakuja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema matumizi haya faida yake itaonekana *gradually* kadiri tunavyokwenda na naamini kazi iliyofanyika ilikuwa ni nzuri na watumishi wale kwasababu nakumbuka tulikata posho zao zote nikawaambia wajitoleee kama hapa Dodoma...

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa



**WAZIRI WA KILIMO:** wachache tu waliotoka sehemu nyingine ndiyo waliolipwa *per Diem* kwa hiyo naamini...

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** ...watafanya kazi nzuri na wata...

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lulida

### T A A R I F A

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa heshima na taadhima nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri anayezungumza sasa hivi kwamba Serengeti peke yake ilikuwa inatoa bilioni 26 lakini sasa hivi Serengeti inatoa bilioni 137 kwa ajili ya utalii. Na *TANAPA* miaka miaka mitano nyuma ilikuwa inapata mapato ya bilioni 57 sasa hivi inapata mapato ya bilioni 257. Bado tunahitaji pesa za kutosha kwa ajili ya kufanya *promotion* na *marketing* ili nchi yetu iweze kupata pesa zaidi na kuvunja na kuhakikisha mianya ambayo inaendelea imepungua ya ujangiri na wanyamapori wanazidi kuendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara waendeleo kutafuta pesa za *promotion* waziweke katika utaratibu ili utalii uweze kuwa mkubwa na nchi yetu iweze kuruka kama wenzetu wakiwa Kenya, nakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Taarifa ya mama utalii hiyo, Mheshimiwa Waziri unaipokea.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili na nataka kuongezea tu kwa kusema kwamba ndiyo maana wameongezeka hapa nchini inawezekana ni kwa sababu ya *Urithi Festival* lakini mapato ya kitalii yameongezeka na pia kujulikana kwa vivutio mbalimbali vya nchi yetu vimekuwepo matangazo yanaendelea, hali ni nzuri kabisa...

**SPIKA:** Catherine Ruge unasema nini, nimekuona umesimama.

## T A A R I F A

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba pesa zilichukuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii zilitoka Ngorongoro, *TANAPA*, *TAWA* na *TFS* na sivyo ambavyo wewe unasema, *according to CAG Report*. Lakini unasema mmepata *approval ya reallocation*, siyo kweli kwasababu *CAG* ameonesha kabisa kwamba haukupata *approval* ya Waziri wala ya *CAG* kutumia pesa nje ya bajeti. Kwa hiyo, usilipotoshe Bunge Mheshimiwa Waziri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hajapotosha Bunge, amesema fedha zilitoka huko unakoeleza lakini huko pia zilikuwa na madhumuni ya kutangaza utalii kwa hiyo, zikachukuliwa badala ya madhumuni ya kutangaza utalii huko, baadhi ya hizo fedha sio fedha zote, baadhi ya hizo fedha zikapelekwa kwenye *Urithi Festival*. Mheshimiwa Waziri kwa sentensi moja tu ili tumalize.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa hilo, na nataka kusema tu kwamba Mheshimiwa Mbunge anayosema mimi ni *auditor* na *accountant by professional* na najua ninachokisema, siwezi kusema kitu ambacho sina ushahidi. Ninayo hapa naonesha na barua imeenda lini na kumbukumbu namba ninayo. Kwa hiyo, si kwamba labda ni vitu ambavyo navisema tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba bado nakubaliana na ripoti ya *audit* kwamba kuna haja ya kufanya tathmini kwa undani.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie kwamba kuna manufaa makubwa sana ambayo yanapatikana kwenye upande wa utalii. Na niwapongeze Wabunge wote na niwaombe waendeleo kutangaza utalii na sisi sote tukiwa na utamaduni wa kutangaza utalii nchi yetu itasonga mbele.

Na ndiyo maana nasisitiza watu waendeleo kula maisha ili kusudi tutangaze utalii wa ndani na nchi yetu iweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, asante sana na nakushukuru sana.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Kampeni yako ya kula maisha huwa naipenda sana hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa sababu mimi ni mmoja wa wahanga wa kujaribu kufyatua tofali mpaka uzeeni, nikiangalia nilichofaidika sikioni. Sasa Mheshimiwa Hasunga alisema bwana, pamoja na kubana kwa sisi Waswahili unachopata kula bata kidogo; na kula bata kidogo ni pamoja na utalii. Kutangaza utalii jamani ni ghali; kusema ukweli ni ghali (*very expensive*), siyo kitu rahisi kuandaa matamasha haya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tafadhali una hoja kama mbili tatu hivi halafu Mheshimiwa Waziri wa Nchi utatufungia upande huo. Mwenyekiti wa Kamati jiaandae utakuwa na dakika chache maana yake tumekuunga mkono kwa kiasi kikubwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pia nami nianze kwa kuipongeza Kamati ya PAC kwa kufuatilia vizuri mapato na matumizi ya fedha za Umma na kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wetu katika eneo hili ambalo amelipa umuhimu mkubwa toka aliposhika kiti cha uongozi.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze CPA Charles Kichere (*CAG*), kwa kweli ameitendea haki hata *title* yake ya CPA, lakini kwangu mimi hasa hasa kwa kuvunja mwiko wa kuanza kukagua hesabu za mashirika yale makubwa ambayo tulikuwa tunaambiwa ukaguzi hauwezi kufanyika bila kutumia *auditors* wa nje. Hongera sana CAG Kichere kwa kazi nzuri. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri, kwa kweli hii ni hoja muhimu na hoja nyeti.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui kama nitaweza kutendea haki hoja zote zilizosemwa, lakini ngoja nijaribu. Kwanza nianze na ile ya *Pride*. Kama Serikali tumehangaika sana na *Pride*; sana, sana. Maana kwa kipindi kirefu imekuwa inaendeshwa kinyemela kama kampuni binafsi mpaka tarehe 18 Oktoba, 2018 ndipo Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia Divisheni ya Biashara ilipotoa uamuzi wa makubaliano (*consent judgment*) kuwa *Pride* ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, pamoja na hatua nyingine ambazo Serikali imefanya kuitwaa rasmi *Pride* lakini tulihitaji kuhakiki mali na madeni ya *Pride* na zoezi hili limefanyika na limekamilika.

Mheshimiwa Spika, pia ni Serikali hiyo hiyo ambayo ilimwagiza *CAG* kufanya ukaguzi maalum ili kuiwezesha kufanya maamuzi stahiki. Niliambie Bunge lako Tukufu kwamba ukaguzi huo umekamilika na tunaendelea kuichambua hiyo taarifa ili tuweze kuchukua hatua za haraka kuboresha utendaji wa *Pride*. Timu ya wataalam ambayo imeundwa ndani ya Serikali ipo, inaendelea na kazi ya kuchambua.

Mheshimiwa Spika na Bunge lako, nikuhakikishie kabisa kwamba wale wote waliojamilikisha *Pride* wakala fedha za Umma, wakachukua na viwanja, hawa tutawashughulikia kwa mujibu wa sheria za nchi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa hiyo kwa sababu imetupa moyo sana, maana watu walishajibinafsishia *Pride*.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Kabisa.

**SPIKA:** Endelea tu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Labda niseme suala lingine kuhusu Benki Kuu na fedha ambazo walizikusanya kwenye maduka ya kubadilisha fedha, miaka miwili iliyopita walitaka kujua hatima yake. Niseme tu tulilazimika kufanya huu uchunguzi kwa sababu kulikuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa

wadau mbalimbali kwamba miamala inayofanywa inajihusisha pia na ukwepaji kodi na vile vile kulikuwa na *channels* za utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulifanya hivyo na uchunguzi ulibaini uvunjifu wa sheria na kanuni za nchi ambayo ndiyo ilipelekea tukachukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufuta leseni na kuwataka walipe kodi zile ambazo zilikuwa zimekwepwa.

Mheshimiwa Spika, wenye maduka yale ambayo yalikuwa yamechukuliwa kwa uchunguzi walitakiwa wafanye majadiliano na *TRA* na kwa wale ambao wamefanya hivyo na wameonesha nyaraka mbalimbali, tumechukua hatua ikiwa ni pamoja na kuwarudishia vifaa na nyaraka mbalimbali ikiwemo fedha taslimu.

Kwa hiyo, maduka yote ambayo yamemaliza majadiliano na *TRA* tayari wamerudishiwa na wale waliolipa kodi stahiki, isipokuwa yamebaki maduka 10 tu ambayo ndiyo huo mchakato unaendelea. Wakimaliza majadiliano watarudishiwa vifaa vyao tukishajiridhisha kwamba tuko sawa sawa, operesheni zao zinaendana na maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kuhusu Benki zile mbili za Uwekezaji Biashara na Benki ya Maendeleo. Niseme tu kwamba tumefanya tathmini ya hizi benki na tathmini imekamilika; na Serikali imefanya maamuzi ya kuunganisha *TIB Corporate* na *TPB Bank Plc* kutokana na ukweli kwamba hizi benki mbili zinafanya biashara zinazoshabihiana. Uamuzi huu kwa kweli umelenga kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji. Pia itakuwa ni utatuzi wa changamoto ile ya mtaji ambayo ilikuwa inaikabili *TIB Corporate*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya *TIB Development*, uamuzi wa Serikali ni kwamba benki hii iendelee kutoa huduma ya mikopo na mitaji ya muda mrefu kwa ajili ya mahitaji ya uchumi wa nchi. Kwa hiyo, changamoto ya mtaji tutaishughulikia kadri tunavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya *BoT* kuhusu kurekebisha dosari...

**SPIKA:** Kidogo tu mwisho Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, umesema hii ya Maendeleo... wana *branch* mbili; Uwekezaji na Maendeleo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, *TIB Development* uamuzi wa Serikali ni kwamba benki hii itaendelea kutoa huduma za mikopo na mitaji ya muda mrefu.

**SPIKA:** Kwa hiyo, zinaendelea zote mbili au!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hapana. *TIB Corporate* na *TPB Bank Plc* hizi ndiyo zinaunganishwa. *TIB Development* inaendelea.

**SPIKA:** Tumekuelewa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sasa kuhusu dosari zile za kuhesabu fedha ambazo zimechakaa ambazo zinatoka kwenye Benki za Biashara, napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli kuhesabu noti chakavu zilizotoka kwenye *Commercial Banks* zinachukua muda mrefu. Tulichofanya, Benki Kuu imeagiza mashine 10 za ziada ili kuweza kuongeza uwezo wa kuhesabu fedha ambazo zinatoka kwenye *Commercial Banks*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shida sasa kwenye fedha chakavu ni vigumu sana kuzihesabu kwa sababu unapoweka kwenye mashine haziwezi kupita bila kuchanika chanika. Kwa hiyo, tunakuwa na hiyo *challenge*, inabidi zihesabiwe kwa mkono na hiyo ndiyo inasababisha zichukue muda mrefu.

**SPIKA:** Na wakati huu wa Corona tena, mtihani.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Eeh!

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tumefanya mambo kadhaa, kwanza ni kuhakikisha kwamba benki zinachakata noti ambazo wanazipokea kutoka kwa wateja wao na kuzirudisha kwenye mzunguko zile tu ambazo wanaona walau ni safi na zile ambazo hazifai kurejeshwa kwenye mzunguko, ndiyo zinazowasilishwa Benki Kuu. La pili, ni kuendelea kutoa elimu kwa Umma juu ya njia sahihi ya utunzaji wa hizi fedha ili zisichakae mapema. Wote ni mashahidi jinsi fedha zetu zinavyokuwa *handled* hasa kwenye masoko na sehemu nyingine. Pia tumeongeza ufanisi katika kusambaza noti safi na hata noti mpya ambazo tumezichapisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nisemee pia ille la kuviboresha na kuviwezesha vyombo vinavyotoa maamuzi kuhusu mashauri ya kodi. Kwa kweli tunaendelea kutenga fedha na kuviwezesha kibajeti hivi vyombo; *Tax Appeals Board* na *Tax Appeals Tribunal*. Nitoe tu mfano, mwaka huu wa fedha tumetoa jumla ya shilingi bilioni 937.3 kwa ajili ya *trub* ambayo ni sawa na asilimia 90 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa upande wa *Appeals Tribunal* tumetoa shilingi bilioni 837.4 ambayo ni asilimia 83 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na hii ni kwa kipindi cha miezi tisa tu mpaka Machi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uongozi, Serikali imefanya mabadiliko hivi karibuni kwenye uongozo wa *Tax Appeals Board* kwa lengo la kuimarisha safu ya utendaji. Pia tumechukua hatua kuharakisha mchakato wa kujaza zile nafasi za Wajumbe wa Bodi za Taasisi hizo mbili ambazo ziko wazi na ninavyosema hivi sasa majina yako kwenye vyombo husika kwa ajili ya upekuzi kwa sababu ni muhimu hili jambo liweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha ufuatiliaji wa mizigo ambayo inakwenda nchi za nje, napenda niseme tu kwamba Serikali imeendelea kufanya jitihada kufuatilia *transit cargo*. Najua kuna upungufu lakini tumefanya jitihada kubwa, Serikali ilianza kitengo cha kupambana na magendo kwa kushirikiana na kikosi maalum ambacho huwa kinafuatilia mizigo kwenda nje ya nchi, tunakiita *Rapid Response Team*. Pia tumekiongezea vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari.

Kwa magari yanayokwenda nje, yale ya mizigo tunayafunga ving'amuzi maalum ili tuweze kufuatilia na kuhakikisha kwamba kweli hiyo mizigo inafika.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na ule utaratibu wa *single customs territory* ambapo bidhaa ambazo zinakwenda nje ya nchi zinatengenezewa kadhia ya forodha ili kusudi sasa kodi stahiki iweze kulipwa katika nchi husika kabla ya kusafirisha ile mizigo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, labda la mwisho, naona kengele imeshapigwa...

**SPIKA:** Kuna la *TRA*, hili la...

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Kuhusu *TRA* kwanza naomba nisisitize, kwa kweli chini ya utawala wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, *TRA* imefanya vizuri sana katika kukusanya mapato. Kwa kweli kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi mpaka shilingi trilioni 1.5 hivi sasa, ni kazi kubwa sana. Ndiyo ukweli, kwa hiyo, hatujashindwa kukusanya mapato. *This is on record. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosema ni kwamba kwenye maeneo yale ambayo imesemwa kwamba tunashindwa kukusanya *tax arrears* upande wa forodha, zile shilingi bilioni 303, nafikiri tutalifanyia kazi vizuri. Nadhani shida iko kwenye; kwanza, kuna *Post Clearance Audit* ambazo zinaweza zikazaa *tax arrears*. Vile vile kuna kulinganisha taarifa zilizopo kwenye *manifest* na zile ambazo zinaenda kwenye ukaguzi wa mafuta, hapo napo kuna kuwa na *discrepancy*.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo linaweza likazaa *tax arrears* ni totaafi kwenye taarifa ambazo zinahitaji *reconciliation* ili tuweze kuona zile ambazo ni *unvalidated* na zile ambazo ni *unpaid declarations*. Sasa hizi zinahitaji



kuwianisha taarifa, nafikiri shida iko hapo na *I would be very much interested*, shilingi bilioni 303 hakika ni fedha ambazo Waziri wa Fedha ningeshangilia sana ningezipata leo, shida iko kwenye *reconciliation* ya hizi kwenye *documentation* tofauti.

Mheshimiwa Spika, niwaahidi kabisa kwamba tutaendelea kuzichambua, *it is in the interest* ya Serikali na Wizara yangu kuhakikisha kwamba *arrears* hizi zinazokusanyika tunazikusanya haraka iwezekanavyo. Baada ya maelezo hayo, nakushukuru tena kwa nafasi. Nitaleta taarifa kwa maandishi tukieleza vizuri katika maeneo mbalimbali.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, tunakushukuru sana. Umepitia kwa kweli hoja zote ambazo zilikuwa zinakuelekea. Tumalizie na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, una hoja mbili tu hapa; Mkulazi na *PSSSF*, karibu sana Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami labda nianze kwa kukupongeza sana kwa kutuongoza vyema katika shughuli za Bunge. Katika kipindi hiki cha miaka mitato umeacha viwango vilivyotukuka kabisa kwa kuongozo Bunge vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuwapongeza Viongozi wetu Wakuu na hasa Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niungane tu na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri wenzangu ambao wamesema viwango vya utendaji wa Mheshimiwa Rais wetu kwa kweli vimetukuka ndani ya nchi yetu na nje ya mipaka ya nchi ya Tanzania. Kwa historia ya miaka hii mitano nadhani nchi yetu imeweza kuwa ni nchi maarufu sana ulimwenguni kwa sababu ya uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe tu Watanzania tumwombe afya njema, lakini sina shaka

uchaguzi wa mwaka huu kwa kweli Mheshimiwa Rais wetu nadhani anayo stahili kubwa sana ya kushinda kwa kishindo kikubwa kweli kweli kwa kazi nzuri aliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nina hoja hizo mbili lakini nianze kwa kumpongeza CAG, amefanya kazi yake vizuri. Nawapongeza sana sana Kamati ya PAC, Mwenyekiti wake, dada yangu Mheshimiwa Kaboyoka na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aeshi na Wajumbe wote wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi walioufanya kwa kweli ni uchambuzi mahiri kabisa na kwa upande wetu sisi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu hoja ambazo wamezileta ni hoja mbili kama ulivyozisema pamoja na michango mingine ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wamezungumzia masuala ya madeni ya mifuko hii naomba kuwahakikishia kwamba Serikali imeanza kuyarejesha hayo madeni na mifuko imeanza kupokea fedha. Kwa hiyo, Serikali imetekeleza wajibu wake na Wizara ya Fedha wanalifahamu vizuri jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya ya kwanza ya Kamati ni ile hoja Na. 3, kifungu kidogo cha 3.9, ambacho Kamati imeagiza Serikali kuhakikisha kwamba Mfuko wa PSSSF itakapofika Septemba, mwaka huu 2020 uwe umeshakamilisha suala zima la *actuarial valuation* kwamba tumeshafanya tathmini ya Mfuko. Naomba kupokea mapendekezo haya ya Kamati ya PAC. Naomba nisema kwa kweli PAC kwa kushirikiana na CAG wameliona jambo la muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye tamko la kisera sehemu ya sita linaangiza kabisa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ni lazima iwe nafanyiwa *actuarial* kila baada ya muda kujua thamani ya mfuko na uendelevu wa mfuko. Sheria Na. 2 ya mwaka 2018 ambayo iliunda Mfuko huu wa PSSSF, imetamka kabisa, kila baada ya miaka mitatu ni lazima mfuko huu ufanyiwe tathmini.

Mheshimiwa Spika, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwa kukubaliana na agizo hili la Kamati na CAG, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli yenyewe kabla ya kuunganisha hii mifuko iliamua kwamba mwaka mmoja kabla ni lazima tathmini ifanyike na mwaka mmoja baadaye ni lazima tathmini wa huu mfuko baada ya kuwa *merged* lazima ufanyike. Kwa hiyo, ndiyo maana nakubaliana na pendekezo hili la Kamati na ni lazima tutalisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwahaikikishie Waheshimiwa Wabunge, kazi kubwa ambayo tulikuwa tunataka ifanyike kwanza ni hii aliyoifanya CAG ya ukaguzi wa fedha katika mfuko. Baada ya kazi hii kuwa imekamilika, kwa sababu mwaka mmoja wa mfuko ulikamilika mwaka 2019 lakini sasa mwaka huu wa 2020 kabla ya Septemba tutakuwa tumekamilisha hiyo kazi ya *actuarial*. Kizuri ni kwamba tumeshaanza kufanya manunuzi ya mtathmini atakayefanya kazi ya kutadhmini huo mfuko. Kwa hiyo, PAC nawashukuru sana kwa hoja hii ya msingi ili kujua afya ya mfuko huu na kuufanya uwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka historia ya uwepo wa mfuko huu, tuliunganisha mifuko minne, tulikuwa na mifuko mitano lakini minne iliwekwa mahsusi kwa ajili ya kuhudumia wafanyakazi wa Sekta ya Umma. Kwa hiyo, ni lazima tuutunze mfuko huu ili uweze kuwatunza na kuhakikisha Watumishi wa Umma wanapostaafu wanaweza kupata mafao yao. Tukirudi historia ya huko nyuma Waheshimiwa Wabunge wengi mmeisema, tusingependa kurudi huko, ni lazima kuwe na uendelevu.

Mheshimiwa Spika, mnakumbuka tarehe 28 ya mwezi wa Kumi na Mbili mwaka 2018, Mheshimiwa Rais ameniagiza kusimamaia kipindi cha mpito cha kuhakikisha tunakuja na mfumo imara endelevu wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, ambapo kazi hiyo tumeshaianza kwa kushirikiana na wadau watatu kwa maana na Serikali, wafanyakazi wenyewe na waajiri. Tutakamilisha kazi hiyo mwaka 2023 kama tulivyoagizwa.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inakwenda vizuri sana kwa ushirikiano wa karibu na baada ya hapo tutakuwa na Sekta ya Hifadhi ya Jamii ambayo ni endelevu yenye kuakisi mahitaji halisi ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa kuzingatia Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sina shida kabisa na pendekezo hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini pendekezo la pili la Kamati pia lilikuwa ni pendekezo namba 3314. Kwanza kuhakikisha Kampuni ya Mkulazi itekeleze majukumu yake kwa kufuata taratibu. Kama Serikali naomba nikualiane na pendekezo la Kamati; pendekezo la Kamati ni zuri na jema. Linachotaka ni kwamba mradi ambao ni mradi wa kimkakati tuna tatizo la *sugar gap* nchini na mradi huu ulianzishwa ili kusaidia kupunguza hiyo nakisi ya sukari katika taifa letu. Kwahiyo ili nakisi hiyo iweze kushukughulikiwa viziru ni lazima tuhakikishie kwamba mradi huu unafanya kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati imeishauri Serikali kwamba kupitia Serikali yenyewe na *MSSF* tuendelee kufanya uchambuzi wa kina na kupata taarifa za utekelezaji zenye ubora ambazo zitapelekea mradi huu uweze kutumika ili kupunguza lile wingu ambalo linaonekana kwamba tunaweza kwenda na hiyo hasara ya bilioni nane kama ilivyosema na CAG.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kazi hii tunaifanya vizuri, na mpaka sasa kwa kweli tumeshalima, lile shamba limeshashalimwa kwa malengo asilimia kama themanini na tatu, limeshapandwa kwa asilimia themanini na tano; kinachoendelea sasa ni manunuzi ya kiwanda chenye. Kiwanda hicho kama kikishapatikana kwa haraka, kama vile Kamati inavyotushauri basi miwa inaweza kuzalisha kama tani laki moja na saba hivi ambacho itakuwa ni kitu kizuri sana katika kuhakikisha kwamba tunasaidia kuondoa tatizo la sukari nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakubaliana kabisa na Kamati pamoja na hoja ya CAG. Naomba niwahakikishie

Waheshimiwa Wabunge kuwa ofisi yangu na Wizara itaendelea kulisimamia jambo hili kwa ukaribu sana. Ninaomba labda nilialifu Bunge lako Tukufu pale mwanzo tulipoona kwamba kuna ulegevu wa namba moja au nyingine tumefanya mabadiliko makubwa sana ya kiutendaji, kwenye bodi ya *NSSF* yenyewe; lakini pia tumefanya mabadiliko kwenye menejimenti ya kampuni, na tumehakikisha kwamba sana tuwe na kampuni ambayo itasimamia huo mradi vizuri na na ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, labda nimalize kwa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba mawanda ya eneo hili la hifadhi ya jamii katika kipindi hiki cha mpito ambacho tunaendelea nacho yameendelea kuwa na changamoto za namna moja ama nyingine. Hata hivyo kwa kweli naomba niwashukuru sana watendaji wa hii mifuko tunakwenda kupambana nazo na kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, na kama nilivyosema, Waheshimiwa Wabunge wanauliza kuhusu madeni nimesema Serikali imeshaanza kulipa madeni hayo na uhakiki umeshaanza na hazi hiyo inandelea. Lakini vilevile nimeeleza hapa kazi nyingine nzuri ambayo inajionesha hadharani.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuungaisha hii mifuko gharama za undeshaji wa mifuko zilikuwa ni kubwa, kulikuwa na ushindani ambao hauna tija na kulikuwa na matumizi mabaya ya fedha; na ndivyo tunachowaelewa Kamati. Kwasababu miradi ambayo ilikuwa inatekelezwa huko nyuma mifuko hii ilikuwa inawekeza kwenye miradi ambayo haina tija kabisa na ambayo haiakisi uhalisia wa miradi; ulikuwa ni upotezaji tu wa fedha bila sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataka tujitahidi sana kuhakikisha kwamba haturudi kule tulikokwenda ambapo sasa tumekuwa tukijaribu kurekebisha na kuhakikisha kazi ya mifuko hii inakuwa ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuwekeza michango hiyo ili iweze kulipa mafao haya. Na kwa mujibu wa *International Standards* ambazo tunatakiwa kuzifuata mwanachama mmoja anayestaafu

anatakiwa alipiwe na wananchama 25. Ili wale wananchama 25 weweze kumlipia mwanachama mmoja lazima fedha yao iwekezwe. Kwahiyo ili iweze kuwekezwa lazima iwekezwe katika miradi ambayo ina tija na inaweeza ikafanya hiyo kazi nzuri ya kulipa hiyo *pension*. Kwa hiyo tumeendelea kujitahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu mpaka sasa thamani ya mfuko wa *NSSF* kwakweli imeweza kuongozeka kutoka tirioni tatu nukta mbili tano kwa mwaka 2018 mpaka kufika tirioni tatu nukta sita sita kwa mwaka 2019. Vilevile mfuko wa *PSSSF* thamani yake inazidi kuongeza; kwa mfano nimesema masuala ya gharama za uweendeshaji kwa mwaka 2018 *PSSF* ilifika bilioni 129 lakini kwa mwaka 2020 uendeshaji kwenye huu mfuko umeshuka mpaka kufika bilioni hamsini mbili nukta moja nane, kwa hiyo unaona kabisa kazi nzuri inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tukichambua maeneo mbalimbali ya utendaji wa kazi unaona kabisa zoezi hili linakwenda vizuri. Lakini cha msingi ni kuhakikisha kwamba sekta inasimamiwa kwa kufuata sheria, sekta inasimamiwa ili iwe na tija na mwisho wa siku hata kipindi hiki cha mipito ambacho tunaendelea nacho tuje kujenga sekta imara ambayo itakaakisi maendeleo ya taifa.

Mheshimiwa Spika, dogo tu la mwisho, kuna baadhi Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba Serikali iliunganisha hii mifuko kuficha dosari ambazo Serikali inazo. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kama mtakuwa mtakuwa mnakumbuka vizuri siku ya tarehe 1 Mei, 2016 vyama vya wafanyakazi vilimuomba Mheshimiwa Rais kabla hajamaliza miaka mitano aunganishe hii mifuko. Kwahiyo unaona kabisa huu ni utekelezaji wa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kutekeleza yale matakwa ambayo yalikuwa na tija yaliyotolewa na vyama vya wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumeendelea kusimamia sekta hiyo na ninaomba kukuhakikishia tutajitahidi, mifuko hii

ita-*survive*, hakuna mfuko ambao utakufa na wafanyakazi wataendelea kulipwa mafao yao. Tutaendelea kutatua changamoto za ucheleweshaji huo wa mafao na vitu vingine mwingine, tumejipanga vizuri. Ninaishukuru Kamati kuyaona haya mambo mawili tutaendelea kuzingatia utaratibu wa uwekezaji ili uwekezaji uwe na tija kwenye sekta ya jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati, nakushukuru kwa kuniruhusu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Sasa narudi kwa mtoa hoja, na kama nilivyosema kwa vile umeungwa mkono na Bunge nzima sasa robo saa inakutosha kuhitimisha hoja yako. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, na kwa kweli nashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wengi sijaona aliyepinga na ninashukuru hata Waheshimiwa Mawaziri wale waliotupongeza nakuona kwamba kamati yetu imefanya kazi vizuri. Kwa mara nyingine na kwa heshimwa kubwa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu kwa kipindi cha miaka mitano kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naendelea kushukuru kwa kuteua kamati hii ambayo kwa muda wote imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa bila kuingiza mambo ya kichama.

**SPIKA:** Samahani kidogo kwa wale ambao, nilivyosema mwanzo, kwamba wale wanzangu mimi wanaojaribu kupiga kura bila kuwa makini katika hija za kamati, mnaona pale yupo pale Mheshimiwa Mwenyekiti na Makamu wake yupo pale pembeni yake kuonesha jinsi ambavyo ushirikiano huwa ni mkubwa na kazi hii ni kazi ya pamoja. Mheshimiwa Mwenyekiti endelea. (*Makofi*)

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika kuhitimisha hoja Kamati nikushukuru pia kwa namna ulivyoendelesha na kusimamia mjadala huu muhimu wa taarifa ya Kamati. Aidha kwa namna ya pekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati yangu ya PAC; kweli tumefanya kazi kama timu moja kama ndugu, kwa hiyo nawapongeza. Sikuona shida yoyote kuendesha kamati hii wamekuwa watu wameangalia *issues* hawakuangalia u-vyama; ndiyo maana Kamati yetu siku zote imeangalia *issues*, hatukungalia mambo ya vyama, niwashukuru sana. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia mjadala huu na wote wametupongeza; kwa hiyo nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kamati imechangiwa na jumla Waheshimiwa Wabunge 48 na katika idadi hiyo Waheshimiwa Wabunge 38 walichangia kwa kusema hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 10 walitoa michango yao kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Kamati kwa ujumla wamesisitiza umuhimu wa uwajibikaji kwa matumizi ya fedha ya umma. Kwa muhtasari mapitio hayo nitayataja machache maana mengi Mawaziri wameyakubali na Waziri wa Fedha amesema ambayo yamejili katika ripoti hii, hasa tukianza na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Tunachosema ni kwamba kamati inasisitiza kwamba katika azimio lake lililowashauri Serikali kuhakiki bodi ya kuhakikisha ya Rufaa za Kodi na Baraza la Kodi TRAT zinatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari; limeongelewa suala hili kwa mapana na marefu, na tunachosema ni kuhusu mifumo na mikataba. Tunaomba sana Serikali ishughulikie kuhakikisha kwamba ile mifumo inafanya kazi vizuri na mikataba ile inaangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye Shirika la *TANESCO*, Waheshimiwa Wabunge pia wameliongelea sana na tumeona tatizo si *TANESCO*, tatizo ni yale Mashirika ambayo hayalipi. Nipende tu kusema kweli Mheshimiwa Rais alisema wasiolipa wakatwe; lakini twende katika uhalisia je, Muhimbili



inaweza kukatiwa umeme? Hospitali zinaweza kukatiwa umeme? Kama hivyo sivyo basi Serikali kupitia Hazina wahakikishe wanalipa hizi fedha kwa muda maana si kosa la hawa Serikali. Wale watu binafsi wanaweza kukatiwa kwa hiyo tunasisitiza kwamba fedha za Umma ziangaliwe na TANESCO isiweze kufanywa ikashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tukija kuhusu *PRIDE* Waziri amelizungumzia vizuri; kwa hiyo tunasisitiza pendekezo la azimio kwamba Serikali itekeleze mapendekezo na ushauri wa CAG kuhusu kadhaa ya Kampuni hii ya *PRIDE*. Tukija kwenye Shirika la TTCL Kamati imependekeza kufanyika mapitio ya kiutendaji ya Bodi ya *Management* ya TTCL ili kuhakikisha mapungufu yaliyopo yanaondolewa na Kampuni iweze kujijendesha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili la Mkulazi kwa kweli hata Kamati walisikitishwa sana na utendaji wake kuonesha kwamba *PSSSF* walishindwa kuhakikisha Kiwanda kinakuwa *installed* kinajengwa ili tusiwe na mapungufu ya Serikali. Kwa hiyo taarifa ya Kamati imefafanua kuwa hadi sasa uzalishaji wa sukari haujaanza kwa ajili hiyo tunasema kwamba ifikapo 2020 *NSSF* ahakikishe kiwanda kinaanza kazi na sukari inapatikana kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu benki zinazomilikiwa na Serikali. Kwakweli tuseme kwamba Kamati ilisikitishwa sana na utendaji wa hizi benki. Hizi benki zina wasomi, hatuelewi kwa nini wanafanya kazi kwa kiwango cha chini sana. Hata tunaposema zinaunganishwa, tukikumbuka kwamba wenzetu wa *Tanzania Postal Bank* kwa miaka minane mfululizo wamekuwa wakifanya kazi nzuri na *growth rate* imepanda mpaka kufikia asilimia 20 kila mwaka kwa hiyo miaka minane; sasa leo unampelekea mgonjwa mahututi.

Mheshimiwa Spika, , ilipeleka Benki ya Wanawake. Kamati ilivyopitia iliona kwamba ile iliangusha *performance* ya Benki ya Posta. Sasa tena tunampeleka mgonjwa mwingine huyu wa *TID*. Kweli wafanyakazi wa *TID* sijui itakuwaje, maana ukiwapeleka kule ni kwamba umehamisha

ugonjwa kutoka benki hizi kumpelekea huyu Benki ya Posta ambaye alikuwa anafanya vizuri. Tunaomba sana Serikali ilianganalie, kwa nini iwe hivyo, kwa nini wasifutwe ikawa hizi benki ya Posta ikachukua majukumu yake kuliko kuwaunganisha halafu wanashusha *performance* ya benki hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha nje ya bajeti. Mheshimiwa Waziri amejaribu sana kueleza jinsi ambavyo fedha zile zimetumika na akatuhakikishia kwamba aliandika barua lakini hayo yote yalitakiwa yakahakikishwe na kuwa *verified* na CAG.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuendelea kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Makamu wangu Mwenyekiti wa PAC, nimemuona amekaa hapa, ni kwamba tumefanya kazi vizuri kwa kushirikiana ndio maana unaona Kamati yetu haijakuletea migogoro yoyote ya kuripoti kwamba tuna migogoro ni kwa vile tumefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Makamu wangu ambayo imetuletea ufanisi mkubwa sana. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia na leo sikuona uvyama nilichoona mmeona Bunge limefanya kazi yake ya kuisimamia Serikali. Na kwa kweli tunamshukuru sana CAG na Ofisi yake, Wafanyakazi wake wote. Wametufanyia kazi nzuri sana, na kwakweli Mheshimiwa Kichere amekuwa muwazi, hata ile sehemu ambazo tuliambiwa Mikataba hii haitaletwa alituletea. Kuonesha kwamba hana usiri wowote katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge na Wajumbe, wenzangu mmeshawashukuru, wa Kamati yetu ya PAC. Nimshukuru Katibu wa Bunge na Sekretarieti ya Kamati kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, nikishukuru Chama changu CHADEMA ambacho kwa kweli wasingenileta hapa Bungeni, msingeona utendaji wangu wa kazi. Nishukuru sana hasa kikiongozwa na Kiongozi wetu

Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa vile ndio aliniteua mpaka nikaenda nikachaguliwa; na Mheshimiwa Spika nilivyokuja ukaona nafaa kuwa kwenye Kamati hii, na nafikiri umeona kwamba kweli kazi hii tumeitendea haki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge likubali mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Taarifa ya CAG kwa Hesabu zilizokaguliwa na Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati, kwa kutoa hoja kwamba Bunge likubali maoni na mapendekezo ya Kamati kama mliyoyawasilisha na hoja yako imeungwa mkono na kwa kumbukumbu zangu hapa karibu Waheshimiwa Wabunge wote wameafiki. Kwa hivyo walioafiki wameshinda. (*Makofi*)

Walioafiki wameshinda na hata ambao walikuwa wamepiga hapana, ni kwa sababu mfumo wetu bado unahitaji kuboreshwa ili mtu akikosea aweze kurekebisha. Sasa hivi bado uko *rigid* ukikosea inabaki pale pale. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kwa kweli kuwapongezeni sana Kamati ya PAC. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kamati ya PAC ndio katika historia ya Mabunge ndio Kamati namba moja kutoka enzi hizo Mabunge yalipoanza kuunda Kamati za kufanyia kazi Kamati ya kwanza ilikuwa ni Kamati ya PAC; na kwa sababu ya jukumu lile la Bunge kuwa jicho la kutazama namna ambavyo bajeti wanayokuwa wameidhinisha sasa matumizi yake nayo yameenda kufuatana na bajeti ile na kwamba hakuna ufujaji

wowote wala matumizi yoyote mabaya. Kwa hiyo imekuwa na historia hiyo; wenzetu hawa wanaiita *Watch Door Committee*; kwa hiyo ni Kamati muhimu sana katika nchi yoyote.

Zinakuwa na mamlaka tofauti tofauti na madaraka tofauti tofauti lakini ni Kamati muhimu sana. Hapa kwetu inaangalia mahesabu ya Serikali Kuu na inaangalia pia mahesabu ya Mashirika yote ya Umma, na hasa yale ambayo Serikali ina Hisa ya asilimia 50 na kwenda juu. Ndio tukaunda *PIC* ya kuyaangalia Mashirika ya Umma ambayo Serikali hatuna *majority share*. Ili pia yasije yakasahaulika kwa sababu miaka ya nyuma hayo yalikuwa hayaangaliwi kabisa; na *PIC* imetusaidia sana, sana katika upande huo pia ku-*revive* huko na kupiga tochi nini kinachoendelea kule kwa kiasi fulani.

Kwa hiyo tunawashukuruni sana *PAC* kazi yenu ni ngumu, ina mambo yake, unajua mambo ya fedha tenda yana mambo yake lakini mmejithahidi sana. Mmefanya kazi kubwa sana katika miaka mitano, kwa kweli mna historia kubwa ya kuiandika. (*Makoff*)

Mmetusaidia sana katika kuwaamsha na kuwaweka sawa wale ambao walikuwa hawaendi sawa. Nakumbuka wakati fulani walikuwa wameitwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, chuo ambacho sehemu kubwa ya mlioko hapa mliopita elimu hiyo mmesoma hapo maana ndicho Chuo anzilishi. Sasa ile *Management* ya Chuo ikawa imeitwa hapa pamoja na Bodi yake walikuwa hawajaweza kufunga hesabu mfululizo sijui miaka mitatu ile kama sikosei. Sasa tukawa tunawashangaa nyie ndio mnawafundisha Wahasibu, Mameneja wa Fedha, wakina Dkt. Mpango ndio wamefundisha huko na wengine wengi wamekuwa walimu huko. Sasa nyie mbona ndio mnakuwa mfano mbaya mwaka wa kwanza, mwaka wa pili, mwaka wa tatu.

Halafu hesabu zenyewe sasa sio kwamba tu walikuwa hawajaweza kuzifunga ili *CAG* akague, yaani zilikuwa hazifungiki jinsi zilivyokuwa shagala bagala. Mwisho wakasema bwana sisi kazi yetu ni kufundisha sie habari ya

kufunga mahesabu hatujui sisi. Tukawaambia wapi hela ya Umma bwana hiyo lugha hiyo hamuwezi kutuambia, ilikuwa kasheshe. Tuliita karandinga hapa kuja kubeba Maprofesa, ilikuwa shughuli pevu.

Watu sukari zikapanda, presha na mengine mengi, nikielezea leo kasheshe za miaka mitano ni nyingi. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana, na kwa maana hiyo Bunge hili limefanya kazi kubwa sana. Tumeisaidia Serikali, tumesaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba usafi huu tunaouona katika Serikali na sisi tumechangia sana katika kuweka fagio la chuma na kuweka misingi ya utendaji kazi; jambo ambalo tunapaswa kujipongeza sana asana sana. (*Makofi*)

Tunakupongeza sana CAG Mheshimiwa Kichere kwa kazi nzuri na Wasaidizi wako wote Ofisini. (*Makofi*)

Na Kamati wenyewe wamesema na tunaomba tuendeleo kuwa nawe kesho na keshokutwa kwenye Taarifa ya LAAC ambapo kazi yako pia bado tunaendelea kuipokea na kuitazama. Kwa kweli Ofisi ya CAG imetulia inafanya kazi vizuri sana. Na ninyi wenyewe mmesema hapa, kule tulikotoka nadhani tumevuka mto Jordan. Sasa tunaelekea kwenye nchi ya ahadi, yale mambo ya kudharauliana yale yamepita. Na ndiyo shida ya sisi wengine unajua watu wengine hawanifahamu vizuri.

Mimi si mgomvi na ukiona naparangana na mtu kanichokoza, mimi sianzishagi vagi hata siku moja; lakini sasa ukinichokoza ooo! sasa hapo! tena nikagundua unanichokoza makusudi! Hapo inakuwa tabu. Maana unaweza ukamchokoza mtu bahati mabaya, inakuwa shida.

Lakini tunamshukuru Mungu yote ni mema na bahati nzuri mbichi na mbovu zimejulikana. Ni sehemu ya Miaka mitano, kelele nyingi, uongo mwingi lakini mwisho wa siku heshima ya Bunge hili lazima isimame maana ndio wawakilishi wa wananchi hivyo ni lazima lipewe nafasi yake na liheshimike, haiwezi kuwa ni *punching bag* ya kila mtu anaropoka anavyotaka, haiwezekani. (*Makofi*)

Basi baada ya shukrani hizo Waheshimiwa Wabunge nanyi mtaona namuda wetu ndio huo, tunashukuru tumeshavuka Mwezi Mtukufu wa Ramadhan bado wachache wetu wapo kwenye Sita Shwari tunawatakia kila la kheri; kwa hiyo sasa hivi tunaweza tukaenda hata baada ya saa kumi na mbili, hata masaa kadhaa baada ya hapo, na hasa baada ya hizi siku sita hizi mtakuwa hakuna anayefunga; kwa hiyo tuko *free* zaidi kuliko tulikotoka. Tulikuwa tumeweka saa kumi na mbili kwa sababu ya Kwaresma na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Lakini Mabunge mengi yanayoanza saa nane mchana huwa yanaweza yakaenda mpaka saa sita usiku. Kwa hiyo huu ni mwanzo tu lakini kwenye Bunge la kumi na mbili endapo utaratibu huu utaendelea, itakuwa hivyo. Au kama utarudia ule wa mwanzo bado ni nyinyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge mtakaoamua. Sasa hivi tunapitia Kanuni zetu za Bunge ili kuona utaratibu unaokuja uweje; na kwa kweli tunahitaji ushauri pia wa tushauri vipi kwenye Kanuni wa Bunge linalokuja kuhusiana na muda wa Bunge. Je, hii *practice* tuliyofanya inapendeza au mazoea yetu yalikuwa ni mazuri zaidi kule tulikotoka? Tutahitaji sana ushauri kabla ya Bunge hili kwisha tutapitisha hizo Kanuni mpya zitakazotumika kwenye Bunge lile linalokuja. Na hilo ni mojawapo ya eneo ambalo ni vizuri tukaliangalia na kushauriana kwa haraka haraka vizuri, tuone njia ipi ni nzuri zaidi.

Ukichunguza unaona kama njia hii ya sasa hivi ya Kibunge zaidi. Ile ya zamani ya kiuanafunzi zaidi. Saa tatu asubuhi Mbunge ushafika hapa hata wapiga kura hujawapigia simu hata Waheshimiwa Mawaziri Ofisini hawaendi, inakuwa tabu tu. Lakini kama ndio utaratibu mzuri ule tutarudi tu huko wala hamna shida, mtakaoamua ni nyinyi wenyewe.

Nina matangazo tu mawili na yote yanatoka kwa Katibu wa Bunge. Anasema kwamba katika kuimaeisha mifumo ya hapa Bungeni na hasa baada ya *Covid -19* kujitokeza na kwa maana ya hiyo tukasema kuanzia sasa

kwenda mbele mambo ya kupiga dole, mnanielewa nikisema hicho Waheshimiwa Wabunge, hayawezakani tena na mambo ya ku-*log in* na yenyewe yana taabu zake, yana changamoto zake. Sasa mfumo umeshafungwa na ni wa uhakika, ambao ni wa *facial recognition*. Mfumo huu hauhitaji Mheshimiwa Mbunge kugusa mahali popote na badala yake kutakuwa na mashine za utambuzi kwenye mageti yetu yote, na tutatakiwa kutoa ushirikiano kidogo pale unapoanza mfumo huu.

Kwa hiyo inatupa uhakika si kwa Waheshimiwa Wabunge tu lakini mtu yoyote anayeingia humu Bungeni kuweza kuweka kumbukumbu halisi za nani amefika na nani ameondoka. Kwa hizo siku zijazo wala hakutakuwa na hili jambo la mimi nilikuja lakini haikuwa sijui kumbukumbu zimefanyaje tunazidi kwenda ki-*digital* zaidi kwenye kila jambo. Kwa hiyo wewe ukipita pale basi wewe mambo yako yote sisi tumeshajua na kila kitu kinakaa kinavyotakiwa kuhusu utaratibu.

La pili ni kwamba bado wako Waheshimiwa Wabunge ambao wanaomba *exemption* ya kodi ile ambayo tunastahili katika miaka mitano, hasa kwenye masuala ya magari tunayoyaagiza au tuanayo yanunua. Sasa msamaha huo wa kodi TRA wameijulisha ofisi yangu kwamba muda wa kufanya hivyo umesha- *expire* kwa kanuni zao. Kwa hiyo wale wote ambao hamjatumia *privilege* hiyo nikiwemo na mimi basi dirisha limeshafungwa hilo. Kwa hiyo msituletee ofisi maombi ya kuwaidhinishia mpeleka karatasi zetu TRA kwa ajili ya *exemption* ya gari lolote kati ya sasa na kumalizika kwa muda wetu siku si nyingi zijazo natumaini tumeelewana.

Kuna Waheshimiwa Wabunge bado wanaleta kuomba *exemption* kuna kanuni ambazo zinataka *exemption* ya gari ambalo unaliombe *at least* ulitumie kwa kazi hiyo kwa kipindi fulani. Sasa ukitazama muda wa sasa na kumalizika kwa muda ni kama vile haitakuwa hivi kwa sababu hizo ni kanuni basi naomba niwatangazieni na mzingatie msitulee maombi ya *Tax Exemption* ya magari, tsubiri tukaombe

Mungu kwa wapiga kura kama utarudi basi utaanza nayo hiyo *exemption* awamu nyingine kuanzia Novemba.

Basi Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa shughuli zetu zimekamilika naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 12:11 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 27 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*